

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 27 Aprili, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. MARYAM OMAR SAID (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu!

NDG. ASIA MINJA– KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba sasa aulize swalii lake.

Na. 97

Ukamilishaji wa Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli

MHE. ISSA J. MTEMVU aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli utakamilika pamoja na kuhakikisha Kituo hiki kinafanya kazi kama kilivyokusudiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mabasi cha Magufuli kinachoendelea na ujenzi katika eneo la Mbezi Luis Kilianza ujenzi Januari, 2019 kwa mkataba wa miezi 18, hivyo ujenzi ulipaswa kukamilika Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi aliongezewa muda wa ujenzi hadi Juni, 2022 kutokana na kuchelewa kutolewa kwa msamaha wa kodi wa vifaa vyaa ukamilishaji wa ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi, 2022, kiasi cha shilingi bilioni 53.09 sawa na asilimia 94.73 zilikuwa zimelipwa kukamilisha ujenzi. Aidha, tarehe 14 Machi, 2022, Serikali imetoa msamaha wa kodi na sasa Mkandarasi anaendelea na manunuvi ya vifaa ili kazi ya ujenzi iendelee na kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2022. Kukamilika kwa kazi hizo kutafanya kituo hicho kutoa huduma kwa wananchi kama ilivokusudiwa.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na ya kuridhisha ya Serikali ningombaa kuuliza haya maswali mawili. Moja, stendi yetu ya Magufuli inaruhusu kuingiza mabasi yote yanayotoka mikoani bila kwenda kokote na kushusha pale abiria, lakini pamekuwepo bado na mabasi mengi kwenda Urafiki na maeneo ya pale kwa Wachina na Maghorofani. Pamoja na maelekezo mengi yanayotolewa na viongozi wa mkoa na wilaya. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kushindwa kwa muda mrefu kusimamia maelekezo yake?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, ni ukweli stendi ile pamoja inaenda kukamilika kwa wachache walioingia kuitia mnada wanalipa *square* mita au mita za mraba Sh.40,000 tofauti na maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam ikiwepo hata maeneo ya pale Mlimani City, kati ya shilingi 15,000 hadi shilingi 25,000, lakini hawa wanalipa shilingi 40,000.

Je, Serikali haioni sasa ni sababu ya kupunguza kufikia hiyo kati ya shilingi 15,000 hadi shilingi 25,000 ili matumizi yaende kama yalivyokusudiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mtemvu kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Kibamba na nimwakikishie Serikali itaendelea kumpa ushirikiano ili aweze kutekeleza miradi mbalimbali ya wananchi wa Kibamba. Kuhusu mabasi ambayo hayaingii kwenye stendi ya Magufuli, ni kweli kumekuwa na baadhi ya makampuni ambayo hayatumii ipasavyo stendi kadri ya maelekezo na malengo ya ujenzi wa stendi ile. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunalichukua hilo tunalifanyia kazi na tutatoa maelekezo mahususi kuhusiana na utaratibu wa mabasi kutumia stendi ile ya Magufuli.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na gharama ya upangishaji kwa *square* mita kufika hadi Sh.40,000 mapendekezo yake ni Sh.15,000 hadi Sh.25,000 naomba niseme tunalichukua hilo kama Serikali tatalitazama na tuweze kuona mazingira kama yanaruhusu basi tuweze *ku-review* bei hizo ili wananchi wapate unafuu katika upangishaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mkoaa wa Songwe ni mionganii mwa mikoa mipyaa na mpaka sasa hatuna stendi ya mkoaa, tayari fedha zilishatengwa. Naomba kufahamu nini mkakati wa Serikali katika kutupatia hizo fedha bilioni 29 ili tuweze kujenga stendi ya mkoaa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoaa wa Songwe kwa sababu ni mpya hauna stendi ya mabasi ya mkoaa na kama alivyosema Mbunge Serikali tayari imeshaweka mpango wa kujenga stendi ya mabasi ya Mkoaa wa Songwe na imeshatenga fedha. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba kazi iliyopo sasa tunatafuta fedha ili twende kujenga stendi ya kisasa ya Mkoaa wa Songwe.

SPIKA: Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa stendi ya Mbezi ni mionganii mwa miradi ya kimkakati inayosimamiwa na TAMISEMI. Je, ni lini mradi wa kimkakati wa Soko la Mlandizi utajengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya maeneo yote ambayo yanahitaji kujengewa stendi za kimkakati ikiwepo Halmashauri ya Kibaha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tushaelekeza halmashauri walete andiko walishaleta na najua kulikuwa kuna mazungumzo ya eneo wapi tujenge ile stendi. Nikuhakikishie kwamba TAMISEMI tunaendelea na kufanya tathmini ya mapendekezo ya halmashauri ili twende kujenga stendi ile na tutafanya hivyo mapema iwezekanavyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Naomba kuuliza kwa kuwa akinamama wa Mkoa wa Dar es Salaam wengi ni akinamama lishe na wanafanya shughuli ndogondogo, lakini katika eneo hilo hilo la stendi ya Mbezi bado kuna eneo kubwa ambalo Serikali inaweza ikawajengea vibanda vidogo vidogo. Je, Serikali haioni haja hata kwa kutumia Mfuko wa Akinamama ile asilimia yao kuwajengea mabanda rahisi ya kuweza kufanya kazi zao, akinamama wote wa Mkoa wa Dar es Salaam? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunahitaji kuboresha maeneo ya wafanyabiashara wadogowadogo na ndio maana Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ameelekeza kuboresha maeneo ya wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo akinamama ntilie lakini pia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

machinga na wafanyabiashara wengine. Nimpakishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la Mbezi ambalo anasema lina nafasi ya kujenga tutakwenda kulitazama ili tuone uwezekano wa kuwekeza hapo. Wazo lake la kutumia asilimia 10 pia tutalifanya tathmini kuona au kutafuta chanzo kingine kwa ajili ya ujenzi huo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 98

Hitaji la Vifaa Tiba Hospitali ya Iliongero na Vituo vya Afya – Halmashauri ya Wilaya ya Singida

MHE. ABEID R. IGHONDO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba katika Hospitali ya Iliongero pamoja na Vituo vya Afya vya Msange na Mgori Wilayani Singida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali ilipeleka Bohari Kuu ya Dawa Shilingi Bilioni 34 kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba. Tayari Vifaa Tiba vimeanza kusambazwa kwenye Hospitali 67 za Halmashauri ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambayo imekwishapokea vifaa vya aina 17 vikijumuisha vifaa vya upasauji na maabara.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshishimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vitakavyopelekwa kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizokamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Abeid Ighondo, swali la nyongeza.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya kutia matumaini ya Serikali awali ya yote kwanza nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini kufatia ajali mbaya iliyotokea juzi na kuuwa wananchi wanne hapo hapo na majeruhi 20 lakini hawakuweza kupatiwa matibabu kwa wakati na ipasavyo kwa sababu ya kukosa vifaa tiba katika hospitali zetu. Lakini...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge ngoja tuelewane vizuri, kwanza ni kipindi cha maswali, pili unaongeza hoja hapo kwamba hawakupatiwa matibabu, hiyo ni hoja nzito sana, unao ushahidi ama huna? Kama huna hebu jielekeze kwenye maswali ondoa hiyo habari nyingine kabisa, kwa sababu tusije tukahama kwenye maswali tukaelekeea kuanza kushughulika na hiyo hoja kwamba walifariki kwa sababu hawajapatiwa matibabu, hiyo ni hoja nzito sana kuletwa hapa Bungeni.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, ni lini tutapatiwa *ambulance* katika hospitali hizi ili kurahisisha huduma kwa wananchi wetu wanaopata magonjwa mbalimbali na mengine ya ghafla kama ajali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini sasa Serikali itapeleka watumishi wa kutosha katika vituo hivi vya afya pamoja na hospitali ya wilaya ili waweze kutoa huduma kwa wakati na ipasavyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la *ambulance* katika bajeti inayokwisha mwaka huu tarehe 30 Juni, Serikali imetenga magari ya wagojwa 195 na kila halmashauri itapata gari la wagonjwa ikiwepo halmashauri ya Singida ambayo tutapeleka kwenye hospitali hii. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba suala hilo tayari linafanyiwa kazi na gari ya wagonjwa itapelekwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na watumishi ni kweli tuna upungufu wa utumishi, lakini Serikali imetoa kibali tayari hivi sasa vijana wanaendelea kuomba ajira ya watumishi wa kada mbalimbali za afya 7,612 na miongoni mwa watumishi hao watapelekwa katika Wilaya ya Singida.

SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgatu, swali la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeleta milioni 500 kumalizia ujenzi wa Hospitali za Halmashauri ya Kibiti, Kibaha Mjini, Kibaha Vijiji na bilioni moja Halmashauri ya Chalinze. Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa wananchi wa maeneo hayo juu ya kuleta vifaa tiba kwa wakati ili iendane na jitihada hizi za uwekezaji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Subira Mgatu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya kwa wananchi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kibiti na wananchi wa Chalinze imepelekwa jumla ya shilingi bilioni moja na milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na hospitali. Hata hivyo, nimhakikishie mara baada ya kukamilika kwa vituo hivi Serikali itapeleka vifaa tiba kwa sababu katika bajeti ya mwaka ujao shilingi bilioni 69.95 imetengwa kwa ajili hiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba na watumishi katika zahanati ya Mwashilalage katika Jimbo la Sumve ambayo ujenzi wake umeshakamilika kwa muda sasa na mahitaji ya watumishi na vifaa tiba ni ya hali ya juu kutokana na kwamba kata nzima ya Sumve haina zahanati yoyote?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Jimbo la Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vifaa tiba na watumishi vyote viko kwenye mpango na viko tayari. Watumishi wanaendelea kuajiriwa hivi sasa na matarajio ya Serikali ifikapo Julai, watumishi watapelekwa kwenye vituo vyetu na tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwenye zahanati ambayo Mheshimiwa Mageni Kasalali ameongelea.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na vifaa tiba mwaka ujao wa fedha tumetenga 69.95 bilioni kwa ajili ya vifaa tiba na tutahakikisha pia vinapelekwa kwenye zahanati hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Kasaka swali la nyongeza.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya cha Chalangwa kimekamilika muda mrefu pamoja na jengo la Mochwari limekamilika, lakini mpaka sasa hivi hakuna majokofu wala vifaa tiba: Je, Serikali inatuhidi nini kupeleka vifaa tiba hivi pamoja na jokofu kwenye Kituo cha Afya cha Chalangwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Chalangwa kimekamilika na ni mionganini mwa vituo afya ambavyo vimetengewa fedha ya vifaa tiba mwaka ujao 2022/2023 ikiwemo jokofu kwa ajili ya chumba cha kuhifadhi maiti.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 99

**Kubadili mtambo unaotengeneza hewa ya naitrojeni
Kituo cha Afya Upuge**

MHE. ATHUMANI A. MAIGE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itabadilisha mtambo wa kutengeneza hewa ya Naitrojeni Kituo cha Afya Upuge na kuleta mtambo wa hewa ya *Oksijen*?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Upuge kilifungiwa mtambo wa kutengeneza *vacuum* mwaka 2012 kwa ajili ya huduma za dharura na upasuaji. Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imefanya tathmini ya mitambo hiyo na matengenezo madogo ya kuzibua njia ya hewa yatafanyika illi iweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kununua mitambo 10 ya kuzalisha hewa ya Oksijeni. Mitambo hiyo itazalisha hewa na kusambaza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo Kituo cha Afya cha Upuge ambacho kimefungiwa mfumo wa kupokea na kutawanya hewa ya Oksijeni. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige, swalii la nyongeza.

MHE. ATHUMANI A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swalii la nyongeza. Katika kituo hicho pia kuna mtambo mkubwa wa kufua nguo ambaao *screen* yake au kisomeo kiliharibika wakati mtambo unapelekwa kwenye *site*: Je, Serikali iko tayari kuleta *spare* nyingine ili kituo kile kiweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; katika kituo kile pia kuna mtambo mkubwa wa *X-Ray* ambaao haufanyi kazi kwa sababu hakuna jengo la kufunga mtambo ule: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusafiri na mimi kwenda huko

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Upuge ili tukaone ufumbuzi wa kupata jengo jipya la kufunga mionzi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mtambo wa kufua nguo ambao umeharibika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafanya tathmini ya mahitaji kwa maana ya gharama, lakini tutaona kati ya fedha ya mapato ya ndani na kutoka Serikali Kuu ipi inaweza ikatumika kuhakikisha mtambo huo unafanya kazi au tunanunua mtambo mwininge.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Jengo la *X-Ray*, kwamba *X-Ray* ipo lakini hakuna jengo, naomba tulichukue suala hili tukalitazame. Pia nitoe wito kwa Halmashauri ya Tabora kuanza kuona uwezekano wa kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga jengo la *X-Ray*, kwa sababu tayari kuna mtambo na wana mapato ya ndani, wanaweza wakatenga kwa awamu kujenga jengo hilo ili tuweze kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge tukapitie eneo hilo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa tuingie Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, lakini tutaelekea Wizara ya Mifugo na Uvuvi halafu tutarejea na mtitiriko wa maswali yetu ili kumpa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kujibu maswali yake, kwa kuwa ana Mkutano.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 106

Kusaidia vikundi vya Uvuvi - Mtwara Mjini

MHE. HASSAN S. MTENGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasaidia vikundi vya Uvuvi katika Jimbo la Mtwara Mjini ?

SPIKA: Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wavuvi kuunda vyama vya ushirika pamoja na kuvunganisha na taasisi mbalimbali za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kuboresha shughuli zao za uvuvi, kukuza uchumi wao binafsi na Taifa ambapo hadi sasa kuna jumla ya vyama vya ushirika 170 nchi nzima. Kati ya vyama hivyo, vitatu viko katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara imetoa mkopo wa shillingi milioni nane kwa Kikundi cha Uvuvi cha Kaza Moyo Mtwara kwa ajili ya kununua injini na nyavu. Aidha, kuitia mradi wa unaoratibiwa na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi kwa maana ya FETA, ufadhili wa UNDPKikundi cha NASARC cha Mtwara Mjini na Kikundi cha wanawake cha Umoja ni Nguvu na chenyewe ni cha Mtwara Vijiji, vimejengewa jumla ya mabwawa 13 ya kufugia samaki wa maji baridi. Jumla ya wanufaika wa mradi huu ni wananchi 140 kutoka katika Vijiji vya Msanga Mkuu, Kijiji cha Mtawanya, Msijute na Mikindani. Mradi huu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

una thamani ya bilioni moja. Vilevile mradi umelipia ghamama zote muhimu za uzalishaji ikiwemo kununua vifaranga na chakula cha samaki hadi kuvuna.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu unayosoma hapo mimi sina. Sijui kama wamekubadilishia ama wamefanyaje hao wataalam, lakini majibu uliyoyasoma hapo, mimi sina. Majibu niliyonayo hapa ni tofauti na uliyosoma.

Mheshimiwa Hassan Mtenga, swalii la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa kunipa majibu yake mazuri sana ambayo nimeyapokea.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ndiyo Jimbo ambalo linazungukwa na bahari. Kwa namna moja au nyingine, vijana wengi wa Mtwara Mjini shughuli zao zinahusika kwenye bahari: Je, ni lini Serikali itanihakikishia kwenye vikundi zaidi ya 30 ambavyo tuliahidiwa kwamba vitapata vitendea kazi, nyavu na vitu vingine, vitasaidiwa? Nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Tunazungumzia bahari kama bahari: Ni lini Serikali itatuletea meli ya uvuvi ili vijana hawa waweze kupata ajira na samaki ambao wanapotea kwa njia bahari tuweze kunufaika sasa Tanzania kama nchi? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwanza naomba radhi kwa kutokupata majibu haya kwa ufasaha katika meza yako. Naomba nikauhidi kwamba tutafanya marekebisho ya utaratibu huu usirejee tena.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kwanza kwa kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya hasa ile niliyotangulia kujibu katika jibu la msingi la kuwavuta wawekezaji na kukubali kuwasaidia wana-Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tutawasaidiaje vijana katika vikundi hivi 30 alivyovitaja waweze kununua nyavu na injini; matarajio yetu katika bajeti inayokuja ya 2022/2023, tunao utaratibu mzuri ambao tutakaposoma bajeti yetu, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wengi, wataona matumaini makubwa ambayo yataenda kujibu swali hili la Mheshimiwa Mtenga. Kwa hiyo, ni matarajio yetu katika mwaka ujao wa fedha, viko vikundi vya vijana vitakavyopata fursa ya kwenda kupata mikopo nafuu ambapo wataweza kununua nyavu na injini.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni juu ya ununuzi wa meli ambazo zitatoa pia ajira kwa vijana. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ina mkakati mzuri wa kwanza kwa kujenga Bandari ya Uvuvi. Bandari ambayo itajengwa katika Mji wa Kilwa Masoko. Vilevile tunayo bajeti ya kwenda kununua meli za uvuvi zipatizo nne. Meli hizi zitakwenda kuajiri vijana wa Kitanzania wakiwemo vijana kutoka katika Jimbo la Mheshimiwa Hassan Mtenga, kwa maana ya pale Mtwara Mikindani. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Asya, swali la nyongeza.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ajali nyingi za wavuvi zinazotokea baharini husababishwa na utabiri wa hali ya hewa: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia taarifa za dharura wavuvi wetu kabla ya kuingia baharini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni jema na zuri, tumekwishalianza. Kupitia Taasisi ya yetu ya Utafiti ya *TAFIRI* tumetengeneza programu maalum ya kuwasaidia wavuvi, inayoweza kuwalishia juu ya makundi ya samaki mahali yalipo. Pia programu hii itaenda mbele, itawasaidia kwenye kufafanua pia na hali ya hewa. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunaendelea nalo hivi sasa na tunalieneza ikiwa ni pamoja na elimu yake ili liweze kuwafaidisha wavuvi wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai sasa aulize swali lake.

Na. 100

Kufufua Shule za Msingi za Ufundı - Hai

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafufua Shule za Msingi za Ufundı Wilayani Hai na kurejesha mfumo wa wanafunzi kufanya mitihani na kupewa vyeti?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mkenda, majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elinikyo Mafuwe Saashisha, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali iko katika mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na uboreshaji wa Mitaala ya Elimu ili iweze kuwajengenea wanafunzi stadi na ujuzi mbalimbali ikiwemo ufundi utakaowawezesha kuhitimu na kuhimili ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Mara baada ya mitaala tajwa kukamilika ikiwa ni pamoja na manunuzi ya vifaa na mashine mbalimbali za ufundi, Elimu ya Ufundu itatolewa katika Shule za Msingi na Sekondari. Aidha, utaratibu wa kufanya mitihani ya Elimu ya Ufundu na kupata vyeti utaandaliwa kwa kushirikiana na mamlaka husika kama vile Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (*NACTVET*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapitio ya Sera na Mitaala, Serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa katika Chuo cha Ualimu Kleruu pamoja na Chuo cha Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi cha Morogoro (*MVTCC*) kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ikiwemo ujenzi wa mabweni ya wanafunzi kwa lengo la kuongeza fursa ya mafunzo kwa Walimu wa masomo ya Ufundu.

Mheshimiwa Spika, pia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kimeanza maandalizi ya utoaji wa mafunzo hayo katika ngazi ya Stashahada katika Elimu ya Ufundu, (*Diploma in Technical Education* na *Postgraduate Diploma in Technical Education*). Kwa sasa mitaala ya masomo hayo inafanyiwa kazi na Tume ya Vyuo Vikuu ili kuidhinishwa na kuanza kutumika katika Chuo hicho. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, swali hili niliwahi kuuliza likiwa linafanana hivi kwenye maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Majibu yaliyotolewa na Serikali na haya yanayotolewa sasa hivi yanapishana. Sasa napenda

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufahamu msimamo wa Serikali kuhusu shule hizi, kwa mfano shule ya Mshara, Sare na Mroma. Shule hizi zina majengo, vifaa na walimu: Je, Serikali inatoa msimamo gani kuhusiana na shule hizo?

Swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Ufundı *VETA* ndani ya Jimbo la Hai ilhali tayari tumeshapanga eneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna shule za msingi 123 hapa nchini ambazo zilikuwa zinatakiwa zitoe mafunzo ya ufundı pamoja na elimu ya msingi, lakini shule zote hizo sasa hivi hazitoi mafunzo hayo kwa sababu ya uhaba wa walimu. Vyuo ambavyo vilikuwa vinatoa mafunzo kwa mfano Chuo cha Ualimu cha Mtwara ambacho kazi yake kubwa ilikuwa ni kuwafundisha walimu elimu ya ufundı kwa ajili ya shule za msingi, imeacha kufanya kazi hiyo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kujibu swalı la msingi, sasa hivi tunapitia mitaala yote ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundı na lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaingiza ufundı na ujuzi katika shule zote ikiwa ni pamoja na hizi shule 123 na hizi shule za Jimbo la Hai kama alivyoeleza Mheshimiwa Saashisha. Tunatarajia kwamba tutamaliza shule za mitaala mwisho wa mwaka huu, hivyo tutaweza kuanza sasa kuhakikisha kwamba tunafundisha wanafunzi katika ngazi zote hizo.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili kuhusu *VETA*, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya hapa nchini na juhudı hizo zinaendelea. Kwa yale maeneo ambayo tayari Wilaya zimeshatenga maeneo na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hasa maeneo yale ambayo Wilaya na Halmashauri na Wabunge wameanza juhudzi za kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi, tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunaenda kuongeza nguvu za Serikali ili kukamilisha azma hii ya kuwa na VETA katika kila Wilaya ikiwa ni pamoja na Jimbo la Hai kwa Mheshimiwa Saashisha.

SPIKA: Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu ni: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunashirikiana na nchi nyingine ambazo zimeendelea katika sekta hii ya ufundi stadi hasa kwa masuala ya *Exchange Program* kuwapeleka watoto wetu *Internship* ili waweze kujifunza zaidi ufundi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Jesca kwa sababu pamoja na swali alilouliza hapa, tunafanya jitihada pamoja kuhakikisha kwamba tunaunganisha nguvu kupeleka vijana kwenda kusoma nchi za nje ikiwa ni pamoja na nchi ya Uturuki ambapo wameendelea vizuri sana katika masuala ya ufundi stadi na elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuhakikisha kwamba tunaanzisha taratibu kwanza za kuwa na *staff exchange* ya walimu wetu wa ufundi kwenda nchi nyingine kuangalia wanafundishwa vipi na kuleta walimu kutoka nje kuja kukaa kwa muda katika vyuo vyetu ili kuboresha elimu ya ufundi. Vile vile kupeleka wanafunzi wetu katika nchi ambazo zimeendelea vizuri zaidi katika elimu za ufundi ikiwa ni pamoja na Uturuki. Namwahidi Mheshimiwa Jesca kwamba jitihada ambazo ameshazianza tutazifanya pamoja mpaka tutazikamilisha. Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaelekea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

Na. 101

Kutatua Mgogoro Kati ya Jeshi la Wananchi na Kijiji cha Dunga – Zanzibar

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Wakazi wa Kijiji cha Dunga – Zanzibar?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu: -

Mheshimiwa spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Kambi ya Dunga 141KJ limejumuishwa katika Mpango wa Miaka Mitatu wa Wizara wa Kutatua Migogoro ya Ardhi wa 2020/2021 – 2022/2023 unaoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, upimaji na uthamini katika eneo hili ulianza tarehe 19 Aprili, 2022 na umemalizika tarehe 25 Aprili, 2022. Hatua zinazofuata ni kuwasilisha kitabu cha uthamini kwa Mthamini Mkuu wa Zanzibar kwa ajili ya idhini na kisha kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa uhakiki na malipo ya fidia. Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge avute subira, kwani mchakato umefikia hatua nzuri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Wizara imedhamiria kumaliza migogoro yote ya ardhi kati ya taasisi zake na wananchi.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanakhamis Said, swali la nyongeza.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kwa kazi hii anayoiendeleza kuwasaidia Watanzania. Nasubiri utekelezaji wa suala hili litakapofikia kwa sababu wananchi wanasubiri, kwani limekuwa ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasubiri utekelezaji wa Serikali. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanahamisi kwa kuelewa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Faustine Ndungulile swali la nyongeza.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mgogoro kama huo huko vilevile katika Jimbo la Kigamboni katika Kata ya Kimbiji eneo la Kijaka.

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro huo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ndugulile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kulifuatilia suala hili kwa karibu, kwa niaba ya wananchi wa Kigamboni na ninapenda kumfahamisha kwamba mgogoro huu tayari na wenyewe unashughulikiwa na upimaji ulishafanyika, kwa hiyo tunasubiri tupate hati na baada ya hapo hatua zinazofuata zitaendelea. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo Mbunge wa Arumeru Mashariki, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

Na. 102

Kukarabati Miundombinu ya Maji – Jimbo la Arumeru Mashariki

**MHE. BENAYA L. KAPINGA K.n.y. MHE. DKT. JOHN D.
PALLANGYO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati miundombinu ya maji katika Kata za Jimbo la Arumeru Mashariki.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Arumeru hali ya huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama ni asilimia 71.5 huduma hii inapatikana kutoka kwenye skimu 39 zilizojengwa kabla ya mwaka 2000. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji kwenye skimu za Kikwe-Msitu wa Mbogo, Kata ya Kikwe na Mbuguni Olkungabo - Ngabobo (Kata ya Ngarenanyuki na Ngabobo na Ngurdoto-Sakila - Ngyeku Kata za Imbaseni, Maji ya Chai na Kikatiti. Kazi hii itakamilika Mwezi Juni, 2022. Aidha, katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji, miradi mipyä itajengwa kwa ajili ya kutoa huduma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwenye Kata za Nkoarisambu na Akheri ambapo kazi hii itakamilika Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, ukarabati wa miundombinu ya maji utaendelea ili kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa maji katika Kata zote inakuwa endelevu.

SPIKA: Mheshimiwa Benaya Kapinga swali la nyongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Arumeru kwanza kabisa tutoe shukrani kwa majibu mazuri ya Serikali, vilevile kwa niaba ya Mheshimiwa Pallangyo anatoa shukrani nydingi sana kwamba aliomba Shilingi Bilioni 2.7 fedha hizo zimefika na tayari zimeanza kufanya kazi, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Kijiji cha Litoho, Kata ya Ukata, unaotokea Liwanga unatoa maji muda wote sijui nisema machafu lakini yasiyokuwa *pure* yana udongo kwa hiyo yanahitaji ujenzi wa chujio. Je, ni lini Serikali itajenga chujio katika mradi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali kwanza nipende kupokea shukrani kutoka kwa Mbunge wa Arumeru, kwa kweli kupeleka fedha ni wajibu wetu na kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu anaendelea kutoa fedha kwenye miradi hii mikubwa ili wananchi waweze kuondokana na matatizo ya maji na kubeba ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, kwenye ujenzi wa chujio naomba nitoe ahadi kwamba ni moja ya majukumu yetu kama Wizara nimelipokea tutalifanyia kazi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la chanzo cha maji cha Geita ni kubwa na ningependa kufahamu ni lini Wizara itakarabati ili kuongeza kiwango cha maji kinachozalishwa kwa ajili ya Mji wa Geita.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kanyasu Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara tumeweka mkakati wa kuona kwamba vyanzo vyote vya maji viweze kutoa maji safi salama na ya kutosha, hivyo hata kwenye Mji wa Geita lipo katika mikakati yetu nipende kumuomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kama ambavyo anafanyaa lengo ni kuona wananchi wanaenda kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amor swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kukamilisha mradi wa maji kutoka Nyamtukuza Wilayani Nyang'wale na sasa hivi maji tumeyapata lakini maji haya si safi na salama kwa sababu mradi ule haukutengenezewa chujio la kuyatibu yale maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chujio la kutibu maji ili wananchi wasije wakaugua na kupoteza fedha nyingi kwa ajili ya matibabu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amor Mbunge wa Nyangwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukrani zake kwa sababu mradi huu ni ile moja ya miradi vichefuchefu na hapa tunampongeza Mheshimiwa Waziri ameweza kusimamia mradi sasa unatoa maji, suala la chujio ni suala linalofuata katika mwaka ujao wa fedha tutahakikisha na suala la chujio nalo linapewa nafasi.

SPIKA: Mheshimiwa Shigongo swali la nyongeza.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Nilishawahidi kuripoti mradi wa Kalumea - Nyehunge Nyakalilo ni kichefuchefu, Mheshimiwa Waziri aliahidi kutembelea mradi ule ili aweze kutoa fundisho kwa watu wanaochezea fedha za Serikali naomba kuuliza tena.

Je, Mheshimiwa Waziri wako tayari kutembelea mradi wa Lumea ili kwenda kutoa fundisho kwa Wakandarasi wanaotumia vibaya fedha za Serikali?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shingongo Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sengerema mimi mwenye nilifika na tuliweza kufanya kazi nzuri na maeneo yale tuliyopita yanakwenda vizuri kwenye mradi huu anaouongelea Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili tutawasiliana kuona namna gani ya kuweza kufika pale kwa pamoja.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ni Mbunge wa Buchosa naona sasa Mbunge wa Sengerema amesimama. Mheshimiwa Tabasamu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, katika miradi ya maji ambayo iliyoko katika maeneo yetu tunao mradi mkubwa wa maji eneo la Nyasibu, Mbungo, Ngoma ambaon na wenyewe umekaa kwa muda mrefu nini majibu ya Serikali ili mradi huo uanze kama uliviyopangwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Tabasamu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Nyasibu tayari tumeshawaagiza vijana wetu waweeze kuona namna ya kuweza kuuendeleza Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane tuweke vizuri illi suala kwa sababu huu mradi ni muhimu wote tunafahamu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 103

Kuanzisha Wakala wa Udhibiti wa Mazao ya Mbogamboga na Matunda

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Wakala wa kudhibiti Mazao ya Mbogamboga na Matunda nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa, Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kuwa na Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza tasnia ya mazao ya bustani kutoptana na mchango mkubwa wa tasnia hiyo kwenye mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa mapendekezo ya kufanya marekebisho madogo *Miscellaneous Amendment* ya Sheria ya Usalama wa Chakula Na. 10 ya mwaka 1991 iliyoanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko - *Cereal and Other Produce Regulatory Authority*, ambapo pamoja na mambo mengine majukumu ya Mamlaka hiyo yatarekebishwa ili kuipa jukumu mahsusili usimamizi na uendelezaji wa tasnia ya bustani.

SPIKA: Mheshimiwa Deodatus Mwanyika swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya udharura na kwa ruksa yako naomba kwanza niwape pole wananchi wa Njombe kwa ajali kubwa iliyotokea na iliyouwa watu nane siku ya juzi.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa suala la gharama na hasa zao la Parachichi lina ushindani mkubwa sana kwenye soko, na suala la gharama ni suala la muhimu sana kuzingatiwa kwa maana ya kupunguza gharama hizo.

Je, Serikali itatuhakikishaje kwamba mamlaka hii inayoenda kuundwa haitaongeza gharama kwa wakulima wadogo kwa kupitia tozo na gharama za uendeshaji?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Je, ni lini sasa hayo mabadiliko yatafanyika kwa kuletwa Muswada hapa ndani. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwajika Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inakuza tasnia hii ya mazao ya mbogomboga na mazao ya bustani na hivyo moja kati ya maeneo makubwa ambayo tutayasimamia ni kuhakikisha kwamba mkulima hapati changamoto kubwa ya tozo nyingi ambazo zitamfanya akate tamaa ya kilimo chake.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali katika uanzishwaji wa mamlaka hii itahakikisha kwamba inalinda maslahi ya mkulima na mkulima anufaikie na kilimo chake.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu ni lini tutaleta mabadiliko haya ya sheria, mchakato umeshaanza ndani ya Wizara ya kuanza kupitia marekebisho haya ya sheria na pindi itakapokamilika kwa mujibu wa taratibu za Bunge utawasilishwa hapa Bungeni kwa ajili ya majadiliano na kupitishwa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swalii lake.

**Hitaji la Ujenzi Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi
hadi Songea**

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya ulinzi kutoka Mtwara – Newala – Masasi hadi Songea kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K.
MSONGWE)** anajibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya ulinzi ya kutoka Mtwara – Newala – Masasi hadi Songea yenye urefu wa KM 358, inaambaa na Mto Ruvuma. Serikali kuitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) kwa sasa inaendelea kuifungua barabara hii kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja makubwa na madogo katika mito na mikondo ya maji inayokatisha barabara hii ili iweze kuitika. Kiasi cha kilometra 208 zimefunguliwa na daraja kubwa la Mbangala lenye urefu wa mita 120 mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 11 Aprili, 2022. Baada ya kuifungua barabara yote Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chikota swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili.

Swali la kwanza, kutokana na changamoto za kiulinzi zilizopo kwa jirani zetu Msumbiji kuna matumizi makubwa sana ya barabara hii hasa sehemu ya Mahurunga, Kitaya, Mnongodi hadi Mchenjele.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta fedha za dharura na kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami Kilomita 70, wakati tunasubiri fedha nyingi za ujenzi wa Kilomita 358?

Swali langu la pili ni barabara sambamba ni hii ni barabara ya Mnivata Newala hadi Masasi tuneshaambiwa kwamba Serikali imeshapata fedha za ujenzi wa barabara hili.

Je, Serikali inawaambiaje wananchi wa maeneo haya, ujenzi huu utaanza lini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajua barabara hii ni muhimu hasa kutokana na changamoto za kiulinzi katika Mkao wa Mtwara na Mkao wa Ruvuma, Serikali mpango wake wa kwanza ni kuifungua yote ili iweze kuititika kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tukishaweza kwamba inaweza ikapitika na kujenga madaraja yote, Serikali sasa tunaona kutakuwa na haja ya kuijenga kwa kiwango cha lami kwani barabara hii siyo tu kwamba inaishia Masasi pia inakwenda Mkao wa Ruvuma ambako pia kuna Kilomita 535. Kwa hiyo ni barabara ambayo tunaomba tuifungue kwanza halafu tuanze kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu barabara ya kuanzia Mwinivata, Newala hadi Masasi yenyе urefu wa Kilomita 160. Benki ya Maendeleo ya Afrika ilishakubali kuifadhili hiyo barabara na tunapoongea sasa hivi tunachasubiri ni *no objection* ya hiyo benki, baada ya hapo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge manunuzi yanachukuwa siku 90 ndiyo barabara hiyo itaanza.

Mheshimiwa Spika, hivyo baada ya kupata *no objection* kutakuwa na mchakato wa manunuzi ambao ni wa kisheria siku zisizopungua 90 na baada ya hapo tutaanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kwa maana ya kuitangaza na kupata Mkandarasi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa hii fursa.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni lini Serikali itajenga barabara ya kimkakati kwa kiwango cha lami yenyе urefu wa Kilomita 176 inayotoka Kitahi, kupita Amani - Makolo, Paradiso, Rwanda, Lituhi, Mbaha, Lundo, mpaka Mbamba Bay kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ambayo inaanza Kitahi, kupitia Amani – Makolo, Rwanda hadi Lituhi ipo kwenye utangazaji kwa ajili ya kujenga barabara yote. Kuanzia Kitahi kwenda Mbamba Bay usanifu umeshakamilika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Serikali inatafuta fedha kujenga barabara hiyo ambayo pia ni sehemu ya barabara ya ulinzi hadi Mtwara. Ahsante.(*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Mtanda swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANROADS* ilikuwa na utaratibu wa kujenga kwa kiwango cha lami maeneo ya vilima korofi ili kurahisisha mawasiliano ya barabara hizo.

Je Serikali inampango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami eneo korofi la kilima cha Miyuu - Ndanda ili kurahisisha mawasiliano ya usafiri kwa wananchi wa Newala wanaoenda kutibiwa.(*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishawaagiza Mameneja wote wa *TANROADS*na kazi hiyo imeshafanyika kuainisha maeneo yote korofi ikiwemo na maeneo haya ya vilima ambavyo viko katika Wilaya ya Newala. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vilima hivyo vitajengwa kwa kiwango cha lami ili isiwe tatizo la wananchi kupata mawasiliano kipindi cha mvua. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kabula Shitobel, swali la nyongeza.

MHE. KABULA E. SHITOBELO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara inayounganisha Hungumalwa - Ngudu Wilaya ya Magu, imekuwa ikiwekwa kwenye llani ya Uchaguzi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2005, 2010, 2015 mpaka 2020 kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, sasa ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kabula, Mbunge wa Viti Maalum Mwanza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara alioitaja ya Hungumalwa kwenda Ngudu ipo kwenye mpango na ipo kwenye bajeti kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo Serikali imeahidi kuifanya. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Katani Katani swalii la nyongeza.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Spika, kutoka Mpwiti, Mkonjoano kuelekea Tandahimba ni barabara ambayo upembusi yakinifu imeshafanywa zaidi ya miaka minne.

Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Katani Katani Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaji ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa usanifu ulishakamilika Serikali inajipanga kutafuta fedha ili iweze kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, azma Serikali ni kujenga na tuna uhakika itajengwa fedha itakapopatikana. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Simon Songe swali la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyashimo Wilayani Busega kuelekea Dutwa Wilayani Bariadi imekuwa ikiahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami yenye takribani kilometra 47 kupitia Malili, Dutwa na pale Shigara.

Leo nataka *commitment* ya Serikali Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi wa Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, barabara hii ya kutoka Nyashimo kwenda Dutwa sasa hivi inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na itakapokuwa imekamilika barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Baran swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua, Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mizani katika Wilaya ya Babati - Kondoa hadi Dodoma.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo Mbunge wa Babati Vijiijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii amekuwa akiifuatilia sana Mheshimiwa Mbunge, nataka nimhakikishie kwamba kama tunavyomwelekeza na kumweleza kwamba Serikali ina mpango wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kulingana na patikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika Ujenzi wa barabara za *TANROAD* huwa kunakuwa na *packageya taa za barabarani* kwenye barabara ambazo zimeanza kujengwa kuanzia mwaka 2019. Barabara kutoka Njombe kuelekea Makete ni barabara ambayo ilikuwa ni *package ya nyuma*.

Je, ni lini Serikali itaingiza *package ya taa ya barabarani* kwenye Mji wa Handara na Makete Mjini, angalau na sisi Makete tuanze kuona taa za barabarani kama maeneo mengine. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo aliyoitaja ndiyo kwanza inakamilishwa kwa kiwango cha lami na Meneja wa Mkoa wa Njombe ameshatoa tathmini ya barabara, kwa maana ya gharama ambapo tutaweka taa za barabarani Mji wa Ramadhani, Ikonda na Makete yenyewe. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 105

Kukamilisha Ujenzi wa Soko la Kimkakati la Kimataifa la Remagwe

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kukamilisha ujenzi wa soko la kimkakati la Kimataifa la Remagwe.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA aliibuu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya Kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi, kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuanzisha masoko ya kimkakati ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa soko la Remagwe katika mpaka wa Sirari chini ya Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo Wilayani, *District Agricultural Sector Investment Project* (DASIP) uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha ujenzi wa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naomba ku-register masikitiko yangu kwa majibu waliyoyatoa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia Serikali inakuwa na miradi ambayo haina mpango mkakati madhubuti ya kuonesha ukomo wa mradi. Mathalani hili Soko la Remagwe limetelekezwa tangu Awamu ya Nne, takribani miaka 10.

Je, ni kwa nini Serikali kwa takribani miaka 10 haikuweza kuwa inatenga walau bajeti kila mwaka ili kuhakikisha kwamba inakamilisha huu mradi ambao inakiri kwamba ni wa kimkakati? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mkoa wa Mara unazalisha mazao ya kibiashara na ya chakula pamoja na mifugo ambapo hulisha ndani ya nchi lakin pia huenda kuuza nchi jirani ya Kenya, ambapo wakulima hawa wanauza kwa bei 'chee' baada ya kuwa wameishiwa na muda.

Ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa dharura wa kukamilisha soko hili la kimkakati la Kimaitaifa la Remagwe ili kutatua changamoto ya kimasoko kwa wakulima? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa maswali hayo pia niwashukuru Wabunge wa kutoka Tarime, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Michael Kembaki ambao wamekuwa wakifuatilia sana maendeleo ya ujenzi wa soko hilo. Kama nilivyosema Serikali inajua umuhimu wa masoko haya na ndio maana tulianza kujenga katika mipaka yote ambayo ni masoko ya kimkakati. Serikali inaendelea kutafuta fedha kama nilivyosema ilikuwa chini ya ufadhili wa benki, ufadhili huo ulisha, kwa hiyo tunatafuta fedha nyingine zaidi ili tukamilishe kujenga majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, zaidi tumeshawaambia wenzetu katika Halmashauri kuanza kutenga fedha kidogo kidogo katika bajeti zao kutokana na umuhimu wa masoko haya, kwa hiyo wanachokisema ndio Serikali inachokifanya na tunaendelea kufanya hivyo lakini kwasababu ni masoko ya kimkakati yana miundombinu muhimu, kwa hiyo ni lazima tupate fedha za kutosha ili tunapokuja kurudia sasa tukamilishe kwa pamoja kuhakikisha masoko haya yanakamilika katika viwango vinayotakiwa. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalii la mwisho Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour Mbunge wa Tumbe, sasa aulize swalii lake.

Na. 107

Mchango wa Utalii katika Pato la Taifa

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK aliuliza: -

Je, Tanzania inapokea watalii wa aina ngapi kutoka nje na sekta hii inachangia kiasi gani katika Pato la Taifa kwa mwaka?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikipokea watalii mbalimbali kutoka masoko ya Kimataifa ikiwemo nchi za Bara la Afrika, Amerika, Asia na Pasifikasi, Ulaya, na Mashariki ya Kat. Watalii hao wamekuwa wakitembelea Tanzania kwa madhumuni tofauti, ikiwa ni pamoja na mapumziko, kutembelea ndugu na jamaa, biashara, mikutano, matukio, na sababu nyinginezo ikiwemo ziara za kujifunza na matibabu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii kabla ya mlipuko wa janga la UVIKO - 19 ilikuwa ikichangia wastani wa asilimia 17.2 ya Pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha za kigeni, asilimia 60 ya biashara za huduma na kuzalisha ajira takribani Milioni 1.5, ikiwa ni ajira za moja kwa moja na zile zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, mlipuko wa janga la UVIKO-19 ulioikumba Dunia mwishoni mwa mwaka 2019 ulisababisha kupungua kwa idadi ya watalii kutoka 1,527,230 mwaka 2019 hadi watalii 620,867 mwaka 2020. Mapato kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.6 hadi Dola za Marekani Bilioni 0.7.

SPIKA: Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour swali la nyongeza.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba tena kwa mara ya pili leo nirekebishe jina langu ninaitwa Amour Khamis Mbarouk.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninashukuru majibu ya Mheshimiwa Waziri ila nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, wapo watalii wanaokuja Tanzania kwa ajili yakutafuta matibabu na tunao waganga wa jadi ambao wanaweza kutibu *COVID* kama vile Mheshimiwa Shekilindii. Swali langu ni kwamba Serikali ina mpango gani kwanza kuwawezesha waganga wa jadi kama hawa wenye ujuzi wa hali ya juu na kuwatangaza pia ili Pato la Taifa lionezeke? Nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii nadhani hilo atusaidie Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya nadhani anafanya mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri swali umelisikia lakini nafikiri linahusu watu wa afya zaidi namna watakavyowasaidia. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya sijui kama umesikia swali ama nikwambie anauliza kuhusu nini? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, nafikiri kama nimelisikia ni kwa namna gani tunaweza tukawasaidia waganga wa asili. Moja ni kwamba na kwa sababu kuna ushirikiano kweli na Wizara ya Maliasili kwa sababu baadhi ya vitu ambavyo vinatumika na watu wetu kama mizizi na vingine viro kwenye maeneo ya maliasili.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba tunaanza kuiweka rasi na kuna tafiti zinazofanyika kuthibitisha hivyo vitu ambavyo waganga wa asili lakini tunajenga ukaribu na Wizara ya Maliasili kwenda kwa pamoja ili tuweze kuwasaidia. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Afya mipango inatakiwa kuwekwa kwa ajili ya kuwasaidia wale waganga wetu wa jadi ili waweze kuwatibu watalii wanapokuja lakini

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii wafanye sasa kazi ya kuwatangaza ninyi mkishawawezesha. Kwa hiyo, upande wa maliasili na utalii wafanyekazi ya kuwatangaza hao waganga ili watalii wanapokuja wapate matibabu hapa nchini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nilete matangazo kwenu tutaanza na tangazo la wageni.

Tunae Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya, ambaye ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni Watatu wa Mheshimiwa Simon Songe, amba ni wapiga kura wake kutoka Busega - Simiyu wakiongozwa na Katibu Mwenezi wa Mkoa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, ambae ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga Ndugu Mabala Mlorwa. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Mipango Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa kwanza ni tangazo la *Iftar* siku ya leo. Kuna tangazo la *Iftar* mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge Jioni, tuna *Iftar* ambayo imeandaliwa na Wasafi *Media* katika viwanja vyta Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutakuwa na *Iftar* hapo niwaombe Wabunge wote lakini pia na Watumishi wa Bunge kuhudhuria futari hiyo ambayo imeandaliwa kwa heshima kabisa kwa ajili yenu na vijana wetu wa *Wasafi Media*. Kwa hiyo, niwaombe sana wote tujitokeze. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, pia ninalo tangazo lingine kwamba Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Mbarali Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed. Nadhani tangazo limeshaeleweka lakini Mbunge wa Mbarali Mheshimiwa Haroon Pirmohamed ametuletea sadaka yake kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kwa sababu sote tunafahamu huwa analeta sadaka ya mchele na mwaka huu ametuletea pia.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge zoezi la kugawa litafanyika baada ya Ibada ya mazishi tuliyonayo hapa siku ya leo. Kwa hiyo mchele huo utakuwa ukitolewa eneo la *basement* kila Mbunge ana haki yake hapo. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili nitasitisha Shughuli za Bunge ili kwenda kupokea mwili wa marehemu, halafu baadaye Waheshimiwa Wabunge wote tutatoka hapo nje tayari kwa ajili ya Ibada.

Waheshimiwa Wabunge, jamani naambiwa mgeni wa Mheshimiwa Godwin Mollel huyu maarufu, Mheshimiwa Mollel kumbe una mgeni wako hapa maarufu kabisa, tunaye Ndugu Ally Masoud Nyomwa, *a.k.a* Masoud Kipanya. Karibu sana, ahsante sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, bila shaka makofi hayo pamoja na zile katuni zake lakini nadhani anaashiria kutambua uwekezaji wake mkubwa katika upande wa magari, ambao amefanya ubunifu mzuri, tunakupongeza sana sana na tunakutakia kila heri katika yaliyo mbele yako. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo nitasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi Kamili Jioni leo.

(Saa 4.20 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu
wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka
wa Fedha 2022/2023**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa mtoe hoja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Selemani Jafo Daktari.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji na Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa pole kwako Spika wetu na kwa mama mzazi Mheshimiwa Anna Lupembe na Bunge lako Tukufu kwa ujumla, kwa kuondokewa kwa kipenzi chetu na Mbunge mwenzetu, Marehemu Irene Alex Ndyamkama. Hakika tumempoteza Mbunge mahiri, mcheshi na mwenye upendo mkubwa kwa watu wote. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchukua fursa hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwalettea maendeleo wananchi. Katika kipindi cha mwaka mmoja

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tumeshuhudia mambo makubwa katika nyanja za elimu, afya, maji, miundombinu na kuimarika kwa Muungano na uhifadhi wa mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza majukumu yake na kusimamia ipasavyo Ofisi ya Makamu wa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa anayofanya kwa lengo la kuwaaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaaliwa, Majaaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Mawaziri na Manaibu Waziri kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira. Napenda pia kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote walioeteuliwa katika nyadhifa zao kwa vipindi tofauti na Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nawapongeza kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuliletea Taifa maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika Spika wetu unaupiga mwingi na unatosha sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mussa Azzan Zungu, Mbunge wetu wa Jimbo la Ilala kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Uwezeshaji Viwanda na Biashara, Mheshimiwa David Kihenzile Mwakiposa na kwa Waheshimiwa Wabunge wote wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kuitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 na malengo ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mapitio na utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya kibajeti ambayo Fungu namba 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu namba 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 12.92 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu namba 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11.93 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi milioni 984.11 zilikuwa kwa ajili ya malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu namba 31, shilingi bilioni 22.14 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.29 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 6.85 zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, jumla ya shilingi bilioni 9.53 sawa na asilimia 73.8 ya bajeti iliyoidhinishwa zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopo katika Fungu namba 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 8.95 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 75.0 na shilingi milioni 581.8 ni kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 59.1. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya shilingi bilioni 9.38 sawa na asilimia 98.4 ya fedha zilizopokelewa zilitumiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa Fungu 31 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Ofisi ilipokea jumla ya shilingi bilioni 11.33 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 74.1 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, shilingi bilioni 2.03 ni mishahara ya Watumishi Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi bilioni 3.09 ni Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) na shilingi bilioni 6.2 ni Matumizi Mengineyo. Kati ya kiasi kilichopokelewa, shilingi bilioni 10.6 zilitumika sawa na asilimia 93.6.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya Maendeleo jumla ya shilingi bilioni 11.26 zilipokelewa sawa na asilimia 164.4 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni shilingi bilioni 3.09, sawa na asilimia 72.3 na fedha za nje zilikuwa jumla ya shilingi bilioni 8.17, sawa na asilimia 317.8. Aidha, katika kipindi hicho, shilingi bilioni 7.71 zilitumika ambapo shilingi bilioni 2.1 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 67.8 na shilingi bilioni 5.62 ni fedha za nje, sawa na asilimia 68.7.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa kazi zilizotekeliza katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa upande wa masuala ya Muungano. Muungano wetu umekuwa ni msingi mkuu wa amani na maendeleo uliojengeka kwa umoja, ushirikiano, mashauriano na kuheshimiana. Aidha, Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ni Tunu ya Taifa letu na ndiyo utambulisho wetu duniani, hivyo kuulinda, kuudumisha na kuuensi ni jukumu la kwetu sisi sote.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais imeratibu vikao sita vya kutafuta ufumbuzi wa hoja 18 za Muungano. Vikao hivyo vilifanyika katika ngazi za Mawaziri, Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ, Kamati ya Uchumi, Fedha na Biashara na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kilichofanyika Zanzibar tarehe 24 Agosti, 2021, chini ya Uongozi ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikubalika kuwa hoja 11 zimeshafanyiwa kazi na kukamilika na hivyo ziondolewe kwenye orodha ya hoja za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu masuala ya kijamii ikiwemo gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo zimeendelea kutolewa katika Majimbo yote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Ufutiliaji wa utekelezaji katika Taasisi za Muungano zinazotekeleza masuala ya Muungano na kuwawezesha wananchi katika pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo ukijumuisha TASAF, MKURABITA na miradi ya kuhimili tabia nchi kwa kutumia mfumo ikolojia.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya pande zote mbili za Muungano. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi Machi, 2022, vikao 18 vya ushirikiano vilifanyika katika sekta za Fedha, Ujenzi na Uchukuzi, Uchumi wa Buluu, Madini, Nishati, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Afya na Maendeleo ya Jamii, Maji, Maliasili, Elimu, Huduma ya Kisheria, Viwanda, Biashara, Uvubi na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano kupitia Redio, Runinga, Magazeti, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mitandao ya kijamii. Aidha, Andiko la Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar limezinduliwa jana wakati wa madhimisho ya miaka 58 ya Muungano na Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazingira; maendeleo ya nchi yetu yanategemea usimamizi endelevu wa mifumo ikolojia na maliasili zilizopo nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali zinazolenga kuboresha uhifadhi wa mazingira nchini. Hata hivyo, nchi yetu imeendelea kukabiliwa na changamoto za kimazingira ambazo ni uharibifu wa ardhi, ukosefu wa maji safi na salama, upotevu wa makazi ya wanyamapori na bionuai, uharibifu wa mifumo ikolojia ya maji, ukataji holela wa milti, uchafuzi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na matumizi yasiyo salama ya bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira huathiri afya ya binadamu, mifumo ikolojia na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa ujumla. Katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda na Miradi ya hifadhi ya mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeweza kutekeleza masuala ya mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanikiwa kutekeleza mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na kujumuisha maeneo mapya ya kimazingira ambapo Sera ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na mkakati wa utekelezaji wake ilizinduliwa tarehe 12 Februari, 2022 na Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uzinduzi huo ultianguliwa na zoezi la wiki moja ya uhamasishaji ya usafi wa mazingira na upandaji miti katika Jiji la Dodoma. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuelimisha wadau

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mbalimbali kuhusu maudhui ya Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021 ili kuwezesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza maandalizi ya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura namba 191 ili kuakisi matakwa ya Sera ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na masuala mengine ya Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, Ofisi imefanya marekebisho madogo katika Sheria ya Mazingira kwa kufuta Kifungu 194 na kuandika upya ili kupunguza mlolongo wa kufungua mashauri yanaohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali ilianda Mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026. Aidha, ili kuungana na jitihada za klimataifa zinazosimamiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuhimili mabadiliko ya Tabianchi, Serikali ilianda taarifa ya Mchango wa Taifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi unaolenga kuiwezesha nchi kuchangia upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 30 mpaka 35 kuitia sekta za misitu, nishati, uzalishaji na udhibiti wa taka katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hicho pia, Ofisi imeratibu vikao viwili vyta ngazi ya Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maji na kuitisha mapendekezo ya hatua za kuchukua katika kuboresha muundo wa usimamizi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imetoe ushauri kwa Wizara za Kisekta kuhusu uandaaji na utekelezaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK). Wizara zilizohusika ni Wizara ya Maji katika mabonde sita ya Maji, Wizara ya Madini, Wizara ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nishati, Wizara ya Maliasili na Utalii katika Pori la Akiba la Selous na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha katika maeneo ya Kongani ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Ofisi iliendelea kujenga uwezo kwa wataalam wa mazingira katika Sekretarieti za Mikoa 26 na Maafisa Mazingira katika Mamlaka za Serikali 184; Kupitia warsha na semina iliongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Mazingira; Maafisa 40 wamejengewa uwezo katika masuala ya udhibiti na usimamizi wa taka ngumu na taka hatarishi; Elimu kuhusu matumizi sahihi ya zebaki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu, matumizi ya nishati mbadala, mabadiliko ya tabianchi, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Tathmini ya Mazingira Kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la udhibiti wa mifuko ya plasitiki; katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Katazo la Serikali la tarehe Mosi Juni, 2019 la kupiga Marufuku uzalishaji, uingizaji, uuzaaji na usambazaji, usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya Mifuko ya Plastiki nchini. Katika ufuatiliaji huo, imebainika kuwa matumizi ya bidhaa za plastiki zilizopigwa marufuku hazitumiki tena bali bado ipo changamoto ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilipiga marufuku matumizi ya lakiri za plastiki katika vifuniko vya chupa za vinywaji hususan maji zinazozalishwa na kuingizwa nchini ifikapo tarehe 11 Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, marufuku hiyo inahusu uzalishaji, usambazaji, uingizaji nchini na utumiaji wa lakiri hizo. Vilevile, katika kutekeleza mabadiliko ya Sheria ya Mazingira, Sura namba 191 yaliyofanyika mwaka 2021, Ofisi ya Makamu wa Rais imetunga Kanuni za Ufifishaji wa makosa yanayohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira ili kutekeleza matakwa ya Kifungu 194 cha Sheria hiyo kwa lengo la kuruhusu makosa hayo kushughulikiwa bila kufungua mashauri mahakmani.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kuutaarifu Umma wa Watanzania hususan wazalishaji,

wasambazaji na waingizaji wa vinywaji vinavyotumia chupa zenye lakiri za plastiki kuacha mara moja kwa kuwa Serikali itachukua hatua stahiki dhidi ya uchafuzi wa mazingira utokanao na matumizi ya lakiri hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayotekelze nchini kwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, idadi ya miti iliyo pandwa ni milioni 202.9 na iliyostawi ni milioni 165.5 sawa na asilimia 81.6. Katika zoezi hilo halmashauri 27 kati ya 184 zilivuka lengo la kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka. Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza halmashauri hizo 27 zilizofikia lengo na kuzitaka halmashauri zote ambazo hazijafikia lengo kuchukua hatua za makusudi ili kunusuru Wilaya zao zitakazoathirika na uharibifu wa vyanzo vya maji. Nitoe rai kwa wananchi na wadau kuongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo yao na kushauri Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zinazohusu uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, suala la Kampeni ya Kukijanisha Dodoma; katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kukijanisha Dodoma. Katika kipindi hicho, Jumla ya miti laki 692.2 ilipandwa. Aidha, napenda pia kutoa wito kwa Jiji la Dodoma, TFS na wadau wengine kuongeza kasi katika utekelezaji wa mpango wa kukijanisha Dodoma ili kutimiza azma ya Serikali ya kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kijani.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia uwepo wa changamoto mbalimbali za kimazingira nchini kama ilivyoainishwa katika taarifa ya awali ya Mazingira ya Mwaka 2019; katika kipindi cha Mwaka 2021/2022, Ofisi inaandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira wenye lengo la kuibua changamoto za kimazingira kwa kuzingatia tofauti za kimaeneo utakaoambatana na Mpango Kazi wa utatuzi wa changamoto hizo. Mpango huo utatumika kama mwongozo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa uibuaji na utekelezaji wa miradi yote ya mazingira nchini. Mpango huo unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi imeendelea kutekeleza Kampeni Kabambe ya Kitaifa ya Uhifadhi na Usafi wa Mazingira iliyozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Juni, 2021, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Kampeni hiyo imelenga kuongeza ushiriki wa jamii na uwajibikaji wa mamlaka za usimamizi wa hifadhi na usafi wa mazingira ili kuchangia katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu. Katika kipindi hiki Ofisi imeandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa Kampeni kabambe wa mwaka 2021 hadi 2025. Aidha, kupitia kampeni hiyo, Ofisi kwa kushirikiana na Mabalozi wa Mazingira, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na wadau mbalimbali Imeendelea kuhamasisha usafi wa mazingira, upandaji wa miti, matumizi ya nishati mbadala na uhifadhi wa mazingira ya vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Nitumie fursa hii kuwashukuru Mabalozi wote wa mazingira nchini kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya katika kuhamasisha uhifadhi na usafi wa mazingira nchini. Ni matumaini yangu kuwa wataendelea kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa kufanya usafi na kutunza mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022; Ofisi imeendelea kuhamasisha upandaji miti kupitia Kampeni ya "Soma na Mti" iliyozinduliwa tarehe 20 Januari, 2022 katika Jiji la Dodoma. Kampeni hiyo imelenga kujenga tabia kwa wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu nchini kushiriki kikamilifu katika upandaji na utunzaji wa miti. Aidha, Kampeni hii inaendelea kuhamasishwa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Mabalozi wa Mazingira katika mikoa mbalimbali hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi imeendelea na maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani inayotarajiwa kufanyika tarehe 5 Juni,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2022. Madhumuni ya maadhimisho haya ni kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira na fursa zilizopo kwa ustawi wa jamii ya sasa na kizazi kijacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2022 maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Kimataifa yatarajiwa kufanyika nchini Sweden na Kauli Mbui ya maadhimisho hayo ni: *"Dunia ni moja, Hifadhi Mazingira kwa Maendeleo Endelevu."* Aidha, Kilele cha maadhimisho haya Kitaifa kinatarajiwa kufanyika Jiji la Dodoma hapa nchini. Aidha, katika maadhimisho hayo, pamoja na mambo mengine, Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira utazinduliwa rasmi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande wa ushiriki wa Tanzania katika Mikutano wa Kikanda na Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira; katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkatuba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Glasgow Scottish, kuanzia tarehe 22 Oktoba mpaka Tarehe 25, 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Tano wa Nchi Wanachama wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira uliofanyika Februari – Machi 4, 2022 Nairobi nchini Kenya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hicho jumla ya miradi nane ilitekelezwa. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Moja, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia, uliotekelizwa katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini 'A', Unguja na Zanzibar; Miradi ya Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini katika Wilaya za Magu (Mwanza), Nzega, Mkalama, Kondoa pamoja na Micheweni Zanzibar; Mradi wa Majaribio

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria; Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo ya Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto wa Asili na Uhifadhi ya Bionuai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika upande wa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (*NEMC*); katika mwaka wa fedha 2021/2022, Baraza limefanya ukaguzi katika miradi takriban 2,455 kwa madhumuni ya kutathmini uzingatiaji wa Sheria na Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Changamoto bubu kubwa za kimazingira zilizobainika kufuatia kaguzi hizo ni utiririshaji wa majitaka kwenye mazingira ikiwemo vyanzo vya maji na makazi ya watu; matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu ya asili kwa ajili ya nishati na ujenzi; ukosefu wa mifumo ya uhifadhi, kurejesha na uteketezaji taka ngumu na taka hatarishi; uzalishaji wa hewa chafu; uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala isiyokidhi viwango; upigaji wa kelele na mitememo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kutokana na changamoto hizo ni pamoja na kutoa ushauri, maelekezo, onyo pamoja na amri ya kizuizi kwenye shughuli zenyne madhara makubwa kwa mazingira, amri za urejeshaji wa mazingira na faini. Jumla ya miradi 2,105 ilipewa ushauri na maelekezo, miradi 350 ilipewa amri ya kizuizi kulinda mazingira. Hatua hizi zimesaidia kulinda afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, malengo na Maombi ya Fedha ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo; kwa mwaka 2022/2023 Ofisi itafanya yafuatayo: moja, kushughulikia masuala yote ya Muungano; pili, kuendelea kuratibu na kutatua changamoto zilizobaki za kimuungano; tatu, kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii ndani ya Muungano; nne, kuratibu masuala yasiyo ya Muungano; tano, kutoa elimu kwa Umma kuhusu Muungano; na sita, kuratibu utekelezaji wa masuala yaliyopatiwa ufumbuzi na Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la mazingira; matarajio ya Ofisi ni kuhakikisha kwamba tunashughulika na mambo yafuatayo: katika uhakikisha Hifadhi Endelevu ya Mazingira mwaka 2022/2023, Ofisi imepanga vipaumbele vifuatavyo: moja, kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; pili, kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa hifadhi ya Mazingira; tatu, kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; nne, kuratibu utekelezaji wa Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira; tano, kuendelea kujenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabia nchi; na sita, kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi itatekeleza miradi tisa yenye jumla ya shillingi 19.14. Miradi itakayotekelawa inajumuisha miradi ya Usimamizi Endelevu wa Ardhi Bonde la Ziwa Nyasa; Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo wa Ekolojia; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi; Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm; Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika; Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabia nchi; Mradi wa Kupunguza Hewa ya Ucaa; na Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Kingo za fukwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Baraza la Kitaifa la Uhifadhi wa Mazingira, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Baraza limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: moja, kuratibu mchakato wa tathmini ya athari za mazingira kwa ajili ya kufanya mapitio ya miradi na kusajili Wataalam Elekezi wa Mazingira; pili, kuendelea kutoa elimu kwa Umma na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya mazingira; kushirikiana na wadau kuandaa miongozo ya kisekta kwa lengo la kuhakikisha mapitio ya taarifa za *TAM* za sekta husika; kukamilisha tathmini ya eneo la Ruvu – Rufiji – Mafia – Kibiti – Kilwa (RUMAKI) ili kujumuishwa katika Mtandao wa Dunia wa Binadamu na Hifadhi Hai uliopo chini ya Shirika la Kimataifa la UNESCO. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake, dira na maelekezo aliyotupatia kuhusu majukumu yetu.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake makini.

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa usimamizi wake na maelekezo yake katika kufanikisha uandaaji wa bajeti. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Khamis H. Khamis au alimaarufu Chilo, Mbunge na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano wake alionipa katika kutekeleza majukumu ya kila siku. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru sana Wenyeviti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama pamoja na Mheshimiwa David Kihenzile; pamoja na Wajumbe wa Kamati yote kwa kazi kubwa waliyoifanya kuishauri Wizara yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kumshukuru Bi. Mary Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; Bw. Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano); na Bw. Edward Nyamanga, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Namshukuru Prof. Mhandisi Esnath Chaggua, Mwenyeekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*); Dkt. Mhandisi Samwel Gwamaka Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara na Vitengo na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Pia ninawashukuru wale wote waliouwesha kutekeleza majukumu ya ofisi kwa kipindi kilichopita, ambao

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi imefanikisha utekelezaji na kushirikiana; na shukrani zangu naomba kutoa kwa wadau wafuataao wa maendeleo; Serikali ya Norway; Serikali ya Sweden; Umoja wa Nchi za Ulaya; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa; Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa; Mfuko wa Mazingira wa Dunia; Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya *CRDB; Foreign and Commonwealth Development Organization*; Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda - UNIDO; Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani – *WWF*; Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo; Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi; Shirika la Kilimo na Chakula Duniani; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani; Asasi Zisizo za Kiserikali; Sekta Binafsi; Kamati ya Usimamizi wa Kampeni Kabambe; na Mabalozi wote wa Mazingira nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na ofisi katika kuimarisha Muungano wetu pamoja na mazingira yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha. Ili kufanikisha malengo tarajiwa kama nilivyobainisha kwenye hotuba yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Fungu 26, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 12,974,292,000 ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2022/2023. Kati ya kiasi hicho, shilingi 974,292,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na shilingi 12,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Fungu 31, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Shilingi 40,142,025,000/= kwa ajili ya Fungu hili. Kati ya kiasi hicho,

shilingi 18,180,328,000 ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na shilingi 21,961,697,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha shilingi 3,297,558,270; Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni shilingi 4,362,627,730; Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC); na shilingi 10,520,142,000 ni Matumizi Mengineyo. Aidha, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo yanajumuisha shilingi 3,602,000,000 fedha za ndani na shilingi 18,359,697,000 fedha za Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuomba fedha hizo sasa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI
KWA MWAKA 2021/22 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA 2022/23 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/23, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/22 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/23.

2. Mheshimiwa Spika, kwa dhati naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwalectea maendeleo wananchi. Katika kipindi cha mwaka mmoja tumeshuhudia mambo makubwa katika nyanja za elimu, afya, maji, miundombinu na kuimarika kwa Muungano na Uhifadhi wa Mazingira.

- 3.** Aidha, ninampongeza Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza majukumu yake na kuisimamia ipasavyo Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).
- 4.** *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie fursa hii kumpongeza pia Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazofanya kwa lengo la kuwaleta maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.
- 5.** *Mheshimiwa Spika*, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira.
- 6.** *Mheshimiwa Spika*, ninapenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nawapongeza kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuitelea nchi yetu maendeleo.
- 7.** *Mheshimiwa Spika*, kipekee napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninampongeza Mheshimiwa **Mussa Hassan Zungu (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa kamati hizo;

na ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

8. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa **Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.)**; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa **David Kihenziile Mwakiposa (Mb.)**; na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2022/23.

9. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2021/22 na malengo ya mwaka 2022/23.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2021/22

10. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Fungu 26

11. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, jumla ya **Shilingi 12,915,077,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,930,965,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 984,112,000.00** zilikuwa kwa ajili ya malipo ya Mishahara.

Fungu 31

12. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Fungu 31, **Shilingi 22,138,382,500.00** ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,287,594,500.00** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 6,850,788,000.00** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya

Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha **Shilingi 3,021,908,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 3,751,798,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na **Shilingi 8,513,888,500.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha **Shilingi 4,280,000,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 2,570,788,000.00** fedha za nje.

Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi, 2022

Fungu 26

13. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, jumla ya **Shilingi 9,529,714,319.33** sawa na asilimia 73.8 ya bajeti iliyoidhinishwa zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya **Fungu 26**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,947,914,319.33** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 75.0 na **Shilingi 581,800,000.00** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 59.1. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi 9,380,571,137.48** sawa na asilimia 98.4 ya fedha zilizopokelewa zilitumika.

Fungu 31

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Ofisi ilipokea jumla ya **Shilingi 11,326,006,101.83** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 74.1 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **Shilingi 2,034,315,643.56** ni mishahara ya Watumishi Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 3,092,783,799.00** ni Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na **Shilingi 6,198,906,659.27** ni Matumizi Mengineyo. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **Shilingi 10,600,098,525.05** zilitumika sawa na asilimia 93.6.

15. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa bajeti ya Maendeleo jumla ya **Shilingi 11,261,679,547.53** zilipokelewa sawa na asilimia 164.4 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni **Shilingi 3,092,406,494.26** sawa na asilimia 72.3 na

fedha za nje ni **Shilingi 8,169,273,053.27** sawa na asilimia 317.8. Aidha, katika kipindi hicho, **Shilingi 7,712,508,184.50** zilitumika ambapo **Shilingi 2,096,925,907.74** ni fedha za ndani sawa na asilimia 67.8 na **Shilingi 5,615,582,276.76** ni fedha za nje sawa na asilimia 68.7.

16. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22– 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020– 2025); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura,191; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu; na Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Vlongozi Wakuu.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2021/22 MASUALA YA MUUNGANO

17. Mheshimiwa Spika, Muungano wetu umekuwa ni msingi mkuu wa amani na maendeleo uliojengeka kwa umoja, ushirikiano, mashauriano na kuheshimiana. Aidha, Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ni Tunu ya Taifa letu na ndio utambulisho wetu duniani, hivyo kuulinda, kuudumisha na kuuensi ni jukumu letu sote. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

18. Mheshimiwa Spika, Kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kilichofanyika Dodoma tarehe 09 Februari, 2019 kilitoa maagizo kuhusu hoja 18 za Muungano zilizohitaji kutafutiwa ufumbuzi. Hadi kufikia tarehe 24 Agosti, 2021 Wizara zenye hoja ziliendelea kufanya kazi maagizo ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

19. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/22 Ofisi ya Makamu wa Rais imeratibu vikao sita (6) vya kutafuta ufumbuzi wa hoja 18 za Muungano. Vikao hivyo vilifanyika katika ngazi ya Mawaziri; Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ; Kamati ya Uchumi, Fedha na Biashara; na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.



Wajumbe wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ngazi ya Makatibu Wakuu wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kukamilika kwa kikao kazi. Katikati ni Mwenyekiti wa Kikao hicho Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango (SMI), Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba. Kikao kilifanyika Dodoma tarehe 2 Agosti, 2021.

20. Mheshimiwa Spika, Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kilifanyika Zanzibar tarehe 24 Agosti, 2021 chini ya Uongozi na Uenyekiti wa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao hicho ilikubalika kuwa, hoja kumi na moja (11) zimekwishafanyiwa kazi na kukamilika na hivyo ziondolewe kwenye orodha ya hoja za Muungano.

21. Mheshimiwa Spika, hoja zilizopatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya Hoja za Muungano ni:

- (i) Uvvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu;
- (ii) Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar;

- (iii) Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano;
- (iv) Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kibajeti;
- (v) Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja;
- (vi) Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba;
- (vii) Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri;
- (viii) Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar;
- (ix) Mapato yanayokusanywa na Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar;
- (x) Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Rufaa za Kodi kutoka Zanzibar; na
- (xi) Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana kutoka Zanzibar.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango akishuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi. Hafla iliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Utalii, Maruhubi, Zanzibar Agosti 24, 2021.

22. Mheshimiwa Spika, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, changamoto za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuendelea kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu. Hivyo, wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali za pande mbili za Muungano kwamba changamoto zilizobakia na ambazo kimsingi zipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi zitakamilishwa. Aidha, makubaliano yaliyofikiwa na pande mbili kwa hoja zilizopatiwa ufumbuzi, yatakekelezwa kama ilivyokubalika.

23. Mheshimiwa Spika, hoja za Muungano zinazoendelea kutafutiwa ufumbuzi ni:- Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu; Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; Kodi ya Mapato yatokanayo na mishahara (Pay As You Earn - PAYE) na Kodi ya Mapato inayozuiliwa (Withholding Tax); Usajili wa Vyombo vya Moto; Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha; Ongezeko la gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO; na Changamoto ya Uingizaji wa sukari katika soko la Tanzania Bara.

(ii) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii

Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

24. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeratibu gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo hadi Machi, 2022 **Shilingi 27,038,498,469.01** zimepelekwa SMZ. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,400,000,000.00** ni fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Zanzibar; **Shilingi 13,318,640,304.00** ni fedha za mapato ya PAYE; **Shilingi 2,348,388,513.01** ni fedha za misaada kutoka nje (GBS); **Shilingi 9,000,000,000.00** ni gawio la faida ya Benki Kuu; na **Shilingi 971,469,652.00** ni gawio la Miamala ya Simu.

Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Zanzibar

25. *Mheshimiwa Spika*, fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo zimeendelea kutolewa katika Majimbo yote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kila mwaka kwa ajili ya kuchochea maendeleo. Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi inayotekelizwa kwa kutumia fedha hizo mwezi Machi, 2022 kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji na kushauri namna ya kukabiliana nazo. Katika ufuatiliaji huo imebainika kuwa fedha hizo zimesaidia kuibua na kutekelezwa kwa miradi ya kijamii ikiwemo maji, afya, elimu na umeme ambayo imewanufaisha wananchi wa majimbo husika.

Utekelezaji katika Taasisi zinazohusu Muungano

26. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji katika Taasisi za Muungano zinazotekleza masuala ya Muungano. Tathmini ilifanyika ili kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji ambapo Taasisi 20 zilifanyiwa tathmini hiyo ambayo imebainisha kuwa, Taasisi za Muungano zinafanya kazi kwa ufanisi pande zote mbili za Muungano na changamoto zilizopo zimebainishwa na kushauri namna ya kukabiliana nazo.

Miradi ya Maendeleo inayotekelizwa pande zote mbili za Muungano

27. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Miradi na Programu hizo zimefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii. Miradi hiyo inagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirkiana na Washirika wa Maendeleo.

28. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22 miradi na programu zinazotekelezwa pande zote mbili za Muungano ni: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Mzunguko wa Pili, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mradi wa Udhibiti wa Uvubi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi; Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga; Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania; Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania; Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia; Mradi wa uboreshaji wa Elimu kuititia “Global Partnership for Education”; na Mradi wa Sumu Kuvu.

(iii) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya SJMT na SMZ

29. Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya pande zote mbili za Muungano. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Vikao kumi na nane (18) vya ushirikiano vilifanyika katika sekta za Fedha, Ujenzi na Uchukuzi, Uchumi wa Buluu, Madini, Nishati, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Afya na Maendeleo ya Jamii, Maji, Maliasili, Elimu, Huduma za Sheria, Viwanda, Biashara, Uvubi na Mifugo.

(iv) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano

30. Mheshimiwa Spika, Ofisiimeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano kuititia Redio, Runinga, Magazeti, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na Mitandao ya Kijamii. Aidha, Ofisiimeandaa **Andiko la Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar** kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu chimbuko, misingi na maendeleo ya Muungano. Andiko hilo litazinduliwa kesho wakati wa madhimisho ya miaka 58 ya Muungano.

HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA

31. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yetu yanategemea usimamizi endelevu wa mifumo-ikolojia na maliasili zilizopo nchini. Katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi

ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali zinazolenga kuboresha uhifadhi wa Mazingira nchini. Hata hivyo, Nchi yetu inaendelea kukabiliwa na changamoto za kimazingira ambazo ni: uharibifu wa ardhi; ukosefu wa maji safi na salama; upotevu wa makazi ya wanyamapori na bionuai; uharibifu wa mifumo ikolojia ya maji; ukataji holela wa miti; uchafuzi wa mazingira; mabadiliko ya tabianchi; na matumizi yasiyo salama ya bioteknolojia ya kisasa.

32. *Mheshimiwa Spika*, Uharibifu wa mazingira huathiri afya ya binadamu, mifumo ikolojia na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa ujumla. Katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda na Miradi ya hifadhi ya mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais imeweza kutekeleza azma hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura, 191, Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Miongozo na Mikakati.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021. Kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo na kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, Mhe. David Kihanzile. Uzinduzi ulifanyika Februari 12, 2022.

Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997

33. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanikiwa kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na kujumuisha maeneo mapya ya kimazingira ambayo ni; kuongezeka kwa viumbe vamizi; taka za kielektroniki; matumizi ya kemikali na bioteknolojia ya kisasa yasiyo salama; kukua kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia; na uwekezaji katika miradi ya mazingira na masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Sera mpya ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na mkakati wa utekelezaji wake ilizinduliwa tarehe 12 Februari, 2022 na Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uzinduzi huo ultanguliwa na zoezi la wiki moja ya kuhamasisha usafi wa mazingira na upandaji miti katika Jiji la Dodoma. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu maudhui ya Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021 ili kuwezesha utekelezaji wake.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akipanda mti katika eneo la wazi Medeli jijini Dodoma Februari 7, 2022 ikiwa ni mojawapo ya shughuli za mazingira kuelekea Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 uliofanywa Februari 12, 2022 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191

34. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza maandalizi ya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ili kuakisi matakwa ya Sera ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na masuala mengine ya Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, Ofisi imefanya marekebisho madogo katika Sheria ya Mazingira kwa kufuta Kifungu cha 194 na kukiandika upya ili kupunguza mlolongo wa kufungua mashauri yanaohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na kanuni zake.

Kanuni na Miongozo ya Uhifadhi wa Mazingira

35. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kuandaa na kufanya mapitio ya Kanuni na Miongozo mbalimbali. Kanuni zilizoandaliwa ni pamoja na: Kanuni ya Uhifadhi wa Maeneo Lindwa na Nyeti ya mwaka 2022 ili kuyalinda maeneo husika; Mapitio ya Kanuni ya Marufuku ya Mifuko ya Plastiki ya mwaka 2019 ili kudhibiti matumizi ya lakiri kwenye mifuniko ya chupa; na Mapitio ya Kanuni za Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni ili kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya kemikali hizo.

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hicho, Ofisi ilianda Mwongozo wa Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira Utokanao na Kelele na Mitetemo wa mwaka 2021 ikiwa ni hatua za kukabiliana na ongezeko la kelele hususan katika maeneo ya mijini. Aidha, Ofisi imeandaa Mwongozo wa Udhibiti wa Taka Ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza wa mwaka 2021. Lengo la Mwongozo huu ni kupunguza uchafuzi wa mazingira na kutoa fursa kwa jamii kuongeza kipato kutokana na shughuli za urejelezaji wa taka. Kukamilika kwa miongozo hiyo ni hatua muhimu katika kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari zitokanazo na uchafuzi wa mazingira.

Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

37. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Serikali iliandaa Mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2021/22 – 2025/26. Aidha, ili kuungana na jithhada za kimataifa zinazosimamiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuhimili mabadiliko ya Tabianchi, Serikali iliandaa taarifa ya Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi unaolenga kuiwezesha nchi kuchangia upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 30 hadi 35 kuititia sekta za misitu, nishati, usafirishaji na udhibiti wa taka katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi 2030.

Kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa

38. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu vikao viwili (2) vya ngazi ya Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maji na kuitisha mapendekezo ya hatua za kuchukua katika kuboresha muundo wa usimamizi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mazingira.

39. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imetua ushauri kwa Wizara za Kisekta kuhusu uandaaji na utekelezaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK). Wizara zilizohusika ni: Wizara ya Maji katika mabonde sita (6) ya Maji; Wizara ya Madini; Wizara ya Nishati; Wizara ya Maliasili na Utalii katika Pori la akiba la Selous; na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha katika maeneo ya Kongani za Viwanda.

40. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hicho, Ofisi iliendelea kujenga uwezo kwa wataalam wa mazingira katika

Sekretarieti za Mikoa 26 na Maafisa Mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 kuititia warsha na semina ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Maafisa mazingira 40 wamejengewa uwezo katika masuala ya udhibiti na usimamizi wa taka ngumu na taka hatarishi; elimu kuhusu matumizi sahihi ya Zebaki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu; matumizi ya nishati mbadala; mabadiliko ya tabianchi; Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM); na Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK).



Wadau mbalimbali wa mazingira kutoka Mkoa wa Dodoma wakimsikiliza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Mhe. Selemani Jafo baada ya kukutana nao Januari 26, 2022, Dodoma.

(ii) Hifadhi ya Mazingira na mifumo Ikolojia katika Vyano vya Maji

41. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyano vya Maji 2021 - 2025. Aidha, katika kipindi hicho, Ofisi ilifanya ufuutiliaji katika Halmashauri 25 ili kubaini changamoto za uhifadhi wa mifumo ikolojia. Vilevile, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Kamati ya Kitaifa ya kuokoa Mifumo Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu pamoja na eneo la Ihefu. Jukumu la Kamati hii ni

kufuatilia utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuokoa maeneo yaliyoharibika katika Bonde hilo ambalo ni chanzo muhimu cha maji cha Mto Ruaha na ikolojia yake.

42. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 katika Halmashauri 19 zilizopo katika mikoa minne (4) ya nyanda za juu kusini ikiwemo Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa. Changamoto zilizobainika ni pamoja na: uharibifu wa vyanzo vya maji; shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini zisizozingatia kanuni za uhifadhi; uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na kilimo kisicho endelevu; ukataji miti ovyo kwa ajili ya kilimo na mkaa; na ufugaji holela. Aidha, kuitia zoezi hilo Ofisi iliweza kuhimiza Mamlaka katika ngazi za Mikoa na Halmashauri husika kuhamasisha wananchi kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika shughuli za kiuchumi. Vilevile, Mamlaka hizo zillielekezwa kutunga na kusimamila Sheria ndogo za uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao.

(ii) Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira

Udhibiti wa Mifuko ya Plastiki

43. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Katazo la Serikali la tarehe 1 Juni, 2019 la Kupiga Marufuku Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji, Usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya Mifuko ya Plastiki nchini. Kuitia ufuatilaji huo, imebainika kuwa matumizi ya bidhaa za plastiki zilizopigwa marufuku hazitumiki tena bali bado ipo changamoto ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilipiga marufuku matumizi ya lakiri za plastiki katika vifuniko vya chupa za vinywaji hususan maji zinazosalishwa na kuingizwa nchini ifikapo tarehe 11 Aprili, 2022. Marufuku hiyo inahusu Uzalishaji; Usambazaji; Uingizaji nchini na Utumiaji wa lakiri hizo. Vilevile, katika kutekeleza mabadiliko ya Sheria ya Mazingira, Sura 191 yaliyofanyika mwaka 2021 Ofisi ya Makamu wa Rais imetunga Kanuni za Ufilishaji makosa yanayohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira ili kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 194 cha

Sheria hiyo kwa lengo la kuruhusu makosa hayo kushughulikiwa bila kufungua mashauri mahakamani.

44. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kuutaarifu umma wa Watanzania hususan wazalishaji, wasambazaji na waingizaji wa vinywaji vinavyotumia chupa zenyenye lakiri za plastiki kuacha mara moja kwakuwa Serikali itachukua hatua stahiki dhidi ya uchafuzi wa mazingira utokanao na matumizi ya lakiri hizo.

Usimamizi wa Taka Hatarishi na matumizi ya taka kama rasilimali viwandani

45. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kusimamia uzalishaji, ukusanyaji, usafirishaji na utupaji wa taka hatarishi hususan chuma chakavu, mafuta machafu, betri chakavu na taka za kielektroniki kwa mujibu wa Kanuni za Udhhibit na Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021 na Kanuni za Taka za Kielektroniki za mwaka 2021. Katika kipindi hicho, Ofisi imetoea vibali 270 vya taka hatarishi, na vibali 32 vya taka za kielektroniki kwa makampuni 83 na watu binafsi 46. Kupitia vibali hivyo jumla ya tani 518,207.9 na litu 977,458 za taka hatarishi zimeondolewa kwenye mazingira. Aidha, katika kurahisisha utekelezaji na kuongeza wigo wa wadau wanaojishughulisha na shughuli za urejelezaji wa taka hatarishi, Ofisi imetafsiri Kanuni za Usimamizi na Udhhibit wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021 na Kanuni za Usimamizi na Udhhibit wa Taka za Kielekitroniki za Mwaka 2021 kwa lugha ya Kiswahili.

Kuratibu utekelezaji wa Mpango - Kazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini

46. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango - Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu nchini. Aidha, Ofisi imetoea elimu kuhusu hifadhi ya mazingira na madhara yatokanayo na matumizi ya zebaki katika shughuli za

wachimbaji wadogo wapatao 2,200 katika maeneo 22 ya wachimbaji kutoka mikoa 10 ya kimadini ikiwa ni pamoja na Mara, Shinyanga, Geita, Kahama, Mbeya, Katavi, Tanga, Tabora, Singida na Dodoma. Vilevile, Ofisi imetoa elimu kwa wanahabari 50 kutoka vyombo vya habari 10 vikiwemo runinga, magazeti, redio na mitandao ya kijamii; viongozi 29 wa vyama vya wachimbaji wadogo; na Maafisa waandamizi 46 kutoka Wizara za kisekta na Taasisi za Serikali zinazohusika na usimamizi na udhibiti wa kemikali. Pia, Ofisi imeshirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara na watumiaji wa kemikali za viwandani na migodini.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Bw. Edward Nyamanga akifungua Warsha ya Uhamasishaji wa Utekelezaji wa Mpango – kazi kitaifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwenye Uchimbaji mdogo wa Dhahabu (2020-25) iliyofanyika Dodoma Machi 15, 2022.

Kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika Migodi, Viwanda na Madampo



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (wa tatu kushoto) akisikiliza maelezo kuhusu mradi wa dampo la kisasa la Chidaya jijini Dodoma kutoka kwa Meneja wa dampo hilo, Bw. John Kiwanga, alipofanya ziara Septemba 3, 2021.

47. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Kisekta imefanya kagazi 15 katika migodi iliyopo mikoa ya Shinyanga, Mara, Geita, Ruvuma, Mbeya na Dodoma. Aidha, ukagazi ulifanyika katika viwanda nane (8) kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kwa lengo la kuhimiza uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Sura, 191. Vilevile, ukagazi wa usimamizi na uteketezaji wa taka ngumu umefanyika katika madampo ya Chidaya - Dodoma, Pugu Kinyamwezi – Dar Es Salaam, Muriet Arusha na Mpiganini - Tanga. Changamoto zilizobainika ni pamoja na kutiririsha majitaka katika mazingira; uchafuzi wa hewa; matumizi yasiyo salama ya kemikali katika kuchenjua dhahabu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu; ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya kuimarisha mashimo ya wachimbaji wadogo; na usimamizi hafifu wa taka ngumu ikiwemo uchomaji holela wa taka.

(iii) Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi

48. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi imeendelea kuratibu shughuli mbalimbali zenyе lengo la upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na; kutoa mafunzo kuhusu utafutaji fedha kwa ajili ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya Tabianchi, uandaaji wa mipango katika ngazi ya jamii inayozingatia kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi; kuratibu Taasisi za Serikali na zisisizo za Serikali zikiwemo UNDP, Foreign Commonwealth Development Organisation - FCDO, Climate Action Network in Tanzania - CANTZ, Forum CC, Care International -Tanzania, Gender and Climate Change Tanzania Coalition (GCCTC), Research and Poverty Alleviation - REPOA zenyе nia ya kutafuta fedha kupitia mifuko mbalimbali ya mabadiliko ya Tabianchi duniani. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Kituo cha Kitaifa Cha Uratibu wa Hewa Ukaa na UNDP ilishiriki kutoa mafunzo kwa wataalam 55 kutoka taasisi za Serikali na Sekta binafsi

Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusu ukusanyaji wa Taarifa za Gesijoto, Mfumo wa Upimaji, Ufuatiliaji na Uhakiki.


49. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu wadau wanaolenga kuanzisha miradi inayohusu biashara ya hewa ukaa kwa mfumo wa mkopo wa hewa ukaa (Carbon Credit). Aidha, katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu Kampuni moja (1) iliyowekeza na Mashirika matatu (3) yenye nia ya kuwekeza katika biashara ya hewa ukaa. Vilevile, Ofisi imeanza kuandaa Kanuni na Mwongozo wa kusimamia biashara ya hewa ukaa nchini katika maeneo ya hifadhi ya hewa ukaa ikiwemo rasilimali za misitu, maji na ardhi.

Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha bahari

50. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni pamoja na Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Katika kipindi hicho, Ofisi imefanya kazi mbalimbali ikiwemo kufanya tathmini ya uharibifu wa fukwe unaosababishwa na kuongezeka kwa kina cha maji katika ukanda wa Bahari katika maeneo ya Mikadi Beach na Ndege Beach - Dar Es Salaam; Mikindani - Mtwara; na fukwe za Msuka na Sipwese zilizopo Micheweni Pemba. Aidha, tathmini zimefanyika katika ukanda wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria.

51. *Mheshimiwa Spika*, ili kukabiliana na uharibifu wa fukwe katika bahari unaotokana na mmomonyoko, Ofisi imekamilisha maandalizi ya miradi yenye lengo la kukabiliana na mmomonyoko wa fukwe hizo katika maeneo ya Mikindani Mtwara na Sipwese Pemba. Miradi hii inalenga kujenga kuta za bahari katika maeneo ya Mikindani Mtwara (mita 1,750) na Sipwese Pemba (mita 500). Miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha za ndani na inakadiriba kugharimu **Shilingi Bilioni 4.4** itakapokamilika. Serikali inaendelea kutafuta rasilimali fedha

kwa ajili ya kutekeleza miradi mingine ya aina hiyo katika maeneo ya fukwe mbalimbali nchini.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Dezo Construction Co. Ltd Bw. Premji Pindoria wakisaini mkataba wa ujenzi na ukarabati wa kingo za fukwe katika maeneo ya mwambao wa Mikindani (Mtwara) hafla iliyofanyika Machi 31, 2022 wanaoshuhudia ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Dusan Shimbo na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi.

Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi

52. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi uliopo chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Katika kipindi hiki Tanzania imefanikiwa kupata mradi wa **Dola za Marekani milioni 100** kupitia benki ya CRDB kwa ajili ya kujenga uwezo wa kiteknolojia wa kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi katika sekta ya kilimo. Mradi huu utawezesha Benki ya CRDB kukopesha wakulima kwa riba nafuu ili kutekeleza miradi ya kilimo cha kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, natoa rai kwa wakulima na wadau wengine kuchangamka fursa hii.

(iv) Kukabiliana na changamoto za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira

Kampeni ya Upandaji Miti milioni 1.5 kwa Kila Halmashauri kwa Mwaka

53. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayotekelzeza nchini kwa kila Halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, idadi ya miti iliyopandwa ni 202,923,907 na iliyostawi ni 165,501,119 sawa na asilimia 81.6. Halmashauri 27 kati ya 184 zilivuka lengo la kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka. Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri zilizofikia lengo na kuzitaka Halmashauri zote ambazo hazikufikia lengo kuchukua hatua za makusudi ili kunusuru Wilaya zao na athari zitokanazo na uharibifu wa ardi na vyanzo vya maji. Nitoe rai kwa wananchi na wadau kuongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo yao na kushauri Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zinazohusu uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao.

Kampeni ya Kukijanisha Dodoma

54. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kukijanisha Dodoma. Katika kipindi hicho, Jumla ya miti 692,247 ilipandwa katika wilaya zote za Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo: Dodoma Mjini miti 584,790; Wilaya ya Mpwapwa miti 21,450; Wilaya ya Bahi miti 20,720; Wilaya ya Chemba miti 4,000; Wilaya ya Kongwa miti 45,587; Wilaya ya Kondoa miti 11,200; na Wilaya ya Chamwino miti 4,500. Aidha, napenda pia kutoa wito kwa Jiji la Dodoma, TFS na wadau wengine kuongeza kasi katika utekelezaji wa mpango wa kukijanisha Dodoma ili kutimiza azma ya Serikali ya kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kijani.

Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira

55. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia uwepo wa changamoto mbalimbali za mazingira nchini kama ilivyoinishwa katika taarifa ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2019, katika kipindi

cha Mwaka 2021/22 Ofisi inaandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira (Master Plan of Environmental Interventions) wenyе lengo la kuibua changamoto za kimazingira kwa kuzingatia tofauti za kimaeneo utakaoambatana na Mpango Kazi wa utatuizi wa changamoto hizo. Mpango huo utatumika kama mwongozo wa uibuaji na utekelezaji wa miradi yote ya mazingira nchini. Mpango huu unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Juni, 2022.

Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira

56. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi imeendelea kutekeleza Kampeni Kabambe ya Kitaifa ya Uhifadhi na Usafi wa Mazingira iliyozinduliwa na **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Juni, 2021 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Kampeni hiyo imelenga kuongeza ushiriki wa jamii na uwajibikaji wa mamlaka za usimamizi wa hifadhi na usafi wa mazingira ili kuchangia katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu. Katika kipindi hiki Ofisi imeandaa Mpango - Kazi wa utekelezaji wa Kampeni kabambe wa mwaka 2021 – 2025. Aidha, kupitia kampeni hiyo, Ofisi kwa kushirikiana na Mabalozi wa Mazingira, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha usafi wa mazingira, upandaji miti, matumizi ya nishati mbadala, na hifadhi ya mazingira ya vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Nitumie fursa hii kuwashukuru Mabalozi wa mazingira kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhamasisha uhifadhi na usafi wa mazingira nchini. Ni matumaini yangu kuwa wataendelea kuhamasisha umma kuhusu umuhimu 38 wa kufanya usafi na kutunza mazingira katika maeneo yetu.

Kampeni ya Soma na Mti

57. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi imeendelea kuhamasisha upandaji miti kupitia Kampeni ya "Soma na Mti" niliyoizindua tarehe 20 Januari, 2022 katika Jiji la Dodoma. Kampeni hiyo imelenga kujenga tabia kwa wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo nchini kushiriki kikamilifu katika upandaji na utunzaji wa miti. Aidha,

Kampeni imeendelea kuhamasishwa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya; na Mabalozi wa Mazingira katika mikoa mbalimbali nchini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akipanda mti na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma wakati alipozindua Kampeni ya upandaji wa miti kwa wanafunzi wa shule na vyuo jijini Dodoma Januari 20, 2022. Kampeni hiyo inafahamika kama 'Soma na Mti'.

(vi) Elimu kwa Umma Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira

58. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; warsha na semina, kampeni; hotuba za viongozi; na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu mazingira. Elimu iliyotolewa ilihusu: Sera, Sheria na Kanuni za usimamizi wa mazingira; mabadiliko ya tabianchi; matumizi ya nishati mbadala; uhifadhi wa tabaka la Ozoni; usimamizi wa matumizi ya zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo; viumbwe vamizi; hifadhi ya bionuai; mikataba ya kikanda na kimataifa ya mazingira; Upandaji miti; udhibiti wa taka na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; hifadhi ya vyanzo vya maji; hifadhi ya mazingira ya ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi; katazo la mifuko ya plastiki; na matumizi ya nishati mbadala.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt Selemani Jafo akijumuika na viongozi na wadau wa mazingira kushiriki zoezi la usafi wa mazingira katika ufukwe wa Feri Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam Machi 26, 2022.

59. *Mheshimiwa Spika*, elimu hiyo imeongeza hamasa kwa wadau kushiriki katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira hususan upandaji miti, usafi wa mazingira na utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

60. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea na Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yanayotarajija kufanyika tarehe 5 Juni, 2022. Madhumuni ya maadhimisho haya ni kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na fursa zillizopo kwa ustawi wa jamii ya sasa na kizazi kijacho.

61. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2022 maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Kimataifa yatafanyika nchini Sweden na Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo ni: "Dunia ni moja, tujali mazingira yetu". Aidha, Kilele cha maadhimisho haya kitaifa kinatarajija kufanyika Jijini Dodoma. Katika maadhimisho hayo pamoja na mambo mengine Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira utazinduliwa. Maadhimisho ya Siku ya Kuhifadhi Tabaka la Ozoni Duniani

62. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi iliratibu maadhimisho ya Siku ya Ozoni Duniani yaliyokuwa na Kauli Mbiu ya "Montreal Protocol - Keeping us, our food and vaccines cool" ambayo huadhimishwa tarehe 16 Septemba kila mwaka. Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika Jijini Dodoma yakiongozwa na Kauli Mbiu isemayo: "Tulinde Afya ya binadamu, hifadhi ya chakula na kuhakikisha chanjo za UVICO 19 zinakuwa salama". Katika maadhimisho hayo shughuli zilizofanyika ni pamoja na: kutoa tamko la Serikali kuhusu maadhimisho ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni; kukagua karakana zinazojishughulisha na matengenezo ya majokofu na viyoyozi vyta magari na majumbani katika majiji ya Dodoma na Dar Es Salaam kwa lengo la kuhamasisha uzingatiaji wa Kanuni za Udhhibit na Usimamizi wa Kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni za mwaka 2007; kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulinda Tabaka la Ozoni kupitia vipindi sita (6) vyta redlo na vipindi viwili (2) vyta Runinga; na kutoa mafunzo kwa maafisa forodha na wataalam kumi na tisa (19) kutoka Mamlaka za Usimamizi wa Kemikali kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni. Vilevile, mafunzo maalum yalitolewa kwa mafundi mchundo 40 wanaojishughulisha na utengenezaji wa majokofu na viyoyozi.

(vii) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi

63. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Glasgow, Uskochi (Scotland) kuanzia tarehe 25 Oktoba hadi 12 Novemba, 2021 ambapo Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na ulishiriki katika Masuala muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano huo ambayo ni pamoja na: Uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi; Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukabiliana

na athari za mabadiliko ya tabianchi; Upatikanaji na uhawilishaji wa teknolojia; Kujenga uwezo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Utafiti na sayansi ya mabadiliko ya tabianchi; Upunguzaji wa gesi-joto; na Athari za sera za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Tanzania iliwasilisha andiko la mchango wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Nationally Determined Contribution).



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia katika Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi COP26 uliofanyika katika Mji wa Glasgow, Scotland tarehe 02 Novemba, 2021.

Mkutano wa Tano wa Nchi Wanachama wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira

64. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Tano wa Nchi Wanachama wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira uliofanyika tarehe 28 Februari – 04 Machi, 2022 Nairobi, Kenya. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Masuala muhimu yaliyopitishwa na nchi wanachama katika mkutano huo ni pamoja na: kuanzishwa kwa Mkataba wa udhibiti wa uchafizi wa mazingira utokanao na taka za plastiki; kuweka mikakati ya hifadhi ya bionuai na athari za mabadiliko ya Tabianchi; na

upatikanaji wa rasilimali fedha na kujenga uwezo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za mazingira. Katika mkutano huo, Tanzania iliahidi kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazoikabili dunia.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akitoa salamu za Tanzania kwa niaba ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano maalum wa miaka 50 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) uliofanyika Machi 3, 2022 jijini Nairobi, Kenya.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis (kulia) na Balozi wa Tanzania nchini Kenya Mhe. Dkt. John Simbachawene wakishiriki ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEA 5) Nairobi nchini Kenya

Mkutano wa Tisa wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika

65. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tisa wa Mawaziri wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika uliofanyika katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji tarehe 16 Desemba, 2021 ambao ulishirikisha nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Tanzania. Mgeni rasmi katika Mkutano huo alikuwa ni **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Masuala muhimu yaliyojadiliwa na kupitishwa katika mkutano huo ni pamoja na kuanzisha taratibu mahsus za kikanda za uvuvi endelevu katika Ziwa Tanganyika; na kuendeleza ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya kitaifa na kikanda ya usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika. Aidha, katika mkutano huo Tanzania ilikabidhiwa uenyekiti wa nchi wanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Desemba, 2021 hadi Desemba, 2022.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza wakati wa ufunguzi Mkutano wa Tisa wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika uliofanyika mkoani Kigoma.

(viii) Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

66. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hicho jumla ya miradi nane (8) ilitekelezwa kama ifuatavyo: -

Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia

67. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia unaotekelezwa katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini A Unguja, Zanzibar. Lengo la mradi ni kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini Tanzania. Katika kipindi hiki, kiasi cha **Shilingi 1,880,662,028** kilitumika. Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoaribika na kuongeza usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania

68. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoaribika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini katika Wilaya za Magu (Mwanza), Nzega (Tabora), Mkalama (Singida), Kondoa (Dodoma) na Micheweni (Pemba), Zanzibar. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo - ikolojia ili kuongeza usalama wa chakula katika maeneo husika. Katika Kipindi hicho, kiasi cha **Shilingi 1,040,000,000** kilitumika.

Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria

69. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliendelea kutekeleza mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria katika Wilaya ya Magu mkoani Mwanza. Lengo la mradi huu ni kuwezesha jamii zinazoishi katika maeneo ya

Ziwa Victoria kuweza kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo yao. Katika kipindi hicho, kiasi cha **Shilingi 439,274,405** zilitumika.

Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai katika mifumo ikolojia ya Bonde la Ruaha Mkoo na Ziwa Rukwa

70. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeanza kutekeleza Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai katika mifumo ikolojia ya Bonde la Ruaha Mkoo na Ziwa Rukwa. Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo - ikolojia na jamii kwa ujumla nchini Tanzania. Mradi huu utatekelezwa katika Wilaya za Iringa Vijijini, Mbeya Vijijini, Mbarali, Wanging'ombe, Tanganyika, Mpimbwe na Sumbawanga Vijijini. Jumla ya **Shilingi 643,619,178.76** zilitumika.

Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu

71. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kuratibu Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu. Lengo la mradi ni kulinda afya ya binadamu na mazingira kutokana na athari za kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu. Kiasi cha **Shilingi 248,646,090** kimetumika.

Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu nchini

72. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu nchini. Lengo la mradi ni kuiwezesha Tanzania kuwa tayari katika utekelezaji wa makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa

Mabadiliko ya Tabianchi na kunufaika na biashara ya hewa ukaa. Kiasi cha **Shilingi 279,045,948.87** kimetumika.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhhibit wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

73. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi unaolenga kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhhibit wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni ambapo kiasi cha **Shilingi 102,590,610** kilitumika.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira nchini. Lengo la mradi ni Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambapo kiasi cha **Shilingi 641,900,000** kimetumika.

MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

75. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/22 Ofisi imeendelea kusimamia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Utumishi wa Umma na imewezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, utendaji kazi wa watumishi umeendelea kupimwa kwa kutumia mfumo wa wazi wa Tathmini na Mapitio ya Utendaji Kazi (OPRAS).

76. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho jumla ya watumishi **94** wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo na kuongeza ujuzi na maendeleo kulingana na kada zao ambapo watumishi **10** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi **84** walihudhuria

mafunzo ya muda mfupi. Aidha, katika kuendelea kuboresha mazingira ya kazi, Ofisi imenunua vitendea kazi kwa ajili ya watumishi, ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais yaliyoko Kilimani - Dodoma na kuanza ujenzi wa Ofisi ya kudumu ya Makamu wa Rais awamu ya pili Mtumba Dodoma.

CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

77. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Makamu wa Rais inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: Kuendelea kuwepo kwa hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi; kutotekelawa kikamilifu kwa Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Mazingira katika ngazi ya Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Muungano na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; uzingatiajji mdogo wa jamii kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira; na kuongezeka kwa madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya Tabianchi.

78. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto hizi, hatua zifuatazo zimechukuliwa:- kuandaa Andiko la Historia ya Muungano litakalotumika kuelimisha umma kuhusu faida za Muungano kiuchumi, kijamii na kislasa; kuendelea kutafuta ufumbuzi wa hoja za Muungano ambazo hazijatatuliwa; kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu kuimarisha muundo wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuratibu shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira katika Wizara za Kisikta na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuendelea na majadiliano na Wizara za Kisikta kuhusu kuimarisha uratibu wa masuala ya mazingira katika sekta husika; na kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu Masuala ya Muungano, Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

79. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, Mpango Mkakati wa Baraza 2021/22 – 2025/26, miongozo na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira ili kuleta maendeleo endelevu hapa nchini.

(v) *Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira Sura 191*

Ukaguzi wa Maeneo ya Uwekezaji na Mazingira

80. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Baraza limefanya kaguzi katika miradi **2,455** kwa dhumuni la kutathimini uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Changamoto kubwa za kimazingira zillizobainika kufuatia kaguzi hizo ni: utiririshaji wa majitaka kwenye mazingira ikiwemo vyanzo vyya maji na makazi ya watu; Matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu ya asili kwa ajili ya nishati na ujenzi; Ukosefu wa mifumo ya kuhifadhi, kurejeleza na kuteketeteza taka ngumu na taka hatarishi; Uzalishaji wa hewa chafu; Uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala isiyokidhi viwango; Upigaji wa kelele na mitetemo zaidi ya viwango vinavyoruhusiwa kikanuni; na uchafuzi wa mazingira katika masoko na machinjio. Changamoto hizi pamoja na mambo mengine zinatokana na kutozingatiwa kwa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za Mipango Miji.

81. *Mheshimiwa Spika*, Hatua zilizochukuliwa kutoingatiwa na changamoto hizo ni pamoja na kutoa ushauri, maelekezo, onyo na amri ya kizuizi kwenye shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira, amri za urejeshaji wa mazingira na faini. Jumla ya miradi **2,105** ilipewa ushauri na maelekezo, miradi 350 ilipewa amri ya kizuizi kulinda mazingira. Hatua hizi zimesaidia kulinda afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira.

82. *Mheshimiwa Spika*, Baraza limepokea malalamiko kuhusu uchafuzi wa mazingira na kuyapatia ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Katika kipindi hicho, jumla ya malalamiko **369** yalipokelewa. Malalamiko hayo yalihusu kelele kutoka kwenye kumbi za starehe na mitetemo, utirishaji majitaka na uchafuzi wa hewa kutoka viwandani, utupaji holela wa taka ngumu, uchimbaji wa mchanga katika vyanzo vya maji na maeneo mengineyo. Malalamiko **359** yalishughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutoa ushauri, maelekezo, onyo na amri mbalimbali za kimazingira. Jumla ya malalamiko **300** yalitatuliwa kuititia ushauri na maelekezo na malalamiko **59** kutatuliwa kuititia maonyo na amri mbalimbali za kimazingira. Aidha, Baraza limeendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Jeshi la Polisi kushughulikia malalamiko hayo.

Udhibiti wa Taka Hatarishi

83. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza limepokea maombi **36** ya usimamizi wa uteketezaji wa taka hatarishi ikiwa ni pamoja na dawa na bidhaa za viwandani zilizokwisha muda wake na kemikali zisizofaa kwa matumizi. Kiasi cha tani **660** za taka hizo zimeteketezwa kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tibu, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(vi) *Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)*

Usajili wa Miradi na Utoaji wa Vyeti vya Mazingira

84. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza lisisajili jumla ya miradi **1,702** ambapo miradi **339** ilisajiliwa kwa njia ya kawaida yaani kuwasilisha nakala ngumu na miradi **1,363** ilisajiliwa kwa mfumo wa ki-elektroniki. Kati ya hiyo, miradi **967** ni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Miradi **735** ni ya Ukaguzi wa Mazingira. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya miradi **731** imeidhinishwa na kupata vyeti vya mazingira, sawa na ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na

mwaka 2020/21. Kati ya miradi hiyo iliyopata vyeti, miradi **573** ni ya TAM na Miradi **158** ni ya Ukaguzi wa Mazingira. Aidha, miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za upembuzi. Ongezeko hili limetokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki unaotumika katika utoaji wa vyeti.

Usajili na uhakiki wa Wataalam Elekezi wa Mazingira

85. *Mheshimiwa Spika*, Baraza limeendelea kusimamia utendaji kazi wa Wataalam Elekezi na Kampuni za Ushauri ili wawze kutoa ushauri wa masuala ya mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Vile vile, daftari la wataalam elekezi waliosajiliwa na Baraza na wenye sifa za kufanya kazi za TAM na Ukaguzi wa Mazingira limeendelea kuhuishwa. Jumla ya wataalam elekezi **164** wa TAM na **102** wa ukaguzi wa Mazingira pamoja na kampuni za ushauri **70** za TAM na **51** za ukaguzi wa mazingira ziko hai katika utoaji wa huduma ya utalaam elekezi.

(vii) Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi ya Mazingira

Kukuza Uelewa na Kujenga Uwezo wa Wadau Kuhusu Hifadhi ya Mazingira

86. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Baraza limetoa elimu ya mazingira kupitia vyombo vya habari ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Aidha, Baraza lilishiriki katika maadhimisho mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu ya mazingira kwa Jamii.

MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23 MASUALA YA MUUNGANO

(i) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano

87. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2022/23, Ofisi itaendelea Kuratibu utatuzi wa changamoto zilizobakia na

zitakazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kupitia Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Vikao hivi vitafanyika katika ngazi tatu (3) ambazo ni: - Kamati ya Pamoja; Mawaziri; na Makatibu Wakuu. Aidha, kutakuwa na Vikao vya Kamati Ndogo za Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala vitakavyofanyika kulingana na mahitaji. Vikao hivyo vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

(ii) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii

88. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelawa pande mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi inayotekelawa kwa fedha za Kuchochera Mfuko wa Jimbo, Zanzibar. Aidha, Ofisi itatoa mafunzo ya usimamizi wa miradi inayoghamariwa na fedha za mfuko wa jimbo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na wataalamu katika Halmashauri za Zanzibar.

(iii) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/23, Ofisi itaendelea na uratibu wa masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Taasisi za SJMT na SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana.

(iv) Kutoa Elimu ya Muungano kwa Umma

90. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/23, Ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma kwa makundi tofauti ya kijamii kupitia njia mabalimbali ikiwemo kupitia Redio, Runinga, Magazeti, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na Mitandao ya Kijamii kwa lengo la kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu.

(v) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano

91. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/23, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 4(3) kama yalivyoordheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ambapo pamoja na mambo mengine, Ofisi inatakiwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mambo ya Muungano na kuchukua hatua kwa changamoto zinazobainika.

HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA

92. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha hifadhi endelevu ya mazingira, kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele sita (6) vifuatavyo: Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021; Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa hifadhi ya Mazingira; kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; kuratibu utekelezaji wa Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira; kuendelea kujenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi; na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

(i) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021

93. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2022/23, Ofisi itaendelea kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Mikakati mbalimbali ya Hifadhi ya Mazingira katika sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191

94. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 katika Wizara za Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi itaratibu mapitio ya Sheria hiyo ili kuzingatia matakwa ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali ya utekelezaji wake. Vilevile, Ofisi

itaendelea kuchambua maombi na kutoa vibali nya mazingira ikiwa ni pamoja na vibali nya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM); Ukaguzi wa Mazingira; Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK); na taka hatarishi ikiwemo taka za kielektroniki.

(iii) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa hifadhi ya Mazingira

95. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaanza utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira kupitia miradi inayotekelzeza na kuibua miradi mipyä ya Hifadhi ya Mazingira katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, katika utekelezaji wa mpango huu, mwongozo kuhusu utekelezaji wa miradi ya mazingira nchini utatolewa.

(iv) Kuratibu utekelezaji wa Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira

96. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira kwa kuhamasisha wadau mbalimbali kuongeza kasi ya upandaji miti, uhifadhi wa vyanzo nya maji, udhibiti wa taka ngumu na taka hatarishi, uzalishaji endelevu viwandani, kuongeza matumizi ya nishati mbadala, udhibiti wa viumbe vamizi, kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, uchimbaji endelevu wa madini, kilimo, ufugaji na uvuvi endelevu.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza na Mkuu wa Jershi la Kujenga Taifa (JKT) Brigedia Jeneralis Rajabu Mabele pamoja na Mkuu wa Kikosi namba 834 JKT Makutupora, Dodoma, Luteni Kanali Festo Mbanga wakati alipokuwa akitoa maagizo ya upandaji miti pembezoni mwa barabara ya kuingia jiji la Dodoma Machi 26,2022.

(v) Kuratibu utekelezaji wa Mpango - Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu Nchini (2020 – 2025)

97. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu athari za Zebaki na kuhamasisha matumizi salama ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. Aidha, Ofisi itaendelea kushirikiana na Mamlaka za udhibiti kuimarissha udhibiti wa uingizaji zebaki nchini ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa wa Mamlaka hizo.

(vi) Elimu kwa Umma

98. Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na: vyombo vyta habari na mitandao ya kijamii; maadhisho ya Kitaifa na Kimataifa ya Mazingira; ziara za Viongozi; Mabalozi wa Mazingira; semina na warsha; makongamano; machapisho; matangazo; na maonesho. Aidha, Ofisi itaendelea kutekeleza Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira inayolenga kutoa elimu na kuhamasisha umma kushiriki katika shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira. Vilevile, Ofisi itaendelea kutekeleza Kampeni ya Soma na Mti inayolenga kujenga tabia ya kupanda na kutunza miti kwa wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.

99. Mheshimiwa Spika, masuala mengine yatakayotekelawa ni pamoja na: - Kuhifadhi Mazingira ya Vyanzo vyta Maji; udhibiti wa taka ngumu; kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na kimataifa ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na Itifaki zake; kuratibu maadhisho ya siku ya mazingira duniani; na kuendelea kufuatilia Kampeni ya Kitaifa ya upandaji miti milioni 1.5 kwa mwaka kwa kila Halmashauri, na Kampeni ya Kukijanisha Dodoma.

(vii) Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

100. *Mheshimiwa Spika*, Kwa mwaka 2022/23, Ofisi itaratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo: -

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa

101. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu utagharimu **Shilingi 2,987,654,000.00** na unatekelezwa katika Wilaya za Ludewa na Makete (Njombe), Kyela (Mbeya), Nyasa na Mbinga (Ruvuma). Lengo la Mradi ni kuhifadhi mazingira ya bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya jamii inayozunguka eneo hilo. Katika mwaka 2022/23, **Shilingi 736,967,714.00** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii ili kukabiliana na uharibifu wa ardhi.

Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai

102. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu utagharimu **Dola za Marekani 11,205,872.00**. Lengo la mradi ni kurejesha uoto wa asili na hifadhi ya bioanuai kupitia usimamizi jumuishi wa mifumo ikolojia. Mradi huu unatekelezwa kwenye Bonde la Ruaha Mkuu na Ziwa Rukwa katika Wilaya za Iringa Vijijini, Mbeya Vijijini, Mbarali, Wanging'ombe, Tanganyika, Mpimbwe na Sumbawanga Vijijini. Katika mwaka 2022/23, **Shilingi 5,775,235,425.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na urejeshaji wa misitu na mazingira.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

103. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23, **Shilingi 94,775,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendesha mafunzo

kwa mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu kutoka Zanzibar na kukusanya takwimu za matumizi ya kemikali husika.

Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu

104. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23, Shilingi 339,427,360.00 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo kuandaa Mpango wa Kitaifa wa uondoshaji wa kemikali zinazodumu katika mazingira jamii ya Polychlorinated Biphenyls (PCBs); na Kutekeleza mradi wa majoribio unaohusisha ujenzi wa vituo vyta kukusanya na kuchakata taka zinazorejelezeka katika Manispaa za Ubungo na Kigamboni.

Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania

105. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23, Shilingi 2,750,521,020.00 zimetengwa kwa ajili ya uchimbaji wa malambo, ujenzi wa mabwawa, ujenzi wa mifumo ya uvunaji maji ya mvua, ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo na majosho, kukarabati tuta la kuzuia maji ya bahari katika bonde la Koowe - Micheweni Pemba.

Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia

106. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23 Shilingi 7,370,839,681.00 zimetengwa kwa ajili utekelezaji wa shughuli za mradi ikiwemo uchimbaji wa malambo; ujenzi wa majosho na mabirika ya kunyweshea mifugo; kuwezesha ufugaji endelevu; na miradi mingine rafiki kwa mazingira katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu

107. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23 Shilingi 965,194,800.00 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha

Mwongozo wa Taifa wa Kupunguza Hewa Ucaa; kuhuisha Mkakati wa Kupunguza Uharibifu wa Misitu na Ukataji Miti katika Sera na Mipango ya Wizara za Kisekta; na kujenga uwezo wa taasisi katika kusimamia na kuratibu shughuli za kupunguza hewa ucaa.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

108. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23 **Shilingi 826,736,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha kanzidata ya usimamizi wa taka nchini; kufanya tathmini ya ufanisi wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi katika kutekeleza Sheria hiyo.

Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Kingo za fukwe katika maeneo ya mwambao Mikindani Mtwara na Sipwese Zanzibar

109. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2022/23 kiasi cha Shilingi **282,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kingo katika fukwe za Mikindani na Sipwese.

MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI

110. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kuajiri na kupandisha vyeo watumishi kwa kuzingatia utendaji kazi na miundo inayotawala kada zao. Aidha, Ofisi itaendelea kusimamia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na kuimarisha Maadili na Utawala Bora katika Utumishi wa Umma. Ofisi itawezesha watumishi kushiriki mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi. Mafunzo ya muda mfupi yatahusisha mafunzo ya uongozi, usimamizi wa miradi, maadili na itifaki pamoja na kutoa elimu na ushauri kuhusu masuala ya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza na UVIKO - 19. Vilevile, Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia Watumishi vitendea kazi pamoja na stahili zao.

111. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2022/23 Ofisi itaendelea kusimamia ujenzi wa awamu ya pili wa Ofisi ya Makamu wa

Rais, Mtumba - Dodoma ili 69 kuwezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

112. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2022/23 Baraza limepanga kuendelea kutekeleza kazi zifuatazo: kuratibu mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kusajili na kufanya mapitio ya miradi na kusajili Wataalam Elekezi wa Mazingira; kuendelea kutoa elimu kwa umma na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya mazingira; kushirikiana na wadau kuandaa miongozo ya kisekta kwa lengo la kurahisisha mapitio ya taarifa za TAM za sekta husika; kuendelea na kaguzi za mazingira katika maeneo mbalimbali ili kulinda na kutunza mazingira; kufanya tafiti za mazingira; kukamilisha tathmini ya eneo la Rufiji-Mafia-Kibiti-Kilwa (RUMAKI) ili kujumuishwa katika Mtandao wa Dunia wa Binadamu na Hifadhi Hai uliopo Chini ya Shirika la Kimataifa la UNESCO; na kuendelea kuratibu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na kujenga weledi wa wadau kuhusu utekelezaji wa Sheria.

HITIMISHO NA SHUKRANI

113. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake, dira na maelekezo aliyotupatia kuhusu majukumu yetu. Aidha, ninamshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake pamoja na maelekezo anayotupatia katika kutekeleza majukumu. Vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutusimamia vema katika kutekeleza majukumu yetu. Ninapenda pia kumshukuru **Mheshimiwa Khamis H. Khamis (Mb.)**, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Ninazishukuru pia Kamati

za Kudumu za Bunge za Katiba na Sheria na Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kazi kubwa waliyofanya ya kupitisha bajeti hii ni nayoiwasilisha kwa mwaka 2022/23.

114. *Mheshimiwa Spika*, Vilevile, ninapenda kuwashukuru **Bi. Mary N. Maganga**, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; **Bw. Abdallah H. Mitawi**, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano); na **Bw. Edward G. Nyamanga** Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Ninawashukuru pia **Prof. Mhandisi Esnath O. Chaggua**, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira, **Dkt. Mhandisi Samwel G. Mafwenga**, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Pia ninawashukuru wale wote wallotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23.

115. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na Wadau mbalimbali. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway; Serikali ya Sweden; Umoja wa Nchi za Ulaya - *EU*; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa - *UNDP*; Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa - *UNEP*; Mfuko wa Mazingira wa Dunia - *GEF*; Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika - *AfDB*; *CRDB*; *UNCDF*; *Foreign and Commonwealth Development Organization* (*FCDO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda - *UNIDO*; Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani - *WWF*; Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - *IFAD*; Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi - *GCF*; Shirika la Kilimo na Chakula Duniani - *FAO*; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani - *GIZ*; Asasi Zisizo za Kiserikali (*AZISE*); Sekta Binafsi; Kamati Maalum ya Usimamizi wa Kampeni Kabambe, na Mabalozi wa Mazingira. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi katika kuimarisha Muungano wetu na kuhifadhi mazingira yetu.

MAOMBI YA FEDHA

116. *Mheshimiwa Spika*, ili Ofisi iweze kufikia malengo tarajiwa kama nilivyobainisha kwenye hotuba yangu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2022/23 kama ifuatavyo: -

FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS

117. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 12,974,292,000** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 974,292,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na **Shilingi 12,000,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

118. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya Matumizi ya Shilingi 40,142,025,000.00 kwa ajili ya Fungu hili. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 18,180,328,000.00** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 21,961,697,000.00** ni Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **Shilingi 3,297,558,270.00** Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 4,362,627,730.00** Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na **Shilingi 10,520,142,000.00** Matumizi Mengineyo. Aidha, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo yanajumuisha **Shilingi 3,602,000,000.00** fedha za Ndani na **Shilingi 18,359,697,000.00** fedha za Nje.

119. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, aje awasilishe maoni ya Kamati.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa ya hii iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; uchambuzi wa Kamati umejkita katika mafungu mawili ya bajeti ya Ofisi hiyo ambayo ni Fungu 26 – Makamu wa Rais, pamoja Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano. Matokeo ya uchambuzi huo yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu Na. 26 - Makamu wa Rais hawakuwa na maoteo ya makusanyo ya Maduhuli yaliyokadiriwa kukusanya. Hii ni kutokana na muundo na majukumu ya ofisi hiyo. Kwa upande wa Fungu Na. 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) liliidhinishiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 6,800,000/= katika mwaka wa fedha 2021/2022. Maduhuli hayo yalitatarajiwa kutoka kwenye mauzo ya zabuni. Hadi kufika Februari, 2022 Kamati ilibaini kwamba Fungu Na. 31

halikuwa limekusanya maduhuli yoyote kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 21,338,212,360/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi hiyo ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 12,638,405,794.5 sawa na asilimia 59.11 ya bajeti iliyoidhinishwa. Jedwali Na. 1 linatoa mchanganuo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa asilimia 59.11 ya makadirio unaridhisha ingawa iko chini ya matarajio. Aidha, Kamati imebaini kwamba hakuna uwiano katika mapokeo ya fedha hizo baina ya mafungu haya mawili. Ni vyema Serikali ikawa na utaratibu wa kutoa fedha na matumizi ya kawaida kwa uwiano ulio sawa kwa kila fungu kulingana na bajeti waliyoidhinishiwa na Bunge na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Kamati imebaini ni kwamba katika Shilingi 12,915,077,000/= illyotengwa kwa Matumizi ya Kawaida katika Fungu Na. 26 - Makamu wa Rais, Shilingi 984,112,000,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya Mshahara na Shilingi 11,930,965,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2022 fungu hilo lilikuwa limepokea Shilingi 455,456,000/= kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 46.28 ya makadirio, na Shilingi 7,804,495,960.67 kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 65.41. Mapokezi ya asilimia 44.28 katika bajeti ya mishahara katika Fungu Na. 26 hayaridhishi kwa sababu Serikali inayo wajibu wa kuhakikisha kwamba mishahara ya watumishi wake inafika kwa wakati na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 3,880,000,000/= kwa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha hizo zilitengwa katika Kifungu Na. 31 ili kutekeleza Mradi Na. 6309 ambao ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ukarabati wa ofisi na makazi ya Makamu wa Rais, Tunguu, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2022 ofisi hiyo ilikuwa imepocha jumla ya Shilingi 2,376,797,800.26 sawa na asilimia 56 ya bajeti iliyooombwa. Kiasi hiki kinajumuisha Shilingi 120,089,211,211 iliyopokelewa kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Makamu wa Rais, na Shilingi 1,234,853,850 kwa ajili ya kulipia fidia wananchi waliokuwa wakiishi karibu na ofisi na makazi ya Makamu wa Rais Tunguu. Aidha, Shilingi 1,021,848,738.7.3 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kutekeleza mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitaarifiwa kwamba mradi huo upo katika hatua ya utekelezaji na kwamba ofisi na makazi hayo sasa yatatumika na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo Zanzibar. Kwa maana hiyo, Serikali inapaswa kujenga jengo jipya kwa ajili ya ofisi na makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 26,383,964,470/. Kati ya fedha hizo, shilingi 3,335,625,770 ni mishahara; shilingi 20,228,339,200 ni Matumizi Mengineyo; na shilingi 2,820,000,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Jedwali Na. 2 linatoa mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mafungu yote mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mpango wa Maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Makamu wa Rais imetenga shilingi 2,820,000,000 ili kutekeleza Mradi Namba 6309 - ukarabati wa ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo pamoja na maandalizi ya ujenzi mpya wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kiasi cha bajeti ya maendeleo kimepungua kwa asilimia 27.32 Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa kuendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi yake kwa kutumia fedha za ndani. Hatua hii inachochea juhudzi za Serikali nzima kukusanya mapato lakini pia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma hasa kwa kuzingatia kuwa fedha hizo ni makusanyo yanayotokana na malipo ya kodi nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya kutoa maelezo ya Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 naomba kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: - Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia Februari 2022 hakuna mapato yoyote yaliyokusanywa na Kifungu Na. 31 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa ukusanyaji. Mabadiliko hayo yameanzisha mfumo mpya unaoweka utaratibu, ambapo maduhuli yatokanayo na zabuni hukusanywa kwa pamoja kuititia mfumo wa manunuzi ya umma kwa njia ya mtandao (*TANePS*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, ili kuweka utaratibu mzuri wa kibajeti ni vyema ofisi hiyo ikaondoa kipengele cha makusanyo katika makadirio ya mapato iwapo ofisi hiyo haina vyanzo vyake vya makusanyo vya maduhuli kwa ajili ya utendaji wake.

Pili, kwa kuzingatia kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano imepewa jukumu kuu la kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo na Muungano, Kamati inashauri ofisi hiyo kutoa elimu ya kutosha kuhusu historia, faida na umuhimu wa Muungano wetu katika ngazi mbalimbali za elimu mashulenii, makundi maalum kuititia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Serikali kuititia Wizara na Taasisi zake ihamasithe walimu na wakufunzi katika ngazi mbalimbali za elimu kuwa na *programza* kubadilishana

na kupeana uzoefu kutoka pande mbili za Muungano, ili kuleta uelewa wa pamoja kuhusu suala la upekee wa Muungano wetu na faida zake. Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa kuandaa na kuzindua rasmi kitabu kinachohusu historia ya Muungano. Kitabu hiki ni nyenzo muhimu katika kuweka kumbukumbu sahihi ya misingi na historia ya Muungano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kitabu hicho kinasambazwa kote nchini na pia kinawekwa katika nakala tete ili kurahisisha upatikanaji wake katika mitandao ya *internet* ikijumuisha mitandao ya Kijamii. Pamoja na kwamba Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maoni na ushauri ambao iliutoa, Kamati inaendelea kusisitiza Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira katika Taasisi ya Muungano. Kamati inaendelea kuishauri Serikali Izingatilie pia uwiano wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za ajira katika Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya utofauti wa kikodi kati ya bidhaa zinazoingizwa Tanzania Bara kutoka Tanzania Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali na Taasisi zake zote zinazohusika na jambo hili kuendeleza juhudzi za kutafuta suluhisho la kudumu la changamoto hizo. Aidha, juhudzi hizo ziende sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano ili kupunguza malalamiko ambayo yanaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayofanyiwa ukarabati katika eneo la Tunguu Zanzibar sasa itatumwiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, hadi kufikia Februari 2022 fedha zilizotengwa kufanya ukarabati huo zilifikia kwa asilimia 56 tu. Kamati inaishauri Serikali itoe fedha kamili ili kutekeleza mradi huo kwani unategemea fedha za ndani kwa asilimia 100. Vile vile,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kamati inashauri Serikali kuharakisha kujenga Ofisi mpya Zanzibar itakayotumiwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii na kuiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo Mbunge Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa ushirikiano wao ambao umesaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi hiyo chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Mary Maganga Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira akisaidiwa na Ndugu Abdallah Ali Mitawi Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Ndugu Nenelwa Mwihambi Katibu wa Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na shughuli za Bunge. Baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti. Kabla hujatoka hapo kwenye maoni na ushauri wa Kamati ulipokuwa unasoma namba tatu, maoni na ushauri wa Kamati, ulipokuwa unasoma, nadhani imeandikwa hapo, Kamati inapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu Muungano. Nafikiri Kamati ilikusudia kusema Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, ili taarifa zetu rasmi za Bunge zikae vizuri.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Haya, sema sasa wewe ili tufanye marekebisho. Ahsante sana.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa kuandaa na kuzindua rasmi kitabu kilichohusu historia ya Muungano. (*Makofii*)

TAARI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ninayowasilisha imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi

b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na namna Serikali ilivyozingatia maoni ya Kamati

c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati

e) Sehemu ya Tano ni na Hitimisho

1.2 Namna Kamati Ilivyotekeliza Majukumu Yake

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya kikao na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) tarehe 28 Machi, 2022. Katika kikao hicho Wajumbe walifanya mambo yafuatayo: -

a) Kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

b) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya hiyo pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

c) Kutoa maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

2.1 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi unatokana na **Kifungu cha 7 (1) (a)** kikisomwa pamoja na **Kifungu cha 6 (2) (c)** cha **Nyongeza ya Nane** ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 118 (4)**. Kanuni hizi zimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) sambamba na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo.

2. 2 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umejikita katika mafungu mawili ya kibajeti ya Ofisi hiyo ambayo ni **Fungu 26** – Makamu wa Rais pamoja na **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Matokeo ya uchambuzi huo yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Hivyo basi, ili kulisaidia Bunge kufuatilia ipasavyo Taarifa ya Kamati na kuweza kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 naomba kubainisha mambo makuu manne ambayo Kamati imeyafanya uchambuzi katika Bajeti ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2021/2022: -

- a) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati
- b) Makusanyo ya Maduhuli
- c) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

d) Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

2.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati kwa ukamilifu, lakini kuna maeneo machache ambayo Serikali bado hajazingatia.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni pamoja na ushauri kuhusu ununuzi wa magari pamoja na uboreshaji wa vitendea kazi vya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati ilishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na kuboresha vitendea kazi. Kamati imebaini kwamba Ofisi hiyo imeanza kuboresha vitendea kazi na imenunua magari nane (8).

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri na maoni ambaeo bado unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, ni ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuratibu jitihada za kutafuta suluhisho la kudumu ili kuzipatia ufumbuzi changamoto za kifedha na kikodi. Kamati imebaini kwamba, bado kuna changamoto ya malalamiko ya mara kwa mara kuhusu utofauti wa kikodi katika bidhaa zinazoingizwa baina ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua ambazo tayari imechukua ikiwemo kufanyika maandalizi ya kujenga Mfumo wa Uthaminishaji wa Moja kwa Moja (*Auto - Valuation*) ambaeo utatumika kupata ufumbuzi wa hoja hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu, ni vema Ofisi ya Makamu wa Rais ikafuatilia na kutoa taarifa kwa Kamati kuhusu maendeleo ya jitahada hizo za Serikali ili hoja hii ipate ufumbuzi wa kudumu, mapema iwezekanavyo.

2.4 Uchambuzi Kuhusu Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Fungu 26** - Makamu wa Rais hakukuwa na maoteo ya makusanyo ya maduhuli yaliyokadiriwa kukusanya, hii ni kutohana na Muundo na Majukumu ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), fungu hilo liliidhinishiwa kukusanya kiasi cha **Sh. 6,800,000** Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Maduhuli hayo yalitarajiwa kutoka kwenye mauzo ya zabuni. Hadi kufikia Februari, 2022 Kamati imebaini kwamba, **Fungu 31** halikuwa limekusanya maduhuli yoyote kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba malengo ya makusanyo hayakufikiwa kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa ukusanyaji maduhuli Serikalini. Mabadiliko hayo yameweka utaratibu ambapo makusanyo ya maduhuli yatokanayo na zabuni hukusanya kwa pamoja kuititia Mfumo wa Manunuzi ya Umma Kwa Njia ya Mtandao (TANEPS) na hivyo basi fedha zinaingia moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa HAZINA.

2.5 Uchambuzi Kuhusu Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) iliidhinishiwa Jumla ya **Sh. 21,382,212,360** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi hiyo ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 12,638,405,794.5** sawa na **asilimia 59.11** ya bajeti iliyoidhinishwa. Jedwali Na. 1 linatoa mchanganuo huo.

Jedwali Na. 1 – Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2021/2022

FUNGULA KIBAJETI	FEDHA ILIYOTENGWA KATIKA BAJETI YA 2021/2022 (TZS)	FEDHA ILIYOPOKELEWA KUFIKIA FEBRUARI, 2022 (TZS)	ASILIMIA YA MAPOKEZI
Fungu 26 – Makamu wa Rais	12,915,077,000	8,259,951,960.67	64%
Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)	8,467,135,360	4,378,453,833.83	52%
JUMLA	21,382,212,360	12,638,405,794.5	59.11%

Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa **asilimia 59.11** ya Makadirio unaridhisha ingawa uko chini ya matarajio. Aidha, Kamati imebaini kwamba, hakuna uwiano katika mapokezi ya fedha hizo baina ya mafungu haya mawili. Ni vema Serikali ikawa na utaratibu wa kutoa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa uwiano ulio sawa kila Fungu kulingana na bajeti waliyoidhinishiwa na Bunge na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Kamati imebaini ni kwamba, katika **Sh. 12,915,077,000** iliyotengwa kwa Matumizi ya Kawaida katika **Fungu 26** – Makamu wa Rais, **Sh. 984,112,000** zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 11,930,965,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2022 Fungu hilo lilikuwa limepokea **Sh. 455,456,000** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 46.28** ya makadirio, na **Sh. 7,804,495,960.67** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na **asilimia 65.41**.

Mheshimiwa Spika, mapokezi ya **asilimia 46.28** katika Bejeti ya Mishahara katika **Fungu 26** hayaridhishi kwa sababu Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kwamba Mishahara ya Watumishi wake inafika kwa wakati na kwa ukamilifu.

2.6 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) illidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,880,000,000** kwa Fedha za Ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zilitengwa katika **Fungu 31** ili kutekeleza **Mradi Na. 6309 ambao ni Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**, Tunguu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi hiyo ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 2,376,797,800.26** sawa na **asilimia 56** ya bajeti iliyombwa. Kiasi hiki kinajumuisha **Sh. 120,089,211.53** iliyopokelewa kwa ajili ya ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais, na **Sh. 1,234,853,850** kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliokuwa wakiishi karibu na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Tunguu. Aidha, **Sh. 1,021,848.738.73** ilitolewa kwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kutekeleza mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitaarifiwa kwamba, mradi huo uko katika hatua za utekelezaji, na kwamba Ofisi na Makazi hayo sasa yatatumika na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awapo Zanzibar. Kwa maana hiyo, Serikali inapaswa kujenga jengo jipya kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Zanzibar.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,383,964,470**. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 3,335,625,270** ni Mishahara, **Sh. 20,228,339,200** ni Matumizi Mengineyo (O.C) na **Sh. 2,820,000,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jedwali Na. 2 linatoa mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mafungu yote mawili.

FUNGUA KIBAJETI	FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA (TZS)		FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO (TZS)		JUMLA YA FEDHA KATIKA FUNGU (TZS)
	MSHAHARA	MATUMIZI MENGNEYO	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	
Fungu 26 – Makamu wa Rais	974,292,000	12,000,000,000	0.00	0.00	12,974,292,000
Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)	2,361,333,270	8,228,339,200	2,820,000,000	0.00	13,409,672,470
JUMLA KUU	3,335,625,270	20,228,339,200	2,820,000,000	0.00	26,383,964,470

Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais

3.2 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) imeongezeka kwa **asilimia 29.35** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko hili linaakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongezeke fedha kwa taasisi zake mbalimbali ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba Ofisi hiyo ifanye tathmini ya maoteo ya bajeti zake ili kuendana na hali halisi ya kiuchumi kwa kuzingatia mfumuko wa bei, na kiwango cha ongezeko la bajeti kinachokubalika katika Mchakato wa Kupanga Bajeti za Serikali, hasa katika Matumizi ya Kawaida.

3.3 Mpango wa Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Makamu wa Rais imetenga **Sh. 2,820,000,000** ili kutekeleza Mradi Na. 6309 – Ukarabati na Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo pamoja na maandalizi ya ujenzi mpya wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kamati imebaini kwamba fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni pungufu kwa **asilimia 27.32** ukililinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, Kamati imebaini kwamba Bajeti iliyotengwa ni Fedha za Ndani kwa asilimia mia moja (100%) kama ambavyo ilikuwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kiasi cha bajeti ya maendeleo kimepungua, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kuendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi yake kwa kutumia Fedha za Ndani. Hatua hii inachochea juhudhi kwa Serikali nzima kukusanya mapato, lakini pia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma hasa kwa kuzingatia kuwa fedha hizo ni makusanyo yatokayo kwa walipa kodi nchini.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya uchambuzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

i) Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2022 hakuna mapato yoyote yaliyokusanywa na **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa ukusanyaji. Mabadiliko hayo yameanzisha mfumo mpya unaoweka utaratibu ambapo maduhuli yatokanayo na zabuni hukusanywa kwa pamoja kuititia Mfumo wa Manunuzi ya Umma kwa Njia ya Mtandao (TANEPS). Kamati inashauri kwamba, ili kuweka utaratibu mzuri wa kibajeti, ni vyema Ofisi hiyo ikaondoa kipengele cha makusanyo katika Makadirio ya Mapato iwapo Ofisi hiyo haina vyanzo vyake vya makusanyo ya maduhuli kwa asili ya utendaji wake.

ii) Kwa kuzingatia kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) imepewa jukumu kuu la kuratibu masuala ya Muungano na

kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano, Kamati inashauri Ofisi hiyo kutoa elimu ya kutosha kuhusu historia, faida na umuhimu wa Muungano wetu katika ngazi mbalimbali za elimu mashulenii, makundi maalum, kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Sambamba na hilo Serikali kupitia Wizara na taasisi zake, ihamasishe waalimu na wakufunzi katika ngazi mbalimbali za elimu kuwa na programu za kubadilishana na kupeana uzoefu (*exchange programmes*) kutoka pande mbili za Muungano ili kuleta uelewa wa pamoja kuhusu suala la upekee wa muungano wetu na faida zake.

- iii) Kamati inapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu (Muungano) kwa kuandaa na kuzindua rasmi kitabu kinachohusu historia ya Muungano. Kitabu hiki ni nyenzo muhimu katika kuweka kumbukumbu sahihi ya misingi na historia ya Muungano wetu. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba kitabu hicho kinasambazwa kote nchini, na pia kinawekwa katika nakala tete (*softcopy*) ili kurahisisha upatikanaji wake katika mtandao wa inteneti, ikijumuisha mitandao ya kijamii.
- iv) Pamoja na kwamba Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maoni na ushauri ambao iliutoa, Kamati inaendelea kuvisitiza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira katika taasisi za Muungano, Kamati inaendelea kuishauri Serikali izingatie pia uwiano wa kijinsi katika nafasi mbalimbali za ajira katika taasisi hizo.
- v) Katika uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti, Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto za utofauti wa kikodi katika bidhaa zinazoingizwa Tanzania Bara kutokea Tanzania Zanzibar. Kamati inashauri, Serikali na taasisi zake zote zinazohusika na jambo hili kuongeza juhudii za kutafuta suluhisho la kudumu la changamoto hizo. Aidha, juhudii hizo ziende sambamba na utoaji wa elimu kwa Wananchi wa pande zote za Muungano ili kupunguza malalamiko ambayo yanaweza kujitokeza.
- vi) Kamati inapongeza Serikali kuzifanyia kazi na kupunguza changamoto za Muungano zilizokuwepo. Hata hivyo, Kamati

inasisitiza na kuishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi ili kuzimaliza na kuzindoa changamoto zilizobaki.

vii) Kamati imebaini kwamba, majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais yanayofanyiwa ukarabati katika eneo la Tunguu Zanzibar, sasa yatatumiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hadi kufikia Februari, 2022 fedha zilizotengwa kufanya ukarabati huo zilifika kwa **asilimia 56** tu. Kamati inashauri Serikali itoe fedha kamili kutekeleza mradi huo kwani unategemea fedha za ndani kwa asilimia mia moja. Vivile Kamati inashauri Serikali iharakishe kujenga Ofisi mpya Zanzibar itakayotumiwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
7. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
8. Mhe. Zainabu Athumanji Katimba, Mb.
9. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb.
10. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb.
12. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb.

13. Mhe. Omar Ali Omar, Mb.
14. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
18. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb.
19. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.
20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
22. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
23. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Mhe. Kamis Hamza Khamis (Mb.), Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (MUungano na Mazingira) kwa ushirikiano wao ambao umesaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nawashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Mary N. Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) akisaidiwa na Ndg. Abdallah H. Mitawi, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndgg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati za Bunge na Shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndgg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndgg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii Ndgg. Yona Kirumbi na Ndgg. Elihaika Mtui wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria
27 Aprili, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa maoni hayo ya Kamati ambayo yatawaongoza Waheshimiwa Wabunge kutoa michango yao kwenye eneo hilo.

Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile aje awasilishe maoni ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. (*Makofi*)

MHE. DAVID M. KIHENZILE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira Fungu Na. 31 Idara ya Mazingira kwa Mwaka, 2021/2022 pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka, 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uzima na kutuwezesha kufika tena siku hii ya leo. Nianze kwa kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge, Familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama (Mb), kilichotokea tarehe 24 Aprili, 2022. Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati yetu na mchango wake kwa Kamati ulikuwa na umuhimu mkubwa. Tunaendelea kumkumbuka kwa ucheshi wake, ukarimu na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

utu wema, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati tunamuombea apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Fungu 31 Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili katika Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya taarifa hii yanagawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo: -

1. Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo,
2. Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022,
3. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya usimamizi wa uhifadhi wa mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 na,
4. Maoni na Ushauri wa Kamati unaotokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa majukumu ya usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 na 2022/2023; kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 ilitokana na masharti ya Kanuni ya 117(1) Kanuni za Kudumu za Bunge inayotaka siku zisizozidi saba zitumike kwa ajili ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Kamati ilizingatia masharti hayo na kupanga kutembelea na kukagua miradi miwili ya usimamizi wa mazingira katika Mkoa

wa Dodoma na Kaskazini 'A' Unguja Zanzibar. Taarifa ya kina kuhusiana na ziara ya ukaguzi wa maendeleo na maoni ya jumla ni kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa tatu hadi ukurasa wa tisa wa taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 Kamati ilifanya ulinganisho wa kiasi cha fedha zilizopokelewa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ambapo matokeo ya uchambuzi inaonesha kama ifuatavyo:-

i. Fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za kusimamia na kudhibiti mazingira kwa ujumla ilipatikana kwa mtiririko unaoridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 fedha iliyoopatikana ilikuwa ni asilimia 131 ya bajeti upatikanaji wa fedha katika kipindi hiki unastahili kuwa ni asilimia 66 ya utekelezaji. Aidha, pamoja na kupokea fedha kwa asilimia 131 katika kipindi hicho miradi mingi ilikuwa hajatekelezwa kikamilifu (*Makof*)

ii. Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira ulifikia asilimia 3.17 ya fedha iliyoopokelewa kwa ajili hiyo. Kiwango cha fedha hizo ni za nje bila kujumuisha fedha za ndani kiasi cha shilingi milioni 400 ambazo hazikupatikana hata kidogo. Hali hiyo inaonesha kuwa kudhibiti na kusimamia mazingira ni Jambo linalotegemea fedha za nje kutoka kwa wadau wa maendeleo. Utegemezi huo unaweza kutafsiriwa kama hakuna dhamira ya dhati ya kudhibiti mazingira kwa maendeleo endelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa Kamati ni kwamba udhibiti na usimamizi wa mazingira unahitaji msukumo mkubwa wa ndani ya nchi kabla ya msukumo wa wahisani wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023; uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi. Kamati

ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha, 2022/2023 jumla ya shilingi billioni 26,732,352,530 zinaombwa chini ya kifungu 31 Idara ya Mazingira kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Mchanganuo wa fedha unaonekana katika kielelezo namba mbili. Takwimu hizi zinaashiria kwamba:-

(a) Kiasi cha makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 kuna ongezeko la asilimia 173 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Tafsiri ya ongezeko hilo ni kwamba utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira unaendelea kuimarika kwa kiwango fulani ikilinganishwa na mpango wa mwaka unaoisha.

(b) Ongezeko la bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 unaleta picha chanya kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo imeongezeka kwa asilimia 614 ikilinganishwa na bajeti ya miradi ya maendeleo ya Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 544 hivyo kusababisha jumla ya bajeti kuu kuongezeka.

(c) Fedha za ndani zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni kidogo ikilinganishwa na uhalisia wa mazingira nchini. Pamoja na ongezeko la asilimia 66 fedha hizi zimekuwa hazitolewi hivyo kupunguza ufanisi na tija iliyokusudiwa. Mfano, kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 fedha za ndani kiasi cha Shilingi milioni 400 hazikutolewa hadi sasa. Kamati inaona kuwa hali hii inaashiria kuwa ajenda ya kusukuma maendeleo ni ya nchi za nje.

(d) Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 17 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo linatokana na ajira na watumishi kupanda vyeo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa Kamati imefanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti kuu ya Serikali na kubaini kuwa bajeti ya Wizara ya Mazingira imeongezeka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutoka asilimia 0.026 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 0.65 mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na. 3.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za miradi ya maendeleo za ndani na nje. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu la 31 Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022 pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa Serikali: -

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati haikuwa ya kuridhisha. Kiasi cha fedha kilichotumika ni kikubwa kuliko ukubwa na tija ya miradi husika. Kamati inaishauri Serikali kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha hizi za miradi. Aidha, matumizi ya fedha zinazotolewa ziendane na kazi na thamani ya fedha (*value for money*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kemikali ya zebaki. Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya mpango kazi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini.

Aidha, waendelee kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na mafunzo kwa maafisa mazingira katika ngazi zote, Maafisa forodha, wakaguzi kutoka katika mamlaka za udhibiti kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji, matumizi na utupaji wa taka zinazotokana na zebaki, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kuzindua sera yake iliyofanyika Februari, 2022. Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

(a) Kumaliza haraka mchakato wa kutafsiri sera hii kwa lugha ya Kiswahili kama ambavyo Mheshimiwa Makamu wa Rais alivyoelekeza katika uzinduzi wa sera hii, ili sasa wananchi wawzeze kuelewa zaidi na kuanza utekelezaji wake.

(b) Serikali kuisimamia na kuitetea Sera ya Taifa ya Mazingira ikizingatiwa kuwa mazingia ni ajenda kuu ya Dunia na ndio mustakabali wa maisha ya viumbe hai kwenye uso wa Dunia.

(c) Kwa kuwa tayari tuna Sera Kamati inasisitiza uharakishwaji wa mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 na Sura ya 175(1).

Sehemu ya Nne, Hitimisho. Shukrani. Naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa; tunakuombea afya njema katika kutekeleza majukumu yako. Vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge letu Tukufu.

Kipekee nimshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Eric James Shigongo Mbunge pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wanaonipa wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna wanavyojituma kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kutoa maoni, ushauri, mapendekezo, michango na mawazo yao mbalimbali wakati wa kutembelea, kukagua na kupitia, kujadili na kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Naomba orodha ya majina yote yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo Mbunge na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Khamis Khamis Mbunge, Katibu Mkuu Mary Ngelela Maganga, Naibu Katibu Mkuu Edwin Kijazi Nyamahanga. Pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao Kamati imekuwa ikipata kutoka kwao kwa wakati wote wa vikao na uchambuzi wa bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi Idara ya Kamati Ndugu Athuman, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Dickson Bisile, Msaidizi wa Kamati Modesta Kipiko na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kipekee tunawashukuru Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Felister Frank Mgonja na Ndugu Nyamwanja Chipala Chilemeji kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa hii inawasilishwa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja; baada ya kusema haya naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31 Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA
MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU
31 – IDARA YA MAZINGIRA KWA MWAKA 2021/2022 PAMOJA
NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA MWAKA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uzima na kutuwezesha kukutana siku hii ya leo. Nianze kwa kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge, Familia ,Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mhe. Irene Alex Ndyamkama (Mb) kilichotokea tarehe 24 Aprili 2022. Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati yetu na mchango wake kwa Kamati ulikuwa na umuhimu sana. Tutaendelea, kumkumbuka kwa ucheshi wake, ukarimu na utu wema. Kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati tunamuombea apumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka **2021/2022** pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili katika uhifadhi na usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023**.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Taarifa hii yanagawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo:-

a) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

- b) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya usimamizi na uhifadhi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- d) Maoni na ushauri wa Kamati unaotokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa majukumu ya usimimamizi na uhifadhi wa mazingira.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 31 katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 yanatokana na uchambuzi wa maeneo matatu yafuatayo:

2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulitokana na masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayotaka siku zisizozidi saba zitumike kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilizingatia masharti hayo na kupanga kutembelea na kukagua miradi miwili ya usimamizi wa mazingira, katika mikoa ya Dodoma na Kaskazini A Unguja (Zanzibar).

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge kuhusu yaliyobainika katika uchambuzi pamoja na maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusu usimamizi na udhibiti wa Mazingira.

2.1.1 Yaliyobainika katika Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, iliidhinishiwa kiasi

cha shilingi **2,970,788,000.00**. Kati ya Fedha hizo shilingi **2,570,788,000.00** ni Fedha za nje na shilingi **400,000,000.00** ikiwa ni Fedha za ndani.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ilipokea kiasi cha shilingi **8,169,273,053.27** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira chini ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Spika, Miradi miwili iliyotembelewa na Kamati kwa Mwaka huu wa Fedha 2021/2022 ni:-

i) **Mradi wa kurejesha ardhi iliyoaribika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame** (*Reversing land degradation trends and increasing food security in degraded ecosystem in semi arid areas of Tanzania – LDFS*) Mradi na. 31. Kifungu 5001.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa katika kijiji cha Haubi na Mafai wilaya ya Kondoa, Mkoani Dodoma. Lengo la mradi huu ni kuboresha usimamizi endelevu wa ardhi na kuwezesha urejeshwaji wa mfumo wa ikolojia ulioaribika unaochangia kutoa huduma muhimu za uzalishaji kwenye maeneo ya ardhi, maji, misitu na bionuai kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi huu kwa Wilaya ya Kondoa ni Jumla ya **shilingi 1,053,400,000**. Hadi wakati Kamati yako inatembelea mradi huu Fedha zilizokua zimepokelewa kwa matumizi ya mradi ni Shilingi **414,449,355** sawa na asilimia **39.3** tu ya Fedha zilizotengwa. Aidha, kwa kipindi kilichobaki cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati ilielezwa kuwa wapo kwenye mchakato wa kuhamisha kiasi cha Shilingi **284,074,428** na kufanya Fedha zitakazotolewa kufikia kiasi cha Shilingi **689,523,783** sawa na asilimia **72** ya Fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa kabisa na namna mradi huu unavyotekeliza, kwakuwa hautoi taswira ya

kilichokusudiwa ikiwa ni pamoa na dhana ya kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame ya Tanzania. Kamati ilibaini yafuatayo;

- a) Walengwa wa mradi hawakua na uelewa wa umuhimu wa mradi wala hawatambui manufaa ya Mradi;
- b) Wananchi/walengwa hawajui wala hawana uelewa juu ya Bajeti ya Mradi iliyotengwa;
- c) Watu wengi hawajafikiwa na elimu juu ya dhana nzima ya mashamba darasa;
- d) Watekelezaji wa mradi wanakaa na Fedha muda mrefu jambo ambalo linakwamisha mradi kutotekelezwa kwa wakati (ofisi ya OMRMM na Halmashauri);
- e) Wananchi walengwa hawanufaiki na Bajeti katika kunyanya kipato chao, ilionekana kama vile hela wanakaa nazo watendaji halafu wakulima wanatumika bila kujuu kama wanapaswa kulipwa chochote;
- f) Lengo mahsusni kurejesha Ardhi iliyoharibika lakini hakuna utaratibu wa kuwa na miti ya mfano iliyopandwa.

Mheshimiwa Spika, Kupitia mtazamo huo, Kamati inaona ipo haja ya Wizara, kufanya tathmini upya juu ya utekelezaji wa mradi huu na kushirikisha wananchi juu ya manufaa ya mradi. Aidha, malengo ya mradi yaendane na kasi ya utekelezaji wake, kwani ipo hofu kuwa malengo hayaendani na kinachotekelzeza katika eneo la mradi huu.

ii) Mradi wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini (Ecosystem – Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania - EBARR) Kaskazini 'A' - Unguja (Zanzibar) mradi na. 31, kifungu 5001

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 mradi ulitengewa Jumla ya shilingi **1,100,112,000** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi upande wa Kaskazini A -

Unguja. Hadi sasa, jumla ya Dola za Marekani **278,937.29** sawa na shilingi **644,066,202.61** sawa na asilimia **58.5** ya kiasi kilichotengwa, zimepokelewa na Idara ya Mazingira – Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - SMZ kwa ajili ya utekelezaji wa Shughuli za Mradi. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi, kiasi kilichokuwa kimetumika ni shilingi **122,091,238** sawa na asilimia **19** ya kiasi kilichopokelewa. Bakaa kwenye akaunti ni shilingi **521,974,964.61**.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unalenga kunufaisha vikundi nya uvuvi, kilimo, ufugaji kuku, ufugaji nyuki, ufumaji na ushoni na utengenazaji wa sabuni. Vikundi hivi vinajumuisha wanawake, wanaume na vijana. Vikundi hivi vimeundwa kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa kuititia mikutano ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea eneo la kijinimbuyutende ili kuona majiko banifu ya mfano ambayo wananchi waliwekewa majumbani kwa lengo la kunyanyua maisha yao na kukuza shughuli zao za kiuchumi. Hatahivyo, Kamati haikuona **tija** ya mradi wala **thamani ya Fedha kwa aina ya majiko yaliyotengenezwa** ambapo majiko hayo yanakadiriwa kutumia zaidi ya shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikagua boti sita (6) zenye thamani ya shilingi **247,000,000** katika eneo la Fumba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa boti zinazotengenezwa kwa ajili ya shughuli za uvuvi, Kamati imekuwa **na wasiwasi kuwa boti hizo zimetumia gharama kubwa ikilinganishwa na muonekano katika utengenezaji wake**. Thamani ya boti moja inagharimu zaidi ya shilingi **40,000,000** kiasi ambacho Kamati imetilia mashaka ukilinganisha na ubora na hadhi ya Maboti yenyeewe.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, utekelezaji wa Mradi kwa upande wa Kaskazini A – Unguja hauakisi kabisa malengo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuongeza umakini katika usimamizi wa miradi hii ili iweze kuwa na tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, wananchi washirikishwe kikamilifu ili wajue kwa undani miradi hii kwa kufanya hivyo wataweza kuilinda na kuitunza na kuifanya kuwa endelevu.

2.1.2 Maoni ya Jumla katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo yamebainisha mambo yafuatayo:-

- a) Kasi ya matumizi ya Fedha za Miradi yote iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati iko chini ikilinganishwa na muda wa utekelezaji wa miradi. **Hivyo Kamati inaishauri Serikali itafute ufumbuzi wa, kwanini Fedha zinachelewa kutumika na kufanya miradi kushindwa kutekelezwa kwa wakati uliokusudiwa;**
- b) Miradi hii imekuwa ikitengewa Fedha za ndani na Fedha za nje, Kamati inasikitika kuwa Fedha ambazo zimekuwa zikitolewa ni za nje tu na hakuna Fedha za ndani, **Kamati inasisitiza Fedha za ndani kutolewa kwa wakati ili utekelezaji wa miradi uwe kwa wakati na endelevu;**
- c) Mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya mazingira yanategemea kwa kiasi kikubwa uelewa wa wananchi ambao wanapaswa kutoa ushirikiano kutokana na kuwa wanufaika wakuu. **Hivyo Kamati inasisitiza elimu iendelee kutolewa kwa wananchi ili waone umuhimu wa kuitunza na kuiendeleza miradi hii.**

2.2 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendelekezo ya Kamati kwa Mwaka 2021/2022

Mheshimwa Spika, Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati ingawa yapo baadhi ya maoni hayajatekelezwa kikamilifu kama vile udhibiti wa matumizi ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo ambao bado una athari kubwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sana kwa Mazingira. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuchukua hatua madhubuti katika uingizaji wa kemikali hizi na kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki.

Vilevile Kamati inaendelea kushauri Serikali kumaliza kufanya mapitio ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 (sura 191).

2.3 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, Kamati ilijielekeza katika maeneo makubwa mawili ambayo ni upatikanaji wa Fedha na hali halisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.


Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Bunge liliidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira, **Fungu 31** kiasi cha Fedha kwa mchanganuo kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 01**

Kielelezo Na. 01

Kielelezo Na. 1 UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 31 MWAKA 2021/2022

MCHANGANUO WA UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 31 MWAKA 2021/2022				
MATUMIZI		KILICHODHINISHWA	KILICHOPKELEWA	ASILIMA
KAWANDA	MSIHARA	798,444,000.00	472,284,999.84	59.15
	OC	2,270,217,140.00	1,494,332,879.89	65.82
	NEMC	3,751,798,000.00	2,732,390,988.00	
	JUMIA	6,820,459,140.00	4,699,008,867.73	69
MAENDELEO	NDANI	400,000,000.00	0.00	0.00
	NJE	2,570,788,000.00	8,169,273,053.27	317.77
	JUMIA NDOGO	2,970,788,000.00	8,169,273,053.27	275
JUMLA BAJETI		9,791,247,140.00	12,868,281.921.00	131

Chanzo: Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira



Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa kiasi cha Fedha zilizopokelewa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ambapo matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa :-

a) Pesa iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za kusimamia na kudhibiti mazingira kwa ujumla ilipatikana kwa mtiririko unaoridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 pesa iliyopatikana ilikuwa ni asilimia **131** ya bajeti. Upatikanaji wa Fedha katika kipindi hiki unastahili kuwa ni asilimia **66.6** ya utekelezaji,

Aidha, pamoja na kupokea Fedha kwa asilimia 131 katika kipindi hicho miradi mingi ilikuwa hajatekelezwa kikamilifu.

b) Upatikanaji wa Fedha kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira ulifikia asilimia **317** ya Fedha iliyopokelewa kwa ajili hiyo. Kiwango cha Fedha hizo ni za nje bila kujumuisha Fedha za ndani kiasi cha shilingi **400,000,000** ambazo hazikupatikana hata kidogo.

Hali hiyo inaonesha kuwa kudhibiti na kusimamia mazingira ni jambo linalotegemea Fedha za nje kutoka kwa wadau wa maendeleo. Utegemezi huo unaweza kutafsiriwa kama hakuna dhamira ya dhati ya kudhibiti mazingira kwa maendeleo endelevu. **Mtazamo wa kamati ni kwamba, udhibiti na usimamizi wa mazingira unahitaji msukumo**

mkubwa wa ndani ya nchi kabla ya msukumo wa wahisani wa maendeleo.

2.4 Utekelezaji wa Kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia majukumu ya Kamati hii, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022** ulifanyika. Jumla ya kazi kumi na tano (15) zilipangwa kutekelezwa na Idara ya Mazingira na Baraza (NEMC). Napenda kuliarifu Bunge hili kuwa kazi zote zilizopangwa zimeripotiwa kutekelezwa. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha yafuatayo:-

- a) Bado wananchi wanaendelea kutupa taka ngumu bila mpangilio, hivyo elimu inahitajika zaidi katika kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mwongozo wa usimamizi na udhibiti wa Mazingira hususan maeneo ya mijini;
- b) Bado hakuna Elimu ya kutosha kwa wenyewe viwanda kuhusu kuweka mifumo ya kutibu majitaka kabla ya kuyatiririsha katika mazingira.

2.5 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

2.5.1 Uchambuzi wa Malengo/Mpango

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa malengo pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023**, vinaendana na majukumu ya msingi, ikiwemo kuzingatia Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na llani ya Uchaguzi. Kwa mfano, jukumu la kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kampeni za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya Tabia nchi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na upandaji miti, linaendana na majukumu ya msingi ya idara ya mazingira. Aidha, jukumu hilo linaendana na llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 235 (a), ukurasa wa 285 wa llani.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilijiridhisha kwa kuangalia Malengo ya mpango wa maendeleo Endelevu ya Dunia (*Sustainable Development Goals*) ambapo ajenda ya **Mazingira ni ya 13 kati ya Malengo 17 ya SDG's (2030)**. Katika lengo namba 13 linalosomeka kama **Climate Action** ambayo ndani yake ina malengo matano yafuatayo;

- a) Kuimarisha ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na hatari zinazohusiana na hali ya hewa na majanga ya asili katika nchi zote;
- b) Kujumuisha hatua za mabadiliko ya tabianchi katika sera, mikakati na mipango ya kitaifa;
- c) Kuboresha elimu, uhamasishaji na uwezo wa kibinadamu na kitaasisi juu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kukabiliana na hali, kupunguza athari na kuchukua tahadhari mapema;
- d) Kutekeleza dhamira inayotolewa na nchi zilizoendelea kwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Kwa lengo la kukusanya kwa pamoja dola bilioni 100 kila Mwaka ifikapo 2020 kutoka kwa vyanzo vyote, ili kushughulikia mahitaji ya nchi zinazoendelea katika muktadha wa hatua za kupunguza na uwazi juu ya utekelezaji na kutekeleza kikamilifu Mfuko wa Hali ya Hewa ya Kijani kuititia mtaji wake haraka iwezekanavyo;
- e) Kukuza taratibu za kuinua uwezo wa upangaji na usimamizi bora, unaohusiana na mabadiliko ya tabianchi katika nchi zilizoendelea kidogo na nchi za visiwa vidogo vinavyoendelea, ikiwa ni pamoja na kuzingatia wanawake, vijana na jumuiya za mitaa na zilizotengwa.

Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kuititia Idara ya Mazingira kwa kuzingatia kikamilifu mpango wa maendeleo endelevu ya Dunia *SDG's (2030)*. Hata hivyo, bado yapo maeneo machache yanayohitaji kufanyiwa kazi. Mionganoni mwake ikiwemo kuendelea kutoa elimu, uhamasishaji na uwezo wa kibinadamu na kitaasisi juu ya

kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ili kuweza kupunguza athari kwa kuchukua tahadhari za uthibiti wa mazingira mapema.

2.5.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi


Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya **shilingi 26,732,352,530.00** zinaombwa chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Mchanganuo wa Fedha hizo unaonekana katika **Kielelezo Na 02**.

Kielelezo Na.02

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 31 KWA MWAKA 2021/2022

MCHANGANUJWA ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 31 KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023					
FEDHA	MATUMIZI	2021/2022	2022/2023	ONGEZIKO/ UPUNGURU	%
KAWIDA	MSIHARA	798,444,000.00	936,225,000.00	137,781,000.00	17
	OC	2,270,217,140.00	2,291,802,800.00	21,585,660.00	1
	NEMC	3,751,798,000.00	4,362,627,730.00	610,829,730.00	16
	JUMLA NDOGO	6,820,459,140.00	7,590,655,530.00	770,196,390.00	34
MAENDELEO	NDANI	400,000,000.00	782,000,000.00	382,000,000.00	96
	NJE	2,570,788,000.00	18,359,597,000.00	15,788,909,000.00	614
	JUMLA NDOGO	2,970,788,000.00	19,141,697,000.00	16,170,909,000.00	544
JUMLA BAJETI	JUMLA KUU	9,791,247,140.00	26,732,352,530.00	16,941,105,390.00	173

Chanzo: Randama ya Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira



Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaashiria kwamba:

- a) Kiasi cha makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kuna ongezeko kwa asilimia **173** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Tafsiri ya ongezeko hilo, ni kwamba utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira unaendelea kuimarika kwa kiwango fulani ikilinganishwa na mpango wa Mwaka unaoisha.
- b) Ongezeko la Bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 unaleta picha chanya kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambayo imeongezeka kwa asilimia **614** ikilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zimeongezeka kwa kiasi cha **Asilimia 544** hivyo kusababisha Jumla ya Bajeti kuu kuongezeka.
- c) Fedha za NDANI zinazoombwaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni kidogo ukilinganishwa na uhalisia wa hali ya mazingira nchini. Pamoja na ongezeko la **asilimia 96**, Fedha hizi zimekuwa hazitolewi hivyo kupunguza ufanisi na tija iliyokusudiwa. Mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 Fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 400,000,000** hazikutolewa hadi sasa. Kamati inaona kuwa **hali hii inaashiria wazi kuwa Ajenda ya kusukuma maendeleo ni ya Nchi za NJE**.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

d) Bajeti ya Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka unaoishia. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo ilimetokana na ajira na watumishi kupanda vyeo.

2.6 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali na kubaini kuwa Bajeti ya Wizara ya Mazingira imeongezeka kutoka **asilimia 0.026** Mwaka 2021/2022 hadi **kufikia 0.065** Mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko zaidi linaonekana katika Fedha za miradi ya maendeleo za ndani na nje. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.**

Kielelezo Na. 3

ULINGANISHO WA BAJETI YA OMRMM (MAZINGIRA) DHIDI YA BAJETI YA TAIFA

ULINGANISHO WA BAJETI YA MAZINGIRA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022			
AINA	BAJETI TAIFA	BAJETI MAZINGIRA	ASILIMIA
O C	4,189,190,000,000.00	2,270,217,140.00	0.054
M ISHABARA	8,155,090,000,000.00	798,444,000.00	0.010
M AEND ELEO N DANI	10,722,989,000,000	400,000,000.00	0.004
M AEND ELEO N JE	4,254,626,000,000	2,570,788,000.00	0.060
DENILA SERIKALI	10,663,278,000,000.00	-	-
NEMC		3,751,798,000.00	
JUM LA	37,985,173,000,000.00	9,791,247,140.00	0.026

ULINGANISHO WA BAJETI YA MAZINGIRA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023			
AINA	BAJETI TAIFA	BAJETI MAZINGIRA	ASILIMIA
O C	4,493,500,000,000.00	2,291,802,800.00	0.051
M ISHABARA	9,740,800,000,000.00	936,225,000.00	0.010
M AEND ELEO N DANI	12,122,100,000,000	782,000,000	0.006
M AEND ELEO N JE	3,399,200,000,000	18,359,697,000	0.540
DENILA SERIKALI	11,308,400,000,000.00	-	-
NEMC	-	4,362,627,730.00	
JUM LA	41,064,000,000,000.00	26,732,352,530.00	0.065

Chanzo: Mapendekozo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na Randama ya Wizara ya Mazingira 2022/2023

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Fungu 31- Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa Serikali:-

3.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati haikua ya kuridhisha. Kiasi cha Fedha kilichotumika ni kikubwa kuliko ukubwa na tija ya miradi husika, Kamati inaishauri Serikali kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya Fedha hizi za miradi. Aidha, matumizi ya Fedha zinazotolewa basi ziendane na kazi na thamani ya Fedha ‘*value for money*’.

3.2 Matumizi ya kemikali ya Zebaki

Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya Mpango kazi wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini. Aidha waendelee kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na mafunzo kwa maafisa Mazingira katika ngazi zote, maafisa forodha, wakaguzi kutoka katika mamlaka za udhibiti kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji, matumizi na utupaji wa taka zitokanazo na zebaki, ikiwa ni pamoja na kuhamasiha matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki.

3.3 Sera ya Taifa ya Mazingira 2021

Mheshimiwa Spika, Kamati **inatoa pongezi** kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa kuzindua Sera yake uliofanyika Februari 2022,

Mheshimiwa Spika, Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri yafuatayo;

- a) Kumaliza haraka mchakato wa kutafsiri Sera hii kwa Lugha ya Kiswahili kama ambavyo Mhe. Makamu wa Rais alivyoelekeza katika Uzinduzi wa Sera hii ili sasa wananchi wawze kuelewa zaidi na kuanza utekelezaji wake;
- b) Serikali kuisimamia na kuitekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ipasavyo ikizingatiwa kuwa mazingira ni agenda kuu ya dunia na ndio mstakabali wa maisha ya viumbe hai kwenye uso wa dunia.
- c) Kwa kuwa tayari tuna sera, Kamati inasisitiza uharakishwaji wa mapitio ya sheria ya usimamizi wa Mazingira sura 191 na sura 175(1).

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Tunakuombea afya njema katika kutekeleza majukumu yako. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Nailbu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Makamu Mwenyekiti Mhe. Eric James Shigongo Mb, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wanaonipa wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa namna wanavyojituma kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja kutoa maoni, ushauri, mapendekezo, michango na mawazo yao mbalimbali wakati wa kutembelea, kukagua, kupitia, kujadili na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo hapa chini: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Eric James Shigongo, Mb – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb
4. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
6. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
7. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
8. Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb
9. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb
10. Mhe. Haji Makame Mlenga, Mb
11. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb
12. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb
13. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb
14. Mhe. Maryam Omar Said, Mb
15. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb
16. Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb
17. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
18. Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb
19. Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb
20. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
21. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
22. Mhe. Dkt. Alfred James Kimea, Mb
23. Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb
24. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb
25. Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira Mhe. Selemani Jafo, Mb. na Naibu Waziri wake Mhe. Khamis H. Khamis Mb, Katibu Mkuu Ndg. Mary Ngelela Maganga, Naibu Katibu Ndg. Edwin Gerald Nyamanga pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao Kamati imekuwa ikiupata kutoka kwao kwa wakati wote wa vikao na uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndg. Athuman Hussein *ndc*, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson Bisile, Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Kipekee tunawashukuru Makatibu wetu wa Kamati Ndg. Felister Frank Mgonja na Ndg. Nyamwanja Chipanda Chilemeji kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa hii inawasilishwa kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka wa Fedha **2022/2023** kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile, Mb
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA
27 Aprili, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea niwatangaze wageni tulionao hapa Bungeni, ili wale ambao watakuwa wanataka kutoka waweze kuendelea na ratiba nyingine.

Kwanza ni wageni walioko jukwaa langu pale, jukwaa la Spika. Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Watendaji Wakuu wakiambatana na Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Ofisi hiyo.

Kwanza yupo Mary Ngelela Maganga ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. Yupo pia Ndugu Edward Nyamanga ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Mazingira, karibu sana. Yupo pia Ndugu Abdallah Mitawi ambaye ni Naibu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Katibu Mkuu Muungano, karibu sana. Yupo pia Ndugu Edwin Makamba ambaye ni Katibu wa Makamu wa Rais, karibu sana. Yupo pia Mhandisi Dkt. Samuel Mafwenga ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *NEMC*, karibu sana. Yupo pia Profesa Asnati Chagu Mwenyekiti wa Bodi ya *NEMC*, karibu sana. Yupo pia Dkt. Emma Liwenga ambaye ni Msaidizi wa Makamu wa Rais Mazingira, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Selemani Jafo ni familia yake ambayo ni mke wake Ndugu Asha Shame Vuai na mtoto wake Ndugu Ismail Selemani Jafo; wameongozana na watoto wa kaka yake Rashid Ally na Abubakar Jafo, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Selemani Jafo ni familia yake amba ni Mke wake Ndugu Asha Shame Vuai na Mtoto wake Ndugu Ismail Selemani Jafo, wameongozana na watoto wa Kaka yake amba ni Ndugu Rashid Ali na Ndugu Aboubakar Jafo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nami ninao wageni 25 kutoka Wasafi Media amba ni Meneja Mawasiliiano, Watangazaji na Wasanii wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wasafi Media, Ndugu Nasib Abdul, maarufu kama *Diamond Platinum*. Mheshimiwa Diamond unasimama mpaka makofi yaishe. Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa naendelea na kutangaza na kikosi chote alichokujanacho pale. Ndugu Nasib Abdul ama *Diamond Platinum*'s sameongozana na Ndugu Nelson Kisanga ambaye ni Meneja Mawasiliiano Wasafi Media. Karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Ndugu Spencer Lameck ambaye ni Meneja Rasilimali Watu Wasafi Media. Neema Lugalata - Meneja Rasilimali Watu, Wasafi Media. Yupo pia Makame Fumbwe - Mkuu wa Kitengo cha Fedha, Wasafi Media. Yupo Baba Levo - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Yupo pia Dida Shaibu - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Yupo pia Juma Lokole - Mtangazaji kutoka pia Wasafi FM. Yupo Zembwela - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Yupo Aurest Kawau - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Ndugu Lil Ommy kutoka Wasagi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

FM. Yupo Ndugu Charles William kutoka Wasafi FM. Yupo Edo Kumwembe - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Mwanaidi Suleiman - Mtangazaji kutoka Wasafi FM. Sekioni David - Wasafi FM. Motown Sanya - Wasafi FM. Rikado Mtomo - Wasafi FM. Mkubwa Fela - Meneja wa Wasafi Classic Baby (*WCB*). (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mboso, Msanii kutoka *WCB*. Yupo pia Zuchu - Msanii kutoka *WCB*. Yupo pia Lavalava kutoka *WCB*. Yupo pia Queen Darling kutoka *WCB*. Yupo pia Mama Dangote, Mama yake Diamond Platinum's. Haya ahsanteni sana. Yupo pia Uncle Shamte. Yupo pia, Esma Platinums - Dada yake na Diamond Platinums, ahsante sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hao ndio ambaao wameongozana hapo na Mkurugenzi Mkuu wa Wasafi Media. Wakati niko hapo bado, kikosi hiki kutoka *WCB* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wao ndiyo ambaao leo watatupa *Iftar*, kama mlivyokuwa mmetangaziwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe pamoja na haya niliyoyasema hapa, wageni wetu hawa wametupa heshima kubwa na sisi basi tujitokeze kwa wingi kwenye *Iftar* hiyo ambayo itafanyika mara baada ya shughuli za Bunge.

Tunakushukuru sana Diamond Platinum, Nassib Abdul, kwa sadaka hii ambayo umekuja kuitoa kwa Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Pia tunatambua mchango wako mkubwa katika sanaa nchi hii, hasa sanaa ya muziki na ajira ulizozitoa hapo. Nilikuwa nasoma orodha ya watu ambaao umewaaajiri wewe, umefanya kazi nzuri, tunakupongeza sana na tunakutakia kila la heri katika mipango yako uliyonayo ya huko mbele kuendeleza sanaa, lakini pia kuendelea kuajiri vijana wa nchi hii. Ahsante sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, katika wageni wa Mheshimiwa Jafo, yupo Katibu wa Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Jafo ni Waziri, lakini kama Mbunge anae Katibu wake, kwa hiyo, Katibu kutoka Jimboni kwake pia yuko hapa anaitwa Ndugu Discipline Mawoza. Karibu sana. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tutaanza na Mheshimiwa Michael Constantine Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

Wabunge wote mtakuwa mkichangia kwa dakika tano.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi na kuwa wa kwanza kwenye kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Ofisi ambayo Ndugu yangu Mzee wa Mzenga anaiwakilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze ye ye na viongozi wote ambao wako Wizarani kwake kwa namna ambavyo wanatekeleza majukumu ya Serikali. Kwa kuwa, muda ni mchache sana naomba akubaliane nami kwamba, nilichokitamka kama pongezi kinatoka ndani ya nafsi ya moyo wangu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo nimeomba nichangie kwenye eneo hili kwa sababu ya kutaka kuzungumza suala moja ambalo nililielewa wakati Mheshimiwa Rais anafanya uapishaji wa Baraza la Mawaziri, alipowaambia Mawaziri na Taasisi za Serikali kwa lengo la ku wahudumia Watanzania ni vizuri wakawa na mawasiliano ili kumaliza kero na changamoto ambazo Watanzania zinawakabili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa jinsi nilivyomuelewa Mheshimiwa Rais na nia yake ilivyo njema ya kutaka vyombo vya Serikali viisaidie nchi hii na hasa kwenye kuondoa changamoto ambazo Watanzania wanazo, nimeona nianzie hapo kwenye kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii

ambayo ndugu yangu Mzee wa Mzenga, Jirani yangu pale wa Jimbo yupo.

Mheshimiwa Spika, nimeamua nichangie hapa kwa kumkumbusha yeye na vingozi wengine...

SPIKA: Mheshimiwa Mwakamo, huyo Mzee wa Mizenga ndiyo nani?

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, ni Mheshimiwa Waziri Jafo. Naomba... (*Kicheko*)

SPIKA: Basi tunamtambua namna hiyo humu ndani. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Sasa Mheshimiwa Waziri lipo jambo ambalo linaendelea ambalo Mkurugenzi wa *NEMC* na ninashukuru ametambulishwa yupo, pale Jimboni Kibaha vyombo hivi vimeshindwa kuwasiliana vizuri. TAMISEMI walitenga pesa kwa ajili ya kupeleka pale kuendesha mradi mkubwa wa ujenzi wa shule ya sekondari, pia TAMISEMI walitoa maagizo mbalimbali maeneo ya pale yalipimwa kwa utaratibu wa kisheria, lakini kwa masikito makubwa Wizara au Ofisi ya *NEMC* imetoa zuo kwa maana eneo lile lisiendelee na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kitu kinachosikitisha wananchi wamepata tataruki kubwa na tataruki hii imesababishwa na wao, kwa sababu hilo eneo lilishapimwa, limepimwa kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi, limepangiwaa matumizi mbalimbali, bahati nzuri au mbaya Serikali wameuza viwanja kwenye maeneo hayo na wananchi wamenunua viwanja hivyo kwa shughuli mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vipo viwanda vimeshaanza kujengwa na vibali wanatoa haohao *NEMC*, lakini kinachosikitisha mwezi uliopita huu wametoa zuo la kutokuendelea na ujenzi wa shule ya sekondari, jambo ambalo limewashtua watu wengi, jambo ambalo limesababisha changamoto kubwa, mpaka hivi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ninavyozungumza wale walionunua viwanja kwenye eneo lile wanani pigia simu wakiwa wanataka kuweka utaratibu wa kwenda kuishtaki Halmashauri kwa sababu ndio ambao wamewauzia viwanja ambavyo vimezuiwa na *NEMC*.

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba awe makini na hawa *NEMC* kwa sababu, ni wao ambao wametoa vibali vyatya ujenzi, lakini hao hao tena waliota idhini ya eneo lile kupimwa, hao hao wenyewe ndiyo wanatoa idhini eneo hilo kuzuiwa lisijengwe.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha sana wanaenda kuzuia miradi ambayo inajengwa ya Serikali lakini ile miradi ambayo watu wanakwenda kuomba vibali kwao wanawapa pasipo mashaka, sasa wanaleta taharuki kwa jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo hilo ambalo wanaliuia tayari kuna jengo la Halmashauri limejengwa pale, limejengwa kwa gharama kubwa ya pesa za Serikali. Sasa sijaelewa zuio hili ni kwa ajili ya sekondari tu au zuio hili na lile jengo la Serikali linavunjwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia sijaelewa, kwa zuio hili walilolitoa na vile viwanda walivyotoa kibali wao wanaenda kuvibomoa? Kama watavibomoa, wale wenyewe viwanda ambavyo wameviendeze watawapa fidia ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, najua muda ni mchache, lakini ninaamini mengi nitazungumza na Mheshimiwa Waziri pale ambapo nitapata nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki. Mheshimiwa Soud Mohamed Juma ajiandae.

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuimarisha muungano wetu, lakini pia kuweka mazingira yetu sawa ili sisi kama binadamu tuwe tunaishi kwa amani kabisa.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeze zaidi kwenye maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza nitazungumzia suala la muungano nae neo la pili nitazungumzia suala la mazingira.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muungano wa nchi mbili, kati ya Zanzibar pamoja na Tanganyika. Jana tu ndiyo tumehitimisha miaka 58 ya muungano wetu wa Tanganyika pamoja na Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, huwa kila mwezi tunapata taarifa kupitia *BOTambazo zinatambua uchumi* wa Zanzibar pamoja na uchumi wa Tanzania Bara, lakini la kustaajabisha taarifa zinapokwenda nje ya nchi kwa maana ya kwenye taasisi za kifedha, *World Bank* pamoja na *IMF* taarifa hizi haziendi kwa sura ya kuitambua Zanzibar. Naomba sana, uchumi wa Zanzibar ni mdogo na ni uchumi ambao ni wa Kisiwa, naomba sana kupitia Wizara hii lazima iangalie ihakikisha kwamba, tunapopeleka taarifa za kifedha lazima kuwe kuna *figuresura* ambayo tayari itaonekana Zanzibar na uchumi wake.

Mheshimiwa Spika, kila mwezi, kila mwaka, *IMF* pamoja na *World Bank* wanatoa taarifa namna ya uchumi, wenyewe wanaita *Economic update*, kwa Zanzibar haitambuliki. Zanzibar ni sehemu ya kisiwa, lakini pia ni nchi ambayo tayari imeunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naiomba sana Wizara yako Mheshimiwa Jafo kuhakikisha kwamba, Zanzibar zinapokwenda taarifa basi uchumi wa Zanzibar unatambulika kwa sura ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niende eneo la pili, eneo la mazingira. Niwapongeze sana watendaji kwa kazi kubwa

ambayo wanaifanya kwa upande wa Tanzania Bara. Ikumbukwe kwamba, eneo la mazingira ni eneo ambalo linajumuisha upande wa pili wa Zanzibar. Tunashangaa sasa hivi kuna miradi ambayo inatekelezwa Zanzibar kwa muda wa zaidi ya miaka mitano, lakini fedha Zanzibar hazifiki kwa wakati. Ukiulizia Zanzibar wanalamika kwamba, fedha zinaganda Tanzania Bara, Tanzania Bara na huku wanasema kwamba, fedha zinafika Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, leo hii kuna mradi ambao unatekelezwa Wilaya yangu ya Kaskazini Unguja kwenye viji ya zaidi ya vitatu. Kuna Kijiji ambacho kinaitwa Mbuyutende, kuna Kijiji ambacho kinaitwa Matembwe Kijini, kuna Kijiji ambacho kinaitwa Juakuu. Fedha zimetengwa nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ikolojia, lakini cha kuchangaza mpaka leo hii zaidi ya miaka mitano miradi ile bado haijakamiliika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, juzi tulienda na Kamati yetu ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kuna baadhi ya vifaa vimenunuliwa, kuna ununuzi wa boti, boti limenunuliwa zaidi ya Milioni 46. Ni jambo la kustaajabisha na la kushangaza kabisa, boti moja limenunuliwa zaidi ya Milioni 46 haiwezekani hata siku moja, haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tathmini ya sisi ambao tayari tumezaliwa kandokando ya bahari, lakini pia ni wavuvi, boti moja linanunuliwa zaidi ya Milioni 12 siyo Milioni 46. Naiomba sana Wizara yako, Wizara ya Muungano kuhakikisha kwamba, kwenye matumizi ya fedha lazima tuende tukaangalie vizuri. Fedha zinapotea kwa upande wa Zanzibar, lazima tukae tuhakikishe kwamba, fedha zinaenda kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia jambo la pili, kuna ujenzi wa majiko sanifu, jiko moja limejengwa zaidi ya shilingi Laki Saba kwa gharama ya kawaida. Kiuhalsia ukiliangalia jiko moja ni sawasawa na Shilingi Laki Mbili. Upotevu wa fedha ni mkubwa sana, fedha ambazo zinaenda Zanzibar hakuna usimamizi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara yako Mheshimiwa Waziri, kwenye fedha ambazo zinaenda Zanzibar za Muungano, zinapoenda Zanzibar Wizara yako ihakikishe ndiyo inasimamia ile fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeefika Zanzibar tumewahoji watu wa Wizara ambao wanashughulika na masuala ya miradi hii hawana majibu. Tunajiliza nani msimamizi wa fedha hizi ambazo zinakuja Zanzibar? Majibu hakuna kuhusiana na fedha ambazo zinaenda Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda ni mdogo naombaa niishie hapo. Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Juma. Mheshimiwa Salum Mohamed Shaafi ajandae.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo katika hotuba hii muhimu yenye maslahi mapana kwa Taifa letu na kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Kaka yangu Mheshimiwa Suleiman Jafo kwa kuja Jimboni kwangu na Wilayani kwangu kuja kunitembelea katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Bila shaka Mheshimiwa Waziri uliweza kuona uhalisia wa athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, hususan katika Kijiji cha Nungwi na Matemwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kunako tarehe 26 Julai, 2021, Wizara ya Madini ilikutana na Wizara ya Maji na Nishati ya Zanzibar, kukaa na kujadili baadhi ya mambo. Licha ya kwamba, taasisi hizi mbili siyo za kimuungano, lakini kwa nini zimekaa na kujadili mustakabali wa Watanzania? Sababu kubwa ni kulinda na kudumisha mahusiano yaliyokuwepo baina ya pande mbili hizi za Muungano.

Mheshimiwa Spika, hii inatupa picha ya wazi kwamba, kuna masuala mengine ambayo yana maslahi mapana kwa Watanzania hata kama siyo ya kimuungano yanaweza kujadiliwa kwa maslahi ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Mkao wa Kaskazini Unguja, hususan katika Vijiji vya Pwani Mchangani, Kijini na Jimbo la Nungwi kwa ujumla ni vijiji ambavyo vimetawaliwa na ukame. Ukame ambaou unasababishwa na maji ya bahari kuvamia maeneo yale, kitu ambacho wananchi wa kule wamekuwa wanapata shida kubwa katika kuyatafuta maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, jambo lile limesababisha wananchi wa maeneo yale kuathirika kwa sababu ya kimaumbile kwa upande wa maji, vilevile wameathirika kutokana na athari nyingine za mabadiliko ya tabianchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ione haja ya kukaa na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuandaa miradi maalum ya kwenda kunusuru maisha ya wananchi wa maeneo yale. Kwa sababu, suala la mabadiliko ya tabianchi ni suala la kimuungano na suala la mazingira siku zote lina *element* ya masuala ya kimuungano, wale wananchi kwa kuwa wameathirika na sababu za kimazingira na athari zinzotokana na mabadiliko ya tabianchi hakuna haja ya kusema labda kwa nini yazungumziwe masuala ya maji katika suala ambalo ni la kimuungano? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii maji ya maeneo yale yameathirika kutokana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Mwanzoni historia inaonekana wazi kwamba tulikuwa tunapata maji safi na salama mnamo mwaka 2010, nafikiri Wizara ya Muungano na Mazingira ilitupa miradi kwa kuona ule uzito, lakini miradi ile imeshakuwa michache kulinganisha na ongezeko kubwa la wananchi wa maeneo yale. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ziara yako uliyokuja wananchi wanatarajia mambo makubwa mno kutokana na ziara yako, lakini bado wana hamu ya kukuona unarejea tena na tena kwa sababu athari zile mkiendelea kukaa kimya bado zinaendelea kuathiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu cha msisitizo kikubwa Wizara hii ione haja na kila sababu ya kufanya mambo mawili kupitia miradi hii ya kimuongano.

Mheshimiwa Spika, kwanza Zanzibar kuongezewa fungu kwa sababu, athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi licha ya kwamba, huku maeneo ya Ukerewe na maeneo mengine zinapatikana, lakini athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi zinaonekana katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, hata kule Pemba kulikuwa na mabonde 18 wananchi wa kule walikuwa wanalima mihogo, mbaazi, kunde, lakini leo hii hatuzungumzii tena maeneo yale yote yameshaliwa na bahari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ndio maana nasisitiza...

(Hapa kuengele illilia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae. Mheshimiwa Soud? Haya, Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King. Mheshimiwa Hajji Makame Mlenga ajiandae.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Moja kwa moja naomba niende katika hoja ambayo iko mezani kwetu. Huu ni mwaka wa 58 wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kihistoria muungano

huu ulikuwa ni baina ya nchi mbili huru; Nchi ya Tanganyika na Nchi ya Zanzibar, lakini nchi zote hizi zilikuwa ni Wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaungana tulikubaliana mambo 11. Katika mambo haya naomba nisiyaseme, lakini yako mambo ambayo si ya Muungano lakini Zanzibar imekosa nafasi kama ni sehemu ya Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar. Naomba niseme masuala ya michezo siyo sehemu ya Muungano, masuala ya afya siyo sehemu ya Muungano, lakini leo yapo mambo tumeambiwa yamepatiwa ufumbuzi, yako mambo ambayo tumeambiwa haya tayari tumeyapatia ufumbuzi na sasa hatuwezi kuyajadili tena badala yake tunaenda katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, masuala ya Afrika Mashariki, masuala ya kikanda pamoja na kimataifa. Leo Zanzibar tuna *ZFF* Tanganyika tuna *TFF* lakini *TFF* inabeba nembo ya Muungano ambayo sasa inakuwa ni *memberwa FIFA* na inaleta misaada *TFF*. Je, naomba kujua Mheshimiwa Waziri atakapokuja, tunafahamu mgao ambao unatoa *FIFA* Zanzibar tunakuwa ni sehemu ya manufaiko katika mgao huo?

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukienda katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuna mahali, kuna sehemu imetutaka kwa mujibu wa makubaliano yetu tutakuwa na *account* ya pamoja na fedha. Katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri amesema haya ni mambo ambayo sasa tunaendelea kuyashughulikia. Sasa ni mwaka wa 58, bado tunaendelea kushughulikia matatizo yale yale, kitu ambacho kwa Wazanzibar hatuoni kwamba sasa kuna nia na dhamira njema katika Muungano huu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme wazi, hakuna mtu ambaye hautaki Muungano huu, sote tunautaka, lakini tunataka Muungano wa haki na tunataka Muungano wa usawa. Naomba sasa ufike muda Serikali ituambie ni lini Akaunti ya Pamoja ya Fedha itafunguliwa, itaananzishwa? Kwa

sababu zimekuwa ni danadana za muda mrefu na sasa tumefika mahali tunaona kwamba Muungano huu ni jambo ambalo linatunyonya Wazanzibar. Tufike mahali kinia safi tu tuseme yapo mambo ambayo tuseme, haya tuyatatte kwa maslahi ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nitoe rai na naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa ifike mahali atuambie sasa ni lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na nia ya dhati kuulinda Muungano huu kwa kufungua akaunti hii ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimwombe Mheshimiwa Waziri na niiombe Serikali sasa ituambie ni lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano itaipatia Zanzibar...

SPIKA: Mheshimiwa Salum kuna taarifa

TAARIFA

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba Muungano wetu una manufaa makubwa kushinda changamoto. Kwa hiyo analipotosha Bunge na Watanzania kusema kwamba muungano unawanyonya, ziko faida nydingi za Muungano ambazo tunazo hata kuwepo hata ndani ya Bunge hili ni faida za Muungano (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Salum Shaafi, unaipokea taarifa hiyo?

61 -

MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI: Mheshimiwa Spika, siipokei na sina haja nayo. Hakuna mimi sijasema naukataa wala naupinga, bali uhalisia ulivyo hakuna asiyejua kama Muungano huu una changamoto nydingi hususan kwa upande wa Zanzibar. Hili ni jambo ambalo naomba litambulike kwa sababu katika lile jambo ambalo kwamba Zanzibar ni sehemu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Afrika Mashariki leo tunachagua Wabunge wa Afrika Mashariki, Zanzibar...

(Hapa kuengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Shafi muda wako ulikuwa umeshaisha nilikuwa nimekupa muda ili umalizie hoja yako

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Ilishapigwa kengele

SPIKA: Kengele ilishagonga.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenga, Mheshimiwa Mariam Omar Said ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nashukuru sana kupata nafasi hii. Nianze na msemo, watu wengi sana huu msemo tulikuwa hatuujui, lakini leo mimi nitautolea maana. Kuna msemo unasema heri ya nusu shari kuliko shari kamili.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natafakari sana juu ya msemo huu, lakini jana nilipata maana yake na alichonifundisha maana msemo huu ni mzee Msekwa aliposema kumbe kulikuwa kuna changamoto kubwa zaidi ya kiusalamu kule Zanzibar baada ya Mapinduzi, kwa maana hiyo kulihofiya kuja kuvamiwa tena na kupinduliwa kwa sababu ilikuwa haina Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii ilikuwa ni shari kamili, lakini nusu shari ndiyo kama haya mambo madogo ambayo tunayazungumza, ni mambo ambayo yanaweza yakarekebishika. Kwa maana hiyo ile shari kamili tumeepukana nayo, lakini sasa hizi nusu shari zinaweza zikaondoka kirahisi. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Muungano wetu huu ni Muungano mzuri sana kwa sababu katika miungano yote ya katika dunia hawana chombo cha kukaa wakazungumza mambo yao, lakini sisi kwenye Muungano wetu huu tunacho chombo ambacho ndiyo hiki cha Mheshimiwa Jafo hapa tunamwambia ambacho tunakaa tunaeleza matatizo na changamoto ambazo zimo katika Muungano na ndipo zinakuja zinatatuliwa changamoto hizo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuna aya moja inasema kule kwenye *Quran* kwamba wanasesma *kulaukana fil-ardhi malaikatu yamshuna mutumainina laa-nazzalna minasamaai malaka rasula*. Ingelikuwa malaika ndiyo wanaoishi kwenye ardhi basi na mitume yao ingekuwa ya kimalaika lakini wanaoishi kwenye ardhi ni binadamu na mitume yao itakuwa ni binadamu. Hii Serikali inaongozwa na wanadamu na ni watu na sisi ni wanaadamu, kwa maana hiyo tunapaswa tuiambie Serikali yetu kuwa kile ambacho kinatutaka. Kwa hiyo tuiambie Serikali ili kuondosha zile changamoto isitoshe na sisi wenyewe ni ndugu, kwa kuwa ni ndugu kwa hiyo tutakapoambizana tutasikilizana zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa na mimi Mheshimiwa Jafo nisikilize jambo moja, kuna makampuni ambayo yamesajiliwa Tanzania Bara yanafanya kazi Zanzibar na kuna makampuni yamesajiliwa Zanzibar yanafanya kazi Tanzania Bara, lakini kampuni zile zilizosajiliwa Tanzania Bara zinafanya kazi Zanzibar hazilipi kodi ya mapato yaani (*Cooperative Tax*) na kwa sababu *Companies Act* ya Tanzania Bara inataka mtu aliipe *Tax Headquarter*, kwa hiyo zile *Cooperative Tax* hazilipwi kule na zile kampuni kule zipo ukichukulia kampuni zote za simu ziko kule, ukichukulia kama benki mengi yako kule, ukichukulia makampuni ya ujenzi yako kule, hayalipi na kule wana-operate under certificate of compliance. Sasa ushauri wangu kule alitoka Waziri mmoja wa Zanzibar alisema hivi kwamba kampuni zinazotoka Tanzania Bara zikajisajili tena Zanzibar, hicho kitu ina maana kwamba hawa ndugu zenu wanakuiteni mwingine katika mazungumzo juu ya jambo hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba na hili jambo la kuhusiana na mambo ya *Cooperate Tax*, kwa sababu tunajua Ibara ya nne iliyotaja kutakuwa na mambo ya Muungano kwenye nyongeza ya kwanzana *item* (10) imetaja hiyo kodi ya mapato kwa watu binafsi na makampuni. Hata hivyo, kulipita makubaliano kwamba kila mmoja atakuwa anakusanya kodi hiyo ya mapato sehemu yake, lakini makampuni yale yanafanya kazi kule, lakini yanalipa kodi ya mapato Tanzania Bara, kwa maana hiyo Zanzibar pamoja na kuwahudumia wananchi ambaao ni wateja wa makapuni yale kwamba inakuwa haipoeki kodi kutoka makampuni yale hakuna *NMB*, hakuna *CRDB*, hakuna *TCB*, hakuna *NBC*, hakuna hizo *TIGO*, hizo zote hazilipi kodi ya mapato kule Zanzibar na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tunaliomba hili lifanyike, kikae kikao maalum hili lifanyike na Muungano huu ninavyosema tumeungana sisi ni zaidi ya haya mambo ambayo yameandikwa. Wizara ya Kilimo siyo ya Muungano lakini nenda katazame katika masoko ya Zanzibar, sisi tunaita mbatata hivi viazi mviringo utakuta kule maharage, utakuta kule kila kitu, hutokuta kule mchele labda umeandikwa huu wa Cheju, lakini mchele wa Mbeya kule utaukuta. Kwa maana hiyo tumeungana zaidi na Muungano wetu siyo wa mambo ambayo yako kwenye makaratasi, Muungano wetu ni wa mambo ambayo tumeungana kwa damu na kiudugu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naunga mkono hoja Mheshimiwa akatutekelezee mambo yetu hayo. Nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Makame Mlenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Omar Saidi na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

MHE. HAJI MAKAME MLENGUE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuwa mionganini mwa wachangiaji katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Niseme tu kwamba Muungano huu una tija

sana na ndiyo maana leo na sisi tuko hapa tunajilabu na kusema ambayo tunayazungumza kupitia suala hili la Muungano. Katika mchango wangu nitaonyesha faida ambazo nimezipata ndani ya Jimbo langu kupitia suala hili la Muungano, lakini hasa mchango wangu utaenda kuzungumzia suala la mazingira katika upande wa hifadhi hai ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumepata bahati ya kuwa na hifadhi hai zisizopungua sita. Katika hifadhi hai hizi sita ambazo zimetambuliwa na UNESCO kuwa hizi tayari zimeshafikia katika kiwango cha hifadhi hai. Kutohana na ziara ya mama ya uzinduzi wa *Royal Tour*, hifadhi hizi nina wasiwasi kwamba zinaweza zikazidiwa na wageni. Kwa hiyo niseme tu kabisa kwamba hifadhi hizi tuweze kuziangalia kwa kiwango kikubwa, kwa sababu hizi hifadhi hai tusiweze kupoteza asili ambayo ipo ndani ya hifadhi hizo kwa sababu tutakapopoteza asili ya hifadhi hai, tunaweza kupoteza ile huduma ambayo tunaweza kuitoa kwa wale wageni ambao tunawatarajia watakuja katika kutembelea hifadhi hai hizi.

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu makubwa ni kwamba, wageni watakapokuja waweze kupendezwa na hifadhi hai hizi ili wawe na ndoto za kuweza kurudi, lakini pia wakazisimulie vizuri ili kuweza kuongeza tija ya kupata wageni. Hifadhi hai hizi ambazo zipo katika nchi yetu ya Tanzania ikiwemo Ngorongoro, Lake Manyara, Serengeti, East Msambara, Gombe na Jozani Chwaka. Kwa bahati nzuri Hifadhi ya Jozani iko katika eneo la Jimbo la kwangu na imepata bahati ya kusajiliwa toka mwaka 2016, lakini kwa bahati mbaya sana hifadhi hii haijakamilisha utaratibu ambao unaotakiwa na UNESCO ikiwemo uzinduzi wa hifadhi hai.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tarehe 24 na tarehe 25 baada ya kuzungumza, walikuja Zanzibar wakafanya kikao pamoja na Idara ya Mazingira pamoja na Idara ya Misitu na kwa bahati nzuri walinalika nikashiriki katika kikao hicho cha kuweza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuona namna gani tunaondoka katika hatua ile ambayo tulikuwa nayo mwanzo ya kutokufanya uzinduzi, lakini hivi sasa mazungumzo yanaenda ili kuweza kufikia hatua ya uzinduzi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 tulitembelea katika eneo lile la Jozani ambalo linategemewa kuwa hifadhi hai pale ambapo tutakamilisha utaratibu kama ambavyo umeelezewa. Hata hivyo, namwomba tu kaka yangu Waziri Jafo, najua watu wake wamekuja kumpa habari na wamefanya kazi nzuri, Wizara yake inafanya kazi nzuri, lakini ningefurahi sana hata ye ye mwenyewe akawa miongoni mwa watembeaji katika eneo hilo ili tuweze kuona namna gani tunaenda kuitengeneza Jozani ili ifikie katika kiwango kizuri.

Mheshimiwa Spika, wakati niko mdogo nilikuwa kijijini kwangu tunazungumza kwamba msitu hautaweza kumalizika hata siku moja, kwa sababu kweli kulikuwa na msitu ambaou ulikuwa wewe mwenyewe unaogopa kutembea, lakini leo hii misitu hii hakuna, misitu ile imebakia katika eneo chache hili la Jozani.

Mheshimiwa Spika, zamani wakati tunatembea, ilikuwa ukienda kazini msituni maana yake unakutana na wanyama tofauti tofauti wakiwemo chui leo chui haonekani, lakini ukirudi mnakaa mnasimuliana, unakuta leo mwenzako anakwambia tumekutana na chui, huyu anakwambia tumekutana na nani, lakini leo hakuna, uoto huu tunautegemea sana katika eneo la Jozani. Naomba tuliangalie sana na Mheshimiwa Waziri basi, naomba siku moja tufuatane twende Jozani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. HAJI MAKAME MLENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Omar Saidi atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Saidi ajilande.

MHE. MARIAM OMAR SAID: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia muda ili kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele jioni hii. Moja kwa moja nitajikita katika suala la Muungano, sote wakati tukiwa tunachangia bajeti hii ya Muungano tunachangia kwa maslahi mapana ya kuwa tunaupenda na kuuensi Muungano. Hata hivyo, tukumbuke na tukubaliane tu na matokeo kwamba, ni kweli zipo changamoto ambazo kwamba zimepatiwa ufumbuzi lakini bado hazijafanyiwa kazi na zipo zile ambazo hazijapatiwa ufumbuzi na hazijafanyiwa kazi na hizi ndiyo changamoto kubwa zaidi ambazo kwamba zinawaumiza wananchi hususan kwa upande wa Zanzibar. Hapo sitaki niendelee sana, niishauri tu Wizara, tuweze kuzifanyia kazi zile changamoto ambazo tayari zimeshpatiwa ufumbuzi, lakini pia na zile ambazo hazijapatiwa ufumbuzi, basi twende kwa haraka zaidi ili kuhakikisha tunauweka Muungano wetu katika sehemu salama.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, kiuhalisia mabadiliko ya tabia nchi hakuna ambaye kwamba hayamgusi, hapa ndani na hata huko nje. Ukitsemu suala la mabadiliko ya tabia nchi kila mtu linamgusa, hakuna mtu ambaye yatamwacha salama pindi yanapotokea. Sasa basi niishauri Wizara kwenda kwa kasi katika ile miradi ya mabadiliko ya tabia nchi, hususan kama kwa upande wa Zanzibar tukiangalia muunganiko wetu wa nchi ya Zanzibar ni visiwa na kawaida visiwa vinapata mabadiliko ya tabia nchi katika sehemu zote, mvua ikiwa kubwa tumo kule Zanzibar, jua likiwa kali tumo, bahari ikipata tetesi kidogo tu tumo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunaathirika zaidi katika pande zote, tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ndiyo wahusika wakuu kwenye masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, kwa kupitia miradi ya mabadiliko ya tabia nchi, watuangalie kwa jicho

la huruma zaidi Zanzibar. Hivi sasa Zanzibar kuna visiwa hususan kule kaskazini Pemba kuna kisiwa cha Mtambwe Kuu ni kisiwa cha Jimbo la Mtambwe la Mheshimiwa Khalifa. Hiki kisiwa tupo karibu kikipoteza kabisa, ni miaka mingi sasa, hii ni changamoto kubwa na hajafanyiwa kazi. Si hicho tu kuna kisiwa cha Kojani, kisiwa cha Fundo, visiwa vyote hivi vina hali mbaya sana. Tukiangalia Kisiwa cha Kojani tuna Naibu Waziri wa Fedha jamani ni aibu, hebu tufanyeni basi twende kwa kasi angalau hizi kero za mabadiliko ya tabia nchi ikifika 2025 tuwe angalau kwenye 85% basi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la mwisho ambalo nataka nilichangie, nimemsikia Mheshimiwa Jafo hapa kawazungumzia sana mabalozi, lakini ni watu ambao tupo katika hali ngumu kiutendaji wa kazi, nazungumza hivyo mimi ni Mbunge lakini pia ni Mwanakamati ya Muungano na Mazingira lakini pia ni balozi. Juzi tu kaka yangu Mheshimiwa kanipita jina lake Mheshimiwa Msukuma alijuzulu ubalozi baada ya kuona kwamba hauna faida. Mheshimiwa Jafo atuangalie kwa jicho la huruma mabalozi, mabalozi wanajituma sana na kazi zao unazijua, mabalozi ili apate fursa ya kufanya kazi akialikwa kwenye shughuli ya mtu ndiyo anaenda kuhamasisha huko. Msanii akialikwa kwenda kutumbuiza ndiyo anapata kwenda kuhamasisha huko, kinyume na hapo hatuwezi kufanya kazi zetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, balozi kama balozi mimi ananijua Waziri tu, nitakapokwenda popote pale nikijitambulisha naambiwa toa kitambulisho hakuna anayenielewa balozi mimi. Hivyo sasa ushauri wangu, tunataka Mheshimiwa Jafo atuwezesha mabalozi kutenda kazi. Anatuona na tunajitolea kwa hali na mali kwa nguvu zetu zote atushirikishe katika kila sehemu ili mradi mabalozi tuweze kufanya kazi zetu kiufanisi. Kama Waziri ameutambua mchango wetu na kuweza kuuelezea hapa, isiishie hapo tu. Mimi Mariam naweza kukimu baadhi ya nini ndogo ndogo, lakini kuna mabalozi ambao wana hali mbaya, mtu hawezi hata kutoa nauli na bodaboda kwenda sehemu nyingine, ukifika kule bado unakumbana na changamoto, unaanza kuulizwa wewe ni balozi? Ndiyo. Kakuteua nani? Nipe kitambulisho, tayari unaanza kutoka

kwenye mood, hata lile ulilolikusudia kwenda kulifanya, linakushinda kufanya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mchango wa Mheshimiwa Balozi wa Mazingira hapo, nadhani unawakumbusha wale mamlaka za uteuzi za hawa mabalozi. Maana nadhani zile mamlaka zinateua mabalozi wengi halafu haziwawezeshi. Sasa wakati ushafika. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Naibu Waziri Khamis Hamza Khamis ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kuipongeza sana Wizara na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudini alizochukua kukutana na asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinafanya kazi ya kuhifadhi mazingira. Wana asasi wamefarijika sana kwa kuwatambua kwa sababu sisi wana asasi zisizo za kiserikali tunafanya kazi kubwa sana kuisaidia nchi hii kuhifadhi mazingira yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kututambua kwako Mheshimiwa Waziri tumefarijika sana. Tunachoomba, tunapokuja Wizarani kwako, sisi wana asasi utupe ushirikiano wa kutosha ili tuweze kutekeleza majukumu yetu pale ambapo tuna kwama.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mazingira, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa juhudini zinazofanywa katika kuhifadhi mazingira ikiwemo upandaji miti. Hata hivyo nataka niishauri Serikali, kwa msamati wa upandaji miti, ni bora sasa twende na msamati wa Uoteshaji wa Miti. Kwa sababu tunapopanda miti, baadaye hatujui inakua au haikui; lakini tukiotesha tutaifuatilia tangu tumeipanda mpaka inakua na kuona imefika hatua gani?

Tunapanda miti mingi lakini mingi inakufa njiani, kwa hiyo, ni bora tuoteshe miti ili kuisimamia miti hii tuone inakuwa endelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye upande wa Muungano. Muungano wetu umefikisha miaka 58, ni safari ndefu, tumeanza mbali; na Muungano huu ni Tunu na Hazina ya Tanzania. Mpaka kufikia miaka 58 Muungano huu umepitia changamoto nydingi sana mpaka kufikia hapa. Changamoto ya kwanza ya kuhakikisha Muungano huu hauendelei, ni pale alipouawa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mheshimiwa Abeid Amani Karume. Hilo ndilo jaribio la kwanza la kutaka kuona Muungano huu hauendelei. Tusishangae kwamba bado Muungano huu kuna watu wanautazama kwa jicho la husuda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika miaka 58, chochote kinachokua kinakuwa na changamoto. Katika kukua kuna changamoto za Muungano, na changamoto hizi hazitaisha kwa sababu Muungano huu unakua na nchi inabadilika na dunia inabadilika na miundombinu inabadilika. Kwa hiyo, changamoto zitaendelea kujitokeza kila Muungano huu unapoendelea kukua (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri, Serikali iendelee kuzitatua changamoto hizi pale zinapojitokeza kwa wakati muafaka ili kuepusha manung'uniko, chuki na kejeli kwa Muungano huu. Tukizitatua changamoto zetu kwa wakati muafaka, Muungano huu utaendelea kudumu na kupendwa kwa muda wote na hakutakuwa na manung'uniko na chokochoko zozote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu na ni imani ya Watanzania kwamba viongozi wetu wana dhamira ya dhati katika kuuendeleza Muungano huu kwa vitendo kwa faida ya nchi zetu mbili za Muungano kwa maana ya Zanzibar na Tanzania Bara. Dhamira zao za dhati zilianzia kwa waasisi wa Muungano huu; Marehemu Mheshimiwa Abeid Amani Karume na Marehemu Mzee Nyerere. Hao ndio waasisi. Marais waliofuatia baada yao, akina Mzee Jumbe, Mzee

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mkapa, Mzee Ali hassan Mwinyi na mpaka sasa tunaye Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akishirikiana na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba wataendeleza nyayo na mema yote yaliyoanzishwa na waasisi wa Muungano huu kuutekeleza na kuusimamia Muungano huu kwa vitendo kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania, maslahi yetu Watanzania na vizazi vijavyo vya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, atafuatiwa na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis na mtoa hoja ajilandae.

Mheshimiwa Mwanahamis, hayupo, namwita sasa Mheshimiwa Zahor, atafuatiwa na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis na Mheshimiwa Mtoa hoja ajiandae

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adhimu. Kwa sababu ya muda, naomba nijikite kwenye mambo manne kwa ufupi na ninaamini wenzangu watanielewa.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, tunayo hoja ya mambo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyazungumza ambayo tumekubaliana. Ameyataja katika hotuba yake. Naomba kushauri kwamba haya ambayo tumekubaliana, basi sasa mchakato wa kisheria uendelee ili mambo haya yaeleweke kisheria kwamba sasa ni mambo tuliyokubaliana na yanatambulika kisheria. Hilo la kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tunayo hoja ya mazingira. Mimi natoka Jimbo moja linaitwa Mwera. Kwa lugha ya kawaida, Mwera ni mbali sana, lakini kiuhalisia Mwera ipo mjini, imezungukwa na majimbo mengi sana. Mwera ni chimbuko la maji, ni chimbuko la chakula, ni chimbuko la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

matunda na ni chimbuko la Zanzibar. Kwa sababu Mwera hii ndiyo ambayo imeleta Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa sababu tumejaribu lakini bado tunayo changamoto. Mwera tunayo changamoto ya uharibifu wa mazingira, hasa kwa sababu maji yanatuathiri sana. Sasa kwa ufupi kabisa naomba Wizara yako na hili lichukuliwe kwa sababu tulishazungumza na hali halisi unaielewa, Mwera unaielewa na umeshakwenda siyo mara moja; siyo mara mbili na siyo mara tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mwera itazamwe kwa jicho maalum ili kujua inasaidiwa je kutatua tatizo letu la mazingira. Mwera inaumia, Mwera inaangamia, Mwera inazama kwa sababu kila mvua inapokuja Mwera tunaingia kwenye matatizo ya mafuriko. Naomba sana iwe ni mradi maalum wa kusaidia Mwera ili kuiondolea tatizo la kuzama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine dogo kabisa, tunazungumza *issue* ya nafasi za ajira za Muungano. Hizi nafasi kwa mujibu wa sheria, tumekubaliana Zanzibar watapata ngapi, wenzetu watapata ngapi? Sasa sipo kwenye hoja hiyo; hoja yangu ipo kwenye hili; mara nyingi tunaangalia vijana wetu ambao wamepata nafasi ya kwenda kwenye Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Kujenga Uchumi. Sasa hiki kimekuwa kigezo kikubwa, kwa hiyo, vijana wetu wengi wanakosa nafasi hii kwa sababu hawakupata nafasi ya kwenda kwenye majeshi haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali hatuna uwezo wa *ku-absorb* vijana wote hawa wakaenda kwenye majeshi yetu, hatuna nafasi hiyo, kwa hiyo, hawawezi kwenda wote kwenye Jeshi la kujenga Taifa wala hawawezi kwenda wote kwenye Jeshi la kujenga Uchumi, nawaomba sana, kigezo hiki cha kwamba mtu amepitia kwenye JKU au JKT kisiwe kigezo pekee. Hiki kiwe ni nyongeza, lakini muhimu iwe elimu na vitu vingine ndiyo viwe vinazingatiwa. Siyo kwamba eti kwa sababu hakwenda JKT au JKU, ndiyo kigezo cha kumfelisha, naomba sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, cha mwisho, amezungumza pale kaka yangu *issue* ya kuheshimiana. Naomba nirudie hapa, kwamba ili mradi sisi ni binadamu, hakuna nafasi kwamba tutakuwa wakamilifu mpaka tunayoingia kaburini. Kwa hiyo, nawaomba sana wenzetu, taaluma ya Muungano mwendelee kuitoa kwa sababu bila ya hivyo tutaendelea kulumbana kila siku; na bila hivyo kila siku tutaendelea kuona tuna matatizo. Matatizo ni sehemu yetu na yataendelea kutatuliwa taratibu, lakini kubwa tuendelee kutoa elimu kwa sababu bila elimu, kila siku tutazungumza hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii naomba kuchangia kama ifuatavyo; kwanza Wizara inatakiwa kuangalia uwezekano wa namna ya kunufaika na miradi ya kupunguza hewa ya ukaa iliyopo duniani ambayo wapo baadhi ya wawekezaji wameanza kuwekeza nchini, tunayo misitu ya asili mingi ambayo kwa maoni yangu inakidhi vigezo vya kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, pili, kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wilaya zenye vyanzo vingi vya maji kama Wilaya ya Kilolo ili kuendelea kulinda vyanzo hivyo na kuwa na njia mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kukamilisha mpango kabambe wa hifadhi ya mazingira kama ilivyojonesha katika ukurasa wa 36 wa hotuba ya bajeti. Pamoja na pongezi hizi ninaomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu kukijanisha Dodoma; ninashauri kushirikisha vyuo vya elimu ya juu na katika kukijanisha Dodoma. Kwa mfano, tunawenza kusema kila wanafunzi wawili wapande mti na kuulea katika muda wote wa

masomo. Tuna vyuo kama vile *UDOM*, *St. John*, *Mipango-IRDP*, *CBE*, Hombolo na baadhi ya vyuo binafsi kama vile *DECA*. Ikiwa wanafunzi wanakaa *almost* miezi tisa katika mwaka, ninaamini wakipewa mche na kukawa ni sehemu kwa mfano ya kigezo cha kupata mkopo, tunaweza kusaidia kukijanisha maeneo ya vyuo na maeneo yanayozunguka.

Pili, *COP26* na namna ya kunufaika na fedha za mifuko ya *GCF*, *GEF*, *Adaptation Fund* na kadhalika, nilifuatilia mkutano wa Glasgow, niliona ambavyo Mheshimiwa Rais alivyoyasihi mataifa makubwa kuheshimu *pledge* zao katika kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi. Tumeona *CRDB* wamepata fedha kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuzisaidie taasisi nyingi zaidi kama vile vyuo vikuu, *NGOs* na kadhalika ziweze kupata fedha hizi ambazo nyingi ni *grants*. Ukipuatilia kwa ukaribu utafahamu kwamba ili ku-*access* hizi *funds* kuna vigezo kama vile kupata *accreditation*. Nchi kama Kenya, Rwanda na Morocco wamekuwa wanufaika wa hizi *funds* na zimesaidia katika miradi ambayo inasaidia kuinua maisha ya wananchi wa kawaida. Kwa mfano kama ilivyo katika mikoa ya Iringa na Njombe ninaamini *funds* hizi zingeweza kuhamasisha zaidi suala la kupanda miti katika mikoa mingine kadri ya *species* ambazo zitafaa.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu hewa ukaa/*carbon credit*; wananchi wengi wa Mafinga/Mufindi wamekuwa wakiomba kupata elimu kuhusu suala hili. Tunawashukuru sana Wakala wa Misitu Tanzania-TFS ambao waliwesheza ziara ya mafunzo kwa Madiwani wa Mafinga na Mufindi kutembelea Wilaya ya Tanganyika kuhusu manufaa ya hewa ukaa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mufindi ama kwa kutojua au kwa shida zao waliuza maeneo yao kwa makampuni makubwa kama vile *green resources* ambapo kuna maelezo yasiyo rasmi kwamba walihidiwa kwamba waachie maeneo yao na kwamba watanufaika na malipo

ya hewa ukaa. Kwa sababu suala hili naweza kusema ni *complicated*, nashauri itolewe elimu kwa kuanza na semina kwa Wabunge na baadae kwa Wenyeviti wa Halmashauri na wadau wengine kadri mtakavyoona inafaa ili tuweze kufahamu ni vigezo gani vinapaswa kuzingatiwa ili taasisi au mwananchi apate kunufaika na masuala ya hewa ukaa. Kwa mfano ilivyo sasa, wananchi wa Mufindi na maeneo ya Morogoro kama vile Uchindile wanadai kuwa fedha za hewa ukaa zinatolewa, lakini wanufaika ni makampuni makubwa yaliyopanda miti katika ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu kupanda miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri; kama nilivyoshauri katika kukijakinisha Dodoma, nashauri ushiriki wa shule za msingi, sekondari na vyuo, sio katika kupanda tu bali katika kuitunza miti. Kwa sababu hakika tumekuwa tunapanda miti kila mwaka lakini inayo-survive ni michache mno.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na fedha za Mfuko wa Jumbo; napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka mpango huu wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo katika Majimbo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kama inavyosomeka dhana ya mfuko huu ni kuchochea maendeleo, lakini kwenye baadhi ya majimbo mengine huwa haikidhi dhana hii; kwa mfano katika majimbo ya Zanzibar kama inavyojulikana kuwa mwaka 2015 ulifanyika ukataji mpya wa majimbo, majimbo mengine yameongezeka sana. Miongoni mwa majimbo hayo ni jimbo la Tumbatu.

Mheshimiwa Spika, kiasi ya fedha tunachopata ni kile kile tangu jimbo halijaongezeka, hivyo basi tunaomba Serikali ichukue hatua maalum ya kuongeza fedha katika majimbo hayo yaliyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu tathmini iliyofanywa juu ya Taasisi za Muungano; napenda kuipongeza Serikali kwa kufanya zoezi hili. Hili ni jambo muhimu sana ili kujua mahitaji ya taasisi hizi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kuwa ni taasisi 20 ndio zilizofanyiwa tathmini, Iakini Mheshimiwa Waziri hakuzitaja. Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuzitaja taasisi hizi ili nasi tuzitambue kwa manufaa ya wananchi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano; napenda kutoa pongezi za dhati kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua hii ya kuwaelimisha wananchi wa Tanzania. Ni dhahiri kuwa mpaka hii leo baada ya miaka 58 bado wapo watu hawajui maana ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili haliwezi kufanikiwa kwa asilimia kubwa kutokana na vyombo vinavyotumika kueneza elimu hii. Kwa mfano wananchi wa vijiji hawawezi kuwa na redio, tv, mitandao ya kijamii au majarida yaliyotajwa katika hotuba hii. Hivyo ushauri wangu katika jambo hili ni kutafuta njia sahihi ya kuwafikia wananchi wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia nchi yanakwenda haraka sana. Nchi lazima iwe tayari kuchukua hatua za kukabiliana nazo. Ziko fedha nyngi duniani zinazotolewa kwenye nchi zinazozalisha hewa ya ukaa inayotokana na kutunza misitu. Nchi hii bado ina misitu mingi. Hivyo nashauri hamasa ya kutunza hii misitu na vijiji vinavyozungukwa na misitu hiyo zipewe fedha ili iwe hamasa kwao.

Mheshimiwa Spika, misitu mikubwa kama ya Kitonga na Nyang'oro mkoani Iringa ukipita wakati wa kiangazi utakuta moshi. Hii inamaanisha watu wanachoma mkaa. Hili likiendelea litaharibu zaldi mazingira na kusababisha ukame kuendelea. Serikali ione namna ya kuongeza ulinzi hata ikibidi kujenga kambi za ulinzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwenye miinuko na vilima vyote kwenye miji kama Morogoro, Iringa, Mwanza, Mbeya na kadhalika uzuiwe. Misitu hii inasaidia miji kupumua kwa maana tunapata *oxygen* nyngi. Binadamu na misitu tunategemeana. Wizara ione namna ya kufanya ili kuzuia kabisa kupima viwanja kwenye maeneo hayo. Nawasilisha.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dkt. Selemani Jafo, Naibu Waziri na wataalamu wa Wizara na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kwenye suala la umuhimu wa kubadilisha sheria na kurudisha eneo la *Half Mile* kwa wakazi wa vijiji vilivyomo katika mipaka ya Mlima Kilimanjaro ili washiriki kikamilifu kutunza mazingira ya Mlima Kilimanjaro.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, *Half Mile* ni eneo lenye upana wa kati ya 0.5-0.8 ya *mile*. Eneo hili lilikuwa linatenganisha Mlima Kilimanjaro na makazi ya watu. Eneo hili kwa upande wa majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo linajumuisha vijiji 40.

Mheshimiwa Spika, wakoloni wa Tanganyika walitumia sheria kandamizi kujimilikisha ardhi ya wana Kilimanjaro na rasilimali za msitu wa Mlima Kilimanjaro na kuwapora wana Kilimanjaro haki yao ya kufaidi rasilimali zao za asili.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 1941 wakoloni walianzisha Sheria ya *Half Mile Strip* kwa lengo la kuwapatia majirani wa msitu Kilimanjaro huduma za mazao ya misitu kama vile dawa za asili (ngesi), mboga za majani (mnafu) miti ya kujenga nyumba, kuni na majani ya ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, tofauti na malengo ya kuanzhishwa kwa eneo la *Half Mile*, kazi za kibinadamu zilisababisha uharibifu wa mazingira katika *Half Mile* na yale maeneo ya hifadhi kwa kukata miti, kupasua mbao, kuchoma misitu, kuchunga mifugo na kuendesha shughuli za kilimo ndani ya hifadhi. Hii ilitokana na kukosekana kwa usimamizi mahiri kutoka katika mamlaka husika Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baada ya uharibifu huu, Serikali ilisimamisha vijiji vyote 40 kutokutumia *Half Mile Strip* toka mwaka 2004, kwa sheria iliyoanza kutumika mwaka 2005. Hii ilitokana na kusainiwa kwa sheria ya kuziingiza *Half Mile Strip* za maeneo ya Moshi Vijijini na Rombo iliyotiwa sahihi na Marehemu Rais Mkapa tarehe 18/7/2005 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali tarehe 16.9.2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya zio hili, Serikali yetu iliondoa ile huruma ya wakoloni kwa Wana Kilimanjaro ya kutumia ile *buffer zone* ya *Half Mile*. Siku hizi hakuna cha *Half Mile* tena na ukikamatwa na maaskari wa KINAPA utakuwa na bahati mbaya sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wapiga kura wangu wamenituma niiombe Serikali ibadilishe sheria hii kwani baada ya kunyima watu wasitumie *Half Mile*, hii imesababisha matatizo makubwa ikiwa ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira ya msituni Kilimanjaro kwa kupanuka kwa shughuli za kukata miti ndani ya msitu ikifanywa na maharamia; kuongezeka kwa wanyama waharibifu wa mazao kwenye mashamba ya wakulima kama nyani, ngedere na kima kuingia kwenye mashamba ya wanakijji na kuharibu mazao.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2005 shughuli za wananchi kwenye *Half Mile* zilizua wanyama kuingia vijiji vya mpakani na ilikuwa hakuna uharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein alipotembelea Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 2008 akiambatana na Waziri wa Malasili Profesa Jumanne Maghembe wananchi walimweleza matatizo yaliyojitekeza baada ya Serikali kuunganisha eneo la Hifadhi la *KINAPA* na misitu ya hifadhi za asili.

Mheshimiwa Spika, baada ya ziara hiyo, Wizara ilikaa na kuigiza *TANAPA* (kwa barua yeny Kumb Na. CAB. 315/484/01/A ya tarehe 22.1.2008 ya Waziri Profesa Maghembe kwenda kwa Mwenyekiti wa Bodii ya *TANAPA*, na barua Kumb Na. CJA.246/374/01/42 ya tarehe 27.2.2009 ya Katibu Mkuu Dkt. Ladislaus Komba kwenda kwa Mkurugenzi wa *TANAPA*) wachore ramani upya na kutenga eneo la *Half Mile* liwe nje ya Hifadhi ya *KINAPA* kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo hayo hapo juu na kukumbushwa mara kwa mara na wadau wa maendeleo wa Mlima Kilimanjaro hadi leo ramani hiyo hajiatoka na sheria hii kandamizi kwa wananchi wa vijiji 40 vya mpaka na Mlima Kilimanjaro bado inawanyanya.

Mheshimiwa Spika, sheria kandamizi kama hii si nzuri na zinasababisha migogoro isiyo ya lazima baina ya wananchi na Serikali yao na uhifadhi wa mlima unawatenga wananchi wa vijiji jirani.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama mwakilishi wa wananchi, hata mimi naikataa kabisa sheria kandamizi kwa wapiga kura wangu na ninamwomba Waziri Jafo amshauri Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan aliangalie jambo hili kwa jicho la huruma kama alivyoelekeza Makamu wa Rais mwaka 2008 ili wananchi wawe sehemu ya kutunza mlima na kuzuia majangili wasiingie mlimani kukata miti na kuharibu mazingira ya Mlima Kilimanjaro. Wananchi wanaoishi vijiji vya mpakani wakielekezwa na kukabidhiwa maeneo ya kulinda, wanaweza wakawa walinzi bora bila hata kutumia bunduki.

Mheshimiwa Spika, sheria ikibadilishwa, *Half Mile Strip* inaweza kutumika kwa mafanikio makubwa chini ya usimamizi wa Serikali Kuu, Serikali ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji na kusaldia wananchi wa vijiji husika kuutunza mlima na kuboresha mazingira yake; kuwapatia wananchi huduma na kuinua uchumi wa wananchi, Wilaya, Mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, sheria ikibadilishwa, wananchi washauriwe kupanda miti ya muda mfupi kama *cypress, pine* na mikaratusi na aina nyinginezo zinazokua haraka kwa ajili ya nguzo za umeme, nguzo za ujenzi wa nyumba zikiwemo ghorofa, miradi kama hii iko Iringa. Rais akiruhusu hili, nchi nzima itanufaika kwani Kilimanjaro ina miundombinu bora ya kusafirisha hizi bidhaa na kuzisambaza zinakohitajika.

Mheshimiwa Spika, kama hatua stahiki hazitachukuliwa mapema, hali itakuwa tete sana miaka michache ijayo, na mazingira ya Mlima Kilimanjaro huenda yakaharibika zaidi.

Mheshimiwa Spika, *KINAPA* hawana watumishi wa kutosha wa kuulinda mlima na kupanda miti mingi ya kutosheleza kulinda mazingira ya mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

SPIKA; Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, na mtoa hoja ajijandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MZINGIRA: Mheshimiwa Spika, nami naomba niseme machache kutokana na yale ambayo yamezungumzwa, lakini zaidi nitajikita kwenye hili jambo la *NEMC*, jambo la Mazingira kwa ujumla na jambo la Muungano ambalo ni sehemu ya zao liliotuleta hapa baadhi yetu wengi.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mmoja nadhani wa mwanzo aligusia suala na *NEMC* na akasema kwamba *NEMC* wamekwenda, wameshafanya *assessment* na wameshatoa vibali, lakini bado wameweka zuio; na kibaya zaidi wameweka zuio kwenye baadhi ya miradi hasa miradi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka niseme katika hili kwamba *NEMC* ni taasisi ambayo inasimamiwa na inafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zote. Kama tutafika wakati *NEMC* tutaona mahali ambapo tutakwenda kuparuhusu pafanyike, ikiwa skuli, ikiwa kiwanda, ikiwa mgodi, ikiwa chochote kikiwa kinaelekeea kuharibu mazingira, kuchafua mazingira ambayo baadaye yanakwenda kuathiri maisha ya watu. Hapa ni lazima kwanza tujuue namna ya kufanya kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tu kuruhusu kwa sababu tu watu wanataka wafanye, kwa sababu mwisho wa siku mazingira yale yakiathirika, athari na lawama zinakuja kwa Serikali, hasa *NEMC* kama ambavyo imezungumzwa. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo tuwaachie *NEMC* waendelee kufanya harakati zilizopo kwa mujibu wa taratibu. Tukifika wakati tukaona sasa usalama wa wananchi upo vizuri, tutaruhusu tuone namna ambavyo itawezekana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la fedha za miradi ya mazingira hasa kwa upande wa Zanzibar. Fedha zinakwenda; na kwa sababu tunasema, kinachofanyika tunakiona katika pande zote mbili za Muungano. Kwa maana Zanzibar tunapokwenda kukagua tunaona miradi; na Bara pia tunapokwenda kukagua tunaona miradi, na utaratibu wa fedha unatoka kwa mujibu wa taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka tutoe wito. Changamoto iliyopo ni kwenye usimamizi na utekelezaji wa miradi hii. Ni kweli sisi ni sehemu ya wajibu wa kusimamia miradi hiyo, lakini tunao wenzetu tunaoshirikiana nao wakiwemo Halmashauri na wenzetu wa upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunataka tutoe wito kwa wenzetu wote ambao tunashirikiana nao, kwa sababu suala la uhifadhi wa mazingira, tunashirikiana Serikali zote mbili. Kwa hiyo, Halmashauri wafanye wajibu wao na wengine wanaosimamia hili watekeleze wajibu wao ili nasi tujue namna ya kufanya katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la changamoto ya Muungano. Sidhani kama tunaweza tukadumu kwenye Muungano kwa zaidi ya miaka 50, halafu ikawa changamoto ni nyingi kuliko mafanikio. Nikiwa naamini kwamba Muungano huu una mafanikio mengi sana kuliko changamoto, na kwa sababu changamoto nyingi au hizo ambazo inaitwa kero, nyingi tayari zimeshasawazishwa, zimeshatatuliwa. Zilizobakia zote, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, niwaambie Watanzania wote kwa ujumla, sasa hivi tupo kwenye harakati za kuweka vikao katika pande zote mbili za Muungano ili lengo na madhumuni, tuhakikishe kwamba changamoto zinazotatiza katika Muungano zinamalizika na zinatatulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukasema tunaenda katika Muungano huu tusiwe na changamoto. Lazima tutakuwa nazo kwa sababu tunaohusika na tunaokubaliana ni binadamu, lakini tunapoona kuna changamoto na tukiona

hii inakwenda kutatiza na kuliweka Taifa mahali pabaya, tunakaa, tunakutana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaambie Waheshimiwa kwamba, hata hizo changamoto ambazo bado tunazo, Serikali ya Jamhuri ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari tumeshakaa, tunaendelea kukaa na tutakaa kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto zote ambazo zinagusia katika Muungano, ili katika miaka tunayokwenda, tukarithishe vizazi vijavyo Muungano ambao hauna changamoto.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, kanuni ya 34 (5) inanipa fursa ya kuongeza muda kwa kadri nitakavyoona inafaa ili nimalize ratiba ilio mbele yangu hapa.

Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, mtoa hoja anahitimisha hoja yake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa, lakini awali ya yote naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uzima. Nimeweza kuwasilisha hotuba yangu hapa, lakini nashukuru sana kwamba Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuichangia.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake makini na madhubuti sana ambao umetuwezesha kufanya kazi zetu ziende vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muungano na Mazingira, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli wasemavyo vijana ameupiga mwangi sana Mama Samia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Suluhu Hassan. Sisi ametuwezesha kuhakikisha kazi yetu inafanya vizuri katika ushiriki wake wa pamoja kama kuiongoza nchi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana, kama alivyosema awali, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa msaada mkubwa wa kuhakikisha katika upande wa Muungano, akishirikiana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Makamu wa Rais ambaye ni msimamizi wangu mkuu katika Ofisi yangu, amenisaidia sana kutimiza majukumu yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa, kwa kweli Waziri Mkuu wetu sisi ni mwalimu kwetu, amekuwa kiongozi makini na hodari sana kutuwezesha tumeweza kufika hapa. Nakushukuru wewe na timu yote ya wasaidizi wako waliokuwa karibu kuhakikisha mambo ya Bunge yanakwenda vizuri na leo hii tunakwenda kuchakata bajeti yetu ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru familia yangu kwa ujumla, kwa kweli wamenipa msaada mkubwa sana kuhakikisha natimiza vyema majukumu yangu. Halikadhalika, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa kuniombea muda wote wakati natimiza majukumu yangu nikiwa katika nafasi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu tuna uchache wa muda, lakini napenda kushukuru Kamati zote hizi mbili ambazo zimewasilisha maoni yake hapa. Kwa ufupi tu niseme kwamba, Ofisi yangu inapokea maoni yote. Kwa kweli maoni yote yameelekeza kwa ajili ya kuhakikisha Wizara hii inafanya na kutimiza majukumu yake vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba ya Sheria imeshauri mambo mengi sana kuhusu Muungano, hili ni jukumu lake. Hivyo naomba niseme jambo moja; kwanza kipekee niishukuru Kamati ya Katiba na Sheria. Kamati hii ndani ya mwaka mmoja imeweka *legacyya* kuhakikisha hoja 11 za Muungano zinatatalika. Kwa dhati niseme wazi kabisa,

imefanya kazi kubwa sana na Wajumbe wa Kamati. Maoni kama mlivyowasilisha hapa, kazi yetu ni kwenda kuyachakata, kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Kamati ya Mazingira, imekuwa mwalimu na kiongozi katika upande wa Mazingira muda wote. Naomba nikwambie; katika Kamati, Kamati hii imekuwa ni mwalimu na mwelekezi. Maoni yote ya Kamati yalivyozungumzwa, kama nilivyosema, muda wenyewe ni mfupi hapa, mliyoyasema kazi yetu ni kuyatekeleza. Mimi Jafo na watu wangu ni nani tushindwe kutekeleza maoni ya Kamati? Jukumu letu kubwa ni kwenda kufanya kazi katika maoni yote kama Kamati ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Hotuba yangu leo hii imechangiwa na Wajumbe takribani 13. Siwezi kuwataja wote kwa ujumla wake, lakini niseme kwamba ile michango yote kama nitakayotoa hapa kiufupi na Naibu wangu aliyotoa hapa, mengine yatakuja kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo naomba niseme kwa ujumla wake. Kuna maombi mahsus ya kwenda kushughulikia hoja za Muungano zilizobakia. Naomba niseme kwamba tulikuwa na hoja takribani 25. Katika kipindi hiki cha uchakataji wa hoja za Muungano, tulipofika mwaka 2020 hoja saba ziliweza kutatuliwa kati ya hoja 25, tukabakiza hoja 18. Naomba niwashukru Viongozi Wakuu, ndani ya kipindi hiki cha mwaka mmoja kama nilivyosema, tumeweza kutatua hoja 11. Ni *legacy* ya kwanza imewekwa katika utatuzi wa hoja za Muungano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie wote, imani yetu na kazi yetu kubwa tutakwenda kufanya, sisi hatulali, tutahakikisha mionganini mwa changamoto, zile hoja saba za Muungano tutakwenda kuzifanyia kazi. Halikadhalika, na hata zile ambazo tumezifanyia kazi, tutakwenda kuhakikisha tunaweka utaratibu mzuri wa kisheria na kila kitu. Lengo kubwa hoja zile ambazo imefanyiwa upembuzi ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu amezungumza hapa masuala ya kikanda na Kimataifa, ni miongoni mwa hoja ambayo imefanyiwa kazi mwaka 2020. Kazi yetu kubwa sasa hivi ni kuweka utaratibu mzuri kama utaratibu wa TFF na wenzake, yote haya ni masuala ya ushiriki katika masuala ya kikanda na Kimatiafa. Tutaya fanya haya vizuri. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tutakwenda kuweka katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Wabunge mbalimbali hasa kutoka Zanzibar, kwa sababu mmekuwa mkitoa hoja; Mzee wa Mtambwe kule na maeneo mengine; dada yangu wa Pandani na maeneo mengine, wote kwa ujumla wake, mmenisaidia sana kuhakikisha wakati natimiza majukumu yetu, kuna masuala ya kiuungano na masuala ya kimazingira. Kama tunavyofahamu kwamba masuala ya kimazingira yapo huku upande wa Bara na Zanzibar kuna Wizara ya kimazingira, lakini Mazingira ni *crosscutting issue*, huwezi kutofautisha na upande mmoja. Ndiyo maana hata baadhi ya miradi yetu mingine tunaitekeleza kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Wabunge wote mlchangia humu ndani, kwa upande wa kimazingira nitashirikiana na mwenzangu Waziri wa Zanzibar katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais anayeshughulika na masuala ya Mazingira. Tutaenda kujadiliana kwa pamoja. Kwa mfano, siku nilipoenda kwa ndugu yangu Sumai, pale Nungwi, kweli ukifika pale unakuta hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alichokisema ni kweli. Nami naomba niseme, nimekuta kuna shida kubwa ya maji, na ndiyo maana katika utashi huu hata Zanzibar wana mradi mkubwa sana wa maji, lakini walikuwa wana changamoto ya upatikanaji wa suala zima la mchanga na kokoto. Tumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hoja ile sasa imepata ufumbuzi kuruhusu mchanga uende kule kwa ajili ya miradi ya maji kwa sababu kuna changamoto ya mchanga katika utekelezaji ule.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla wake miradi hii mingine ya kisekta naomba niwahakikishie, kwamba tutashirikiana kwa pamoja kwa kuwa hii ni nchi yetu sote. Naomba niwaambie ndugu zangu uongozi ni dhamana. Licha ya kufanya kazi kama unatenda kazi lakini uongozi ni sehemu ya ibada. Unapofanyakazi kwa kuwahudumia watu na kupata tija na kupata mafanikio makubwa na wewe Mungu anakulipa. Kwa hiyo naomba niwahakikishie, kwamba yale yote ambayo yamejadiliwa hapa tutajitahidi kushirikiana kwa pamoja kwa mustakabali mpana wa Taifa letu hili. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

MWENYEKITI: Kamati ya Matumizi. Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

KAMATI YA MATUMIZI

KITABU CHA PILI MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na
Mazingira**

Kifungu 1001 - *Administration and Human
Resources Division* Sh. 4,765,707,470

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hili ndiyo fungu lenye mshahara wa Waziri lakini hapa mbele hatujapata majina ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kupata ufanuzi wa kisera kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. (Makofi)

Kwa hivyo sasa nitaendelea na utaratibu wetu ule wa kawaida kwa sababu katibu ameshasoma, sasa nitawahoji. Kifungu kinaafikiwa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 492,795,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Division</i>	Sh.1,126,620,000
Kifungu 1004 - <i>Government Comm. Unit</i>	Sh. 367,680,000
Kifungu 1005 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 485,395,000
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 603,148,000
Kifungu 1007 - <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh. 412,780,000
Kifungu 1008 - <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 653,016,000
Kifungu 2001 - <i>Union Secretary</i>	Sh.1,682,531,000
Kifungu 5001 - <i>Environment</i>	Sh.7,590,655,530

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 26 – Makamu wa Rais

Kifungu 1001 - *Administratopn and Human Resources Division* Sh. 12,974,292,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Division* Sh. 2,820,000,000
Kifungu 5001 - *Environment*..... Sh. 19,141,697,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Tukae. Mtoa hoja taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati na limekamilisha kazi yake; naomba Taarifa ya Kamati ikubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoaafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Nadhani walioafiki wameshinda. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inayohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na baada ya Bunge kuhojiwa hoja hii imepita kama ilivyokuwa imeletwa. *(Makof)*

Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Naibu wake, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Vilevile ninawapongeza watendaji wenu ambaao baadhi yao wapo humu Bungeni tunawapongeza kwa kazi nzuri na pongezi hizo zinatokana na kwamba Waheshimiwa Wabunge kuweza kuitisha hoja yenu bila kushika vifungu hapa ni dhahiri kwamba wameikubali kazi yenu. Kwa hiyo nawapongeza sana. *(Makof)*

Pia nawatakia kila kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeyaahidi katika bajeti yenu ya Mwaka 2022/2023 tunawatakia kila kheri katika utekelezaji baada ya Bunge kufanya kwa sehemu yake. Na pia nichukue fursa hii kuzishukuru sana kamati zetu mbili, Kamati ya Katiba na Sheria tunawashukuru sana sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa niaba yetu sisi sote Wabunge hapa ahsanteni sana lakini pia Kamati yetu ya Viwanda Biashara na Mazingira tunawashukuru sana pia kwa maoni ambayo mmeatoa hapa bila shaka hayo ndiyo yaliyowaongoza Waheshimiwa Wabunge kuweza kutoa maoni ambayo kama Mheshimiwa Waziri alivyosema wameyapokea yote na yale yaliyokuwa yanahitaji ufanuzi watatoa ufanuzi kwa maandishi kama ilivykawaida yetu. *(Makof)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, niwashukuru pia Wabunge wote ambao mmepata fursa ya kuchangia kwa sababu lengo lenu lilikuwa ni kuhakikisha tunalinda mazingira yetu lakini pia tunaweka mazingira mazuri ya kuimarisha Muungano wetu. Kwa hiyo ninawashukuru pia kwa michango yenu mliyoitoa.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyokuwa nimetangaza mwanzo, nilisema leo kutakuwa na *Iftar* ambayo inafanywa na ndugu zetu kutoka Wasafi, na Mkurugenzi Mkuu yupo hapa. Sasa nimekumbushwa hapa mbele kwamba kuna meneja mmoja wa *WCB* ambaye yupo humu ndani na lilikuwa sijamtangaza. (*Makofi*)

Kwahiyo katika ile orodha ya wageni, lakini yeze ni mwenyeji, ila nimbambue kwamba na yeze ni Meneja wa Wasafi *WCB*, Mheshimiwa Hamis Taletale. (*Makofi*)

Ahsante sana nadhani hiyo itakuwa imetoa ishara kwamba humu ndani huwa kuna makofi fulani hivi kwa hiyo ndugu yetu Diamond makofi uliyopigiwa ni *special* ni makofi ya heshima kubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka...

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, mgeni wangu mbona umemsahau?

SPIKA: Ni kweli kama aliyesema kwamba si Itifaki ila si utaratibu mzuri na huyu ni Mbunge mzoefu, ila ngoja nimpe tu hiyo nafasi. Sijui ile karatasi yake aliyandika hapa ipo wapi, huu siyo utaratibu jamani leo ni vile tu nimefurahi kwamba kuna *Iftar* baada ya hapa lakini mambo huwa hayafanyiki kwa stahili hii ama kwa namna hii. (*Makofi*)

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ambaye ni ndugu yake kutoka Zanzibar, ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge ndugu yake huyu anaitwa Dkt. Mwatima Abdallah Juma ambaye pia ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwenyekiti wa *Tanzania Organic Agriculture Movement* ambayo inaitwa Mwavuli Kilimo Hai Tanzania. Karibu sana; na mnaweza kuona namna walivyofanana. Kwa hiyo si tu mgeni lakini ni dada yake. Karibu sana dada wa Mheshishimiwa Asha Abdullah Juma ambaye humu ndani tunamuita Mshua, karibu sana. (*Makofi*)

Haya, Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 12.12 Jioni Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi
Tarehe 28 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*